

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 23 APRILI, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA SHERIA, KATIBA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Huduma za Jamii kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. JOB Y. NGUDAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. MOHAMED A. CHOMBOH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. PINDI H. CHANA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA SHERIA NDOGO):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Sheria Ndogo kwa Mwaka 2009/2010.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka 2009/2010.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ilikuwa ndio wakati mahsusi wa kuwasilisha Taarifa za Kamati zetu zote 17. Kama mnavyojua ni mahitaji ya kanuni zetu kwenye 114(15) kwamba “Itakuwa ni lazima kwa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti”.

Lakini hakuna aliyesimama kutaka kuomba taarifa yoyote ijadiliwe. Kwa hiyo tunaendelea. Lazima hizi kanuni muwe mnazisoma, maana yake kama hamzisomi basi tena. Kwa hiyo, tunaendelea. (*Makofi*)

**MASWALI NA MAJIBU**

**Kuutazama Upya Muundo wa Utumishi**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kuutazama upya Muundo wa Utumishi kwa Watafiti hapa nchini kwa lengo la kuuboresha:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Muundo mpya Watafiti waliopo Kituo cha Uyole (Kilimo na Mifugo)?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Utumishi unaotumika kwa Watafiti wote wakiwemo wale wa Uyole, ulitolewa mwaka 2002 kupitia Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 5 wa mwaka 2002. Kwa sasa Serikali inaendelea na mchakato wa kuhuisha Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Watafiti wote wakiwemo wale wa Uyole.

Zoezi hili linafanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Baada ya hatua hii, utawasilishwa katika Baraza Kuu la Wafanyakazi kwa ajili ya kupitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Na. 19 ya Mwaka 2003, ili utekelezaji wake uanze katika mwaka wa fedha 2010/2011.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya kuuliza swali la nyongeza nilitaka niseme tu kidogo kwamba mimi nawakilisha jimbo la Mbeya Mjini na sio Vijijini.

Baada ya hapo naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza nafurahi kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa ni karibu mwaka mzima sasa toka ilipotolewa ahadi ya kujaribu kuangalia upya muundo huu wa Watafiti hawa. Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa ni wakati muafaka tunapotekeleza kilimo kwanza kwa *Fast Track* madaraja haya ya Watafiti ili waweze kupata kile ambacho wanastahili kwa wakati huu.

Swali la pili, kwa kuwa Watafiti hawa ni muda mrefu sasa wamekuwa wakilipwa tofauti kabisa na wenzao walio katika Vyuvo Vikuu.

Je, Serikali baada ya kuurekebisha Muundo huu itakuwa tayari kulipa nyongeza ya mishahara ambayo walikuwa wananyimwa kutokana na Muundo ulivyokuwa umekaa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumwomba radhi Mheshimiwa Mpesya kwa kumtambua kama Mbunge wa Mbeya Vijijini. Baada ya hapo naomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba maelekezo ya kuhuisha Muundo yalitolewa muda mrefu sana lakini mchakato wa kuhuisha Muundo nao una taratibu ndefu sana. Kwanza ni lazima huu utaratibu uanzie katika Taasisi ndiyo ambayo unapenda muundo wake uhuishwe. Na wakishatoa mapendekezo ni lazima upitie katika Baraza la Wafanyakazi la Taasisi husika ndipo uwasilishwe Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuupitia na uweze kuwasilishwa katika Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kufurahi na kumhakikishia Mheshimiwa Mpesya kwamba taratibu zote hizi sasa hivi zimekamiliika tunachosubiri sasa hivi ni kuhuisha Muundo huu katika Baraza Kuu la Wafanyakazi ambalo tunategemea litafanyika kati ya tarehe 5 na 7 mwezi Mei kule Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba Watafiti walikuwa wanalipwa tofauti na watumishi wengine wa Vyuo Vikuu na kwamba baada ya kuhuisha muundo alikuwa anapendekeza kwamba tualipe ma malimbikizo. Kwa kweli katika Utumishi wa Umma hatuna utaratibu huo.

Na. 107

### **Kuimarisha Maslahi ya Wauguzi na Wakunga**

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, asilimia 60 ya wafanyakazi katika Sekta ya Afya nchini ni Wauguzi na Wakunga ambao hufanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuimarisha maslahi ya watumishi hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa jimbo la Kiwani, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Fani ya Wauguzi na Wakunga ina miundo ya Maendeleo ya Utumishi mitatu ambayo ni:-

- (i) Muundo wa Wauguzi unaohusu wale wenye elimu ya ngazi ya cheti.

- (ii) Muundo wa Maafisa Wauguzi Wasaidizi ambao ni wale wa ngazi ya stashahada.
- (iii) Muundo wa Maafisa Wauguzi wenye shahada ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mazingira magumu waliyonayo Wauguzi pamoja na watumishi wengine wa Kada za afya. Katika kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikiboresha maslahi yao kila mwaka kutegemea ukuaji wa uchumi na ongezeko la mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na dhamira ya dhati ya kuboresha maslahi ya Wauguzi, mishahara yao imekuwa ikiboreshwa mara kwa mara.

Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitano yaani kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010 mishahara ya kada hizi imepanda kama ifuatavyo:-

- Mishahara ya kuanzia kazi kwa kada ya Wauguzi/Wakunga imepanda kutoka shilingi 88,680 hadi shilingi 201,870 kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 128, wakati mishahara ya kuingilia ya watumishi wengine waliokuwa wanalipwa mishahara inayofanana kwa wakati huo, imepanda kutoka shilingi 88,680 hadi shilingi 151,240 kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 71.
- Mishahara ya kuanzia kazi kwa Maafisa Wauguzi Wasaidizi imepanda kutoka shilingi 120,300 hadi shilingi 329,680 kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 174 (174%) wakati mishahara ya kuingilia kwa watumishi wengine waliokuwa wanalipwa sawa na ambao wana sifa ya stashahada imepanda kutoka shilingi 120,300 hadi shilingi 201,870 kwa mwezi sawa na ongezeko la asilimia 68.
- Mishahara ya kuanzia kazi kwa Maafisa Wauguzi wenye shahada ya kwanza ni shilingi 454,970 kwa mwezi wakati mishahara ya kuanzia kazi kwa wahitimu wengine wenye shahada ya kwanza katika fani kama vile Uchumi, Uhasibu na Utawala ni shilingi 322,460 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa mishahara ya Wauguzi imekuwa ikipanda na kupewa kipaumbele ikilinganishwa na ile ya kada nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi wake, wakiwemo Wauguzi na Wakunga, kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, sera na vipaumbele vyake ili kwenda na wakati.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba nimwulize.

Kwa kuwa kuna miundo mitatu ya Wauguzi. Je, ni lini Serikali itaanzisha Kurugenzi ili kutatua tatizo lao? Hilo la kwanza.

La pili, je, ni lini Wauguzi watapatiwa *risk allowance* na *allowance* nyingine ili waweze kutekeleza kazi zao vizuri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwamba ni lini Serikali itaanzisha Kurugenzi ya Wauguzi. Kwa kweli siwezi kutamka lakini kila Wizara yenyewe ndiyo inapanga miundo yake kutegemeana na mahitaji yake. Lakini ndani ya Wizara ya Afya ipo Idara ambayo inashughulikia kabisa masuala ya Wauguzi.

Mheshimiwa Spika, kwamba ni lini Wauguzi wataanza kulipwa posho za kufanya kazi katika mazingira magumu. Kama tulivyozungumza mwanzo kwamba posho nyingi ziliingizwa katika mishahara ya watumishi, lakini bado zipo posho ambazo Wauguzi wanaendelea kulipa kulingana na ugumu wa kazi zao na mazingira yao ya kazi.

Na. 108

### **Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. DR. BANILITH SATANO MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya sababu zinazosababisha nchi za Afrika kuendelea kuwa maskini ni uharibifu wa mazingira; na kwa kuwa zaidi ya asilimia themanini (80%) ya wananchi waishio mijini na vijijini hutumia mkaa na kuni kama nishati vitu ambavyo vinasababisha uharibifu wa mazingira na hali inayoleta majanga ya njaa mara kwa mara.

Je, nini mkakati wa Taifa wa kupunguza matumizi ya mkaa mijini na vijijini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mkaa na kuni kwa ajili ya nishati ya kupikia ni changamoto kubwa ambayo nchi yetu inakabiliana nayo, hasa kutokana na uharibifu

mkubwa wa misitu ya asili. Inakadiriwa kuwa asilimia 90 ya nishati ya kupikia nchini inatokana na kuni na mkaa. Hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa utowekaji wa misitu unaokadiriwa kuwa zaidi ya hekta 92,000 hukakwa kila mwaka. Aidha, kwa sehemu kubwa shughuli za uchomaji mkaa zinafanywa kwa kukata miti katika misitu na sio mashamba ya miti iliyopandwa rasmi kwa ajili ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, mikakati inayotumika kupunguza matumizi ya mkaa na kuni mijini na vijijini imejielekeza katika kupata ufumbuzi wa upatikanaji wa nishati mbadala na nishati jadidifu. Juhudi hizi zinafanywa kwa njia mbalimbali na baadhi ya juhudi hizi ni kama ifuatavyo:-

1. Kuhimiza matumizi ya gesi asilia; kama tutakumbuka mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali iliondoa ushuru wa bidhaa na kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi ya kupikia na mitungi ya gesi ili kuhamasisha matumizi yake pamoja na bidhaa zile za moto poa.
2. Kuhimiza matumizi ya nishati ya jua, upepo na bayogesi.
3. Kuhamasisha makampuni, viwanda na taasisi mbalimbali kutumia nishati mbadala na kama matumizi ya kuni yatafanyika, basi kila taasisi iwe na mashamba yake ya miti kwa ajili ya nishati.
4. Kuanzisha wakala wa umeme vijijini na mfuko wa usambazaji umeme vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme vijijini.
5. Kuendeleza utafiti ili kuwezesha makaa ya mawe kutumika kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kukiri kuwa pamoja na juhudi hizi, ni wazi kuwa hadi sasa hakuna nishati mbadala ambayo imeweza kuenea kwa kiwango kikubwa na hivyo kutumiwa na wananchi wengi, kama inavyotegemewa, na moja ya sababu kubwa ni gharama kubwa ya uwekezaji wa awali.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini wa Wizara ya fedha na Uchumi itaendelea na jitihada za kuongeza motisha na kupunguza kodi na teknolojia hizi ili kuweza kutumika na wananchi wengi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha tena wakuu wa Mikoa na wakuu wa wilaya kuendelea kusimamia kwa vitendo agizo la Mheshimiwa Makamu wa Rais la mwaka 2006 la Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, unaozitaka taasisi na watumiaji wengine wa kuni na mkaa kuwa na mashamba yao ya miti na kudhibiti ukataji miti kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa; na vijiji kuwa na mashamba mahsusi ya miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha nishati inapatikana kwa ajili ya kupikia na shughuli zingine lakini mijini ambako umeme unapatikana, gesi inapatikana na ambako wanaishi watumishi ambao wana hali nafuu kuliko vijijini bado kuna matumizi ya mkaa na hasa watumishi wanaokaa kwenye nyumba za Serikali, viongozi wakubwa bado wana matumizi ya mkaa.

Je, Serikali itakuwa tayari kuzuia matumizi ya mkaa kwa watumishi na viongozi wanaoishi kwenye nyumba za Serikali na kuweka ushuru kwa mkaa unaoingia kwenye miji mikubwa ili kukatisha tamaa matumizi ya mkaa na watu waweze kutumia nishati zilizopo?

Swali la pili, kulikuwa na kauli ya kata mti panda mti. Je, Serikali itakuwa tayari kufanya tathimini mpango huu wa kata mti panda miti ikilinganisha na uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa miti ya asilia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana kwa sababu kwa kweli suala hili ni changamoto kwa nchi yetu lakini kujibu tu maswali yake mawili kwanza suala la kuzuia. Mimi nadhani ili tuwasaidie watumishi wetu wa Serikali na wanaishi wanaoishi maeneo ya mijini kwa ujumla ni vizuri tukawasaidia katika kuwawezesha katika kupata suluhisho mbadala.

Kwa hiyo sisi tunadhani kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati nikuona watumishi hawa wote wa Serikali na wale wa mashirika binafsi tukaweza kuhamasisha waajiri wao kuweza kutoa fursa ya mikopo ili waweze kuingia katika nishati ya kupikia kwa kutumia gesi asilia.

Sote tunajua gesi asilia ni salama na si hatari kama ilivyokuwa inadhaniwa na watu wengi. Tutaendelea kutoa elimu na kuona kwamba fursa za mikopo kama tulivyofanya katika kutoa mikopo katika mabati ya kujengea basi tutoe mikopo kwa ajili ya majiko na mitungi kwa watumishi wetu na wananchi wengi walioko mijini waweze kutumia gesi hii asilia.

Lakini pili, nampongeza sana kwa mkakati huu wa kata mti panda mti. Sisi tunasema kabla hujakata miti upande miti na si mti mmoja. Panda miti mingi na ndipo ukate. Kwa hiyo nasema kwamba tutaendeleza jitihada hizo lakini kwa kusimamia na kuonesha kwamba wale wanaoingiza mikaa mijini waoneshe mikaa hiyo inatoka kwenye mashamba rasmi kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Taasisi za Umma kama Magereza na



mashule ni miongoni mwa taasisi zinazoongoza sana katika ukataji wa miti kwa ajili ya matumizi ya mkaa na kuni; na kwa kuwa Waziri amekiri hapa kwamba safari ya kupata nishati mbadala bado ni ndefu; na kwa kuwa taasisi hizi muundo wake unatoa fursa ya kufanya kampeni nzuri kabisa ya kukata mti panda miti. (*Makofi*)

Je, Serikali imejipanga vipi kutumia fursa hii ili kuanza kukidhi haja ya kupunguza tatizo hili wakati tunatafuta nishati mbadala?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**  
Mheshimiwa Spika, ni kweli taasisi mbalimbali na hasa taasisi za ulinzi na mashule nyingi zinatumia nishati mbalimbali za kuni lakini pia taasisi hizo tayari zimeshajiingiza katika matumizi ya nishati mbadala. Tunajua magereza yetu sasa hivi wanatumia baogesi kwa kutumia kinyesi cha binadamu. Lakini tunajua kwamba taasisi hizo pia zimejitika katika jitihada za kupanda miti kwa ajili ya nishati hizo. Sisi tunasema kwamba tutaongeza fursa zaidi na kutoa elimu zaidi ili kuhakikisha taasisi hizo zinakuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza jitihada hizi za kutumia nishati mbadala. (*Makofi*)

Na. 109

### **Wagonjwa Kutakiwa Kulipia Huduma Hospitali ya Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa kero ya wagonjwa kusumbuliwa na kutoa chochote hata kabla ya kupatiwa huduma wanapokwenda Hospitali. Vituo vya Afya, Zahanati nyingi zimeripotiwa mara kwa mara kwenye maeneo ya nchi yetu likiwemo pia katika hospitali ya Wilaya ya Kahama hususan kitengo cha Uzazi na Huduma kwa Watoto:-

(a) Je, tatizo hili limeripotiwa kuwa sugu katika hospitali ngapi hapa nchini?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inakomesha kabisa tabia hiyo kwenye vituo vyote vya huduma kwa wagonjwa hapa nchini pamoja na hospitali ya Wilaya ya Kahama?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika vituo vya kutolea huduma za afya, baadhi ya wagonjwa husumbuliwa na baadhi ya watendaji katika vituo hivyo kwa kuombwa kutoa chochote hata kabla ya kupatiwa huduma. Serikali haina idadi ya hospitali zinazotoa taarifa ya wagonjwa kusumbuliwa kwa kutoa chochote hata kabla ya kupatiwa huduma.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka taratibu za kushughulikia makosa mbalimbali pamoja na tabia ya kuomba chochote kwa wagonjwa yanayofanywa na watendaji wake katika vituo vya kutolea huduma ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Kahama. Taratibu hizo ni kama ifuatavyo:-

·Kuanzisha kamati za Maadili kwenye Vituo vyote vya kutolea huduma ili kusimamisha maadili na utendaji wa watumishi wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii.

·Kuweka sanduku la maoni kwa ajili ya kuweka malalamiko ikiwa pamoja na majina ya watumishi wanaowadai wagonjwa fedha kabla ya huduma na hasa katika huduma ya uzazi na mtoto.

·Kuundwa kwa Mabaraza ya Taaluma za Afya ambayo pamoja na kazi nyingine yana wajibu wa kuchukua hatua za nidhamu kwa watumishi wa afya wanaobainika kufanya matendo ambayo ni kinyume cha maadili ya taaluma zao.

·Kupeleka malalamiko na taarifa katika ofisi za TAKUKURU katika wilaya zote ili kuhakikisha kuwa vitendo vyote vya rushwa ikiwemo tabia ya kuomba chochote kutoka kwa wagonjwa kinachofanywa na watendaji katika vituo vya kutolea huduma za afya vinashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi kutoa taarifa kwa uongozi wa vituo husika pale wanapotendewa jambo lolote kinyume na utaratibu ikiwa ni pamoja na kuombwa chochote kwa ajili ya huduma ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Aidha, naomba niwafahamishe kuwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Afya ya (2007), huduma za uzazi na huduma za afya kwa watoto chini ya miaka mitano ni kati ya huduma zinazotolewa bila malipo katika vituo vya Serikali. Hivyo yoyote anayedaiwa kuchangia huduma hizi katika vituo vya serikali anatakiwa kutoa taarifa kwenye uongozi wa kituo cha huduma au katika mamlaka husika ili hatua za kinidhamu zichukuliwe.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu la msingi la swali langu Serikali imekiri kabisa kwamba tatizo la wagonjwa kuombwa chochote kabla hata ya kupewa huduma lipo. Na kwa kuwa licha ya Serikali kuweka taratibu za kuhakikisha kwamba malalamiko dhidi ya vitendo hivyo yanaifikia Serikali taratibu hizo imedhihirika kwamba taratibu hizo hazifanyi kazi yoyote na hasa katika Wilaya ya Kahama.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhakikisha kwamba tatizo hili linatoweka na kero kwa wagonjwa hususan wakina mama wajawazito, watoto na wazee linatoweka kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge na kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi,

Serikali kweli imekiri. Lakini vilevile katika jibu langu la msingi nimesema Mabaraza mbalimbali na juhudi mbalimbali nimezianisha ambazo zinachukuliwa ili kuhakikisha kwamba suala la kuwaomba pesa wanapokwenda kupata huduma linakomeshwa.

Lakini si kweli kwamba haya mambo yote ambayo tumeyachukulia hayafanyi kazi kwa sababu katika Mabaraza haya wako watumishi ambao wamefukuzwa kazi, wengine wamepewa onyo kali. Lakini nitakachokisema hapa kwamba tunapokuwa tunapita katika hospitali zetu huwa tunalazimisha Wakurugenzi wawape watendaji wao vitambulisho na wawe wanavaa ili wanapotoa huduma na ikitokea kwamba ameomba rushwa au amekwenda kinyume cha utaratibu basi mgonjwa aweze kumtambua na kuweza kushtaki mahali panapohusika.

Lakini hata hivyo wale wote wanaotoa huduma za afya sasa hivi ni marufuku kuomba pesa au chochote kile kabla hajampa huduma na Serikali kwa kweli haitamwonea huruma mtu yoyote atakayefanya hivyo na hatua kali itachukuliwa ikiwemo na kufukuzwa kazi.

Na. 110

### **Ukarabati wa Hospitali ya Taifa Muhimbili**

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO** aliuliza:-

- (a) Je, ni lini ukarabati wa Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Muhimbili ulianza na utakamilika lini kwa gharama gani?
- (b) Je, Mkandarasi wa ukarabati huo ni nani na amefikia hatua gani kwa sasa?
- (c) Je, Ukarabati huo unahusisha majengo yote katika Hospitali hiyo na gharama za ukarabati huo zinabebwa na nani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassani Chande Kigwalilo Mbunge wa Liwale lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Muhimbili ulianza Machi, 2003 na ulipangwa kukamilika katika kipindi cha miezi 34 hivyo ungekamilika mwaka 2006. Hata hivyo ukarabati huo ulikamilika mwezi Aprili, 2009. Gharama ya mradi kulingana na Mkataba ilikuwa ni Shilingi za Kitanzania bilioni (10,136,258,273.49). Gharama ya ukarabati iliendelea kuongezeka kutokana na mabadiliko ya bei ya vifaa vya ujenzi pamoja na kazi za nyongeza na muhimu zilizokuwa zinajitokeza kadri ujenzi ulivyokuwa unaendelea. Hivyo hadi kukamilika ukarabati huo umegharimu kiasi cha Sh. Bilioni (15,511,447,105.44). kukiwa na ongezeko la jumla ya Sh. Bilioni (5,375,188,831.44) juu ya gharama za awali.

(b) Mkandarasi wa ukarabati huo ni *M.A. Kharafi & Sons AS Nomerco Construction (JV)*, na kama nilivyoeleza kwenye kifungu (a) hapo juu kazi za ukarabati zimekamili na Mkandarasi yupo kwenye kipindi cha uangalizi (*Defect Liability Period*).

(c) Mheshimiwa Spika, Ukarabati ulihusisha karibu Majengo yote ya Hospitali ukiondoa jengo la Utawala/Mapokezi na Maabara. Gharama za ukarabati wa Hospitali ya Taifa Muhimbili zilibebeba na Serikali; asilimia 46 ikiwa ni mkopo kutoka *OPEC Fund*, asilimia 31.4 mkopo kutoka *BADEA* na asilimia 22.6 ikiwa ni fedha za Serikali.

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza ukarabati ambao umefanywa katika hospitali hiyo pamoja na kwamba fedha zilizotumika ni nyingi lakini inaonesha kwamba haijaleta tasfiri halisi kwa mwananchi yoyote akifika pale amerahisishwa kitu cha aina fulani. Kwa hiyo, mgonjwa anapata shida sana kujua wapi ofisi ya kitu fulani iko. Je, ukarabati huo mpaka kufikia hali hii kweli ulifanywa kwa kushirikiana na wataalam wahusika na wale ambao wanahusika na hospitali hiyo ili wajue nini cha kufanya?

La pili, tuna wataalam wengi sana na hasa kipindi hiki ambacho nimejaribu kuwa mimi ni mteja na mgonjwa wao na nimekuta maeneo mengi sana hasa kwa ofisi za wataalam mpaka sasa hivi unakuta ofisi hizo ni finyu na ziko vichochoroni na hata ukienda kwa Mkurugenzi unaingia kwenye uchochoro kabisa. Sasa hawa wataalam ambao wanafanya katika mazingira magumu, hakuna njia ya kufanya ili kuboresha ofisi zao ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi kuliko hivi sasa wanapofanya kazi katika mazingira magumu kama fundi cherahani mahali pamoja na Sekretari wao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama namwelewa vizuri anachozungumzia ni kwamba unapokwenda Muhimbili hakuna maelezo yanayokueleza kama vile kibao kinachokueleza kwamba ofisi fulani ipo mahali fulani. Lakini kama anazungumzia suala zima la kuboresha hospitali ya Muhimbili naweza kusema kwamba mtizamo wa haraka haraka mtu yoyote anayeweza kwenda pale anaweza kuona kwamba hali ya Muhimbili majengo yaliyokuwepo miaka miwili au mitatu nyuma kwa kweli ni tofauti sana na kwa kweli yameboreka. Lakini kama anamaanisha kwamba kumwezesha mtu kufika pale mimi nachukua ushauri wake na tutazingatia hilo ili tuweze kuona kwamba watu wanaweza kufika maeneo fulani bila kuwa na mzunguko. Lakini tulipokuwa tunafanya ukarabati Mkandarasi wa Wizara na Wakandarasi wengine wametumika na ndiyo maana tukaweza kufikia pale tulipofikia sasa kwa ubora. Kuhusu suala lake la pili, suala la maeneo finyu na katika maeneo wanayoyataja kama nilivyosema Ofisi za Mkurugenzi na Wakurugenzi wengine katika swali la msingi amezungumzia ukarabati wa Muhimbili lakini kwenye jibu langu nimesema kwamba haukuhusisha jengo la utawala. Lakini nakubali kabisa jengo la Utawala kule bado hakujatengenezwa na ofisi yao ni finyu. Kwa hiyo, tutakapopata fedha za kukarabati jengo la utawala na ofisi nyingine basi tutachukua ushauri ili kuhakikisha kwamba tunaziboresha ziwe nzuri zaidi.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swala langu linafanana fanana na swali la Mheshimiwa Kigwalilo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni ukweli usiopingika na ulithibitishwa na Serikali mwakla 2008 hapa Bungeni kuwa Mkoa wa Shinyanga, hauna Hospitali stahili ya Mkoa; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais tarehe 31 Mei, 2009 alikubali ombi la wananchi wa Shinyanga Serikali kujenga Hospitali ya Mkoa. Je, kwa kuwa ujenzi huo unatarajiwa uanze katika mwaka wa fedha wa Julai, 2010 (mwaka huu), ningependa kujua hivi ujenzi wa Hospitali ya Mkoa huwa unachukua miaka mingapi kwa wastani ili kusudi wananchi wa Shinyanga waweze kujiridhisha? Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Hili Mheshimiwa umechomekea tu, lakini kwa kuwa naelewa uwezo wa Naibu Waziri, nina hakika atakujibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mkoa wa Shinyanga hauna Hospitali ya Mkoa, na kweli Serikali tulikuwa tumeagizwa kwamba tufanye utaratibu wa kuweza kujenga Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Lakini, si Shinyanga tu, kwa sababu katika Mpango wetu wa Maendeleo ya Afya ya Msingi unatuelekeza kwamba katika kila Mkoa kuwe na Hospitali ya Mkoa ambayo ni ya Rufaa. Kwa hiyo, kuzingatiwa kujengwa kwa Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga, mimi nadhani tuko katika ule utaratibu.

Mheshimiwa Spika, ninachokifahamu mimi hapa, kama Mkoa wa Shinyanga unatakiwa hili swala ufanye Bajeti yao ili waweze kuingiza katika Bajeti ya Mkoa. Lakini vile vile wenyewe huwa wanapeleka maombi maalum kule Hazina kwa sababu wale Hazina ndio wanatoa hizi pesa. Sasa kama inaanza Julai, 2010/2011, kusema kwamba itachukua muda gani, kwa kweli itategemea kupatikana fedha za kujenga ile Hospitali. Kama fedha zitapatikana zote kwa wakati mmoja, hata katika miaka miwili itakuwa imeisha. Lakini kama itakuwa pesa inapatikana kidogo kidogo, inaweza ikachukua hata miaka kumi kulingana na pesa itakayokuwa inatolewa na Serikali. Kwa hiyo, ni azma yetu kwamba Mwenyezi Mungu akitujalia na Bajeti yetu ikituruhusu, tungependa Shinyanga na Mikoa mingine iweze kuwa na Hospitali za Mikoa ili kuweza kupunguza msongamano mkubwa sana ambao unaleta adha katika Hospitali ya Muhimbili.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa. Bado tuko Wizara ya Afya, swali linalofuata linahusu matibabu kwa wenye vichaa vijijini, linaulizwa na Mheshimiwa Ramadhani Maneno wa Chalinze.

**MHE. RAMADHAN A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni vichaa vya mbwa!

**SPIKA:** Vichaa vya?

**MHE. RAMADHAN A. MANENO:** Mbwa!

**SPIKA:** Aaa, vichaa vya mbwa, haya!

**Matibabu kwa Mbwa Wenye Vichaa Vijijini**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO** aliuliza:-

Kwa kuwa, vijijini ndiko kwenye mbwa wengi wenye ugonjwa wa kichaa na wengi wao hawana chanjo; na kwa kuwa vijijini hakuna dawa (chanjo) ya kinga kwa ajili ya binadamu na mtu aking'atwa hulazimika kwenda kupata matibabu katika hospitali ya Wilaya au Mkoa iliyo umbali wa kilometa 150 au zaidi:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wanaoshindwa kwenda kupata matibabu katika hospitali hizo kwa kukosa nauli na hatimaye kupoteza maisha?
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka huduma hiyo kwenye vituo vya Afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, Mbunge wa Chalinze, lenye sehemu (a) na (b kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuweka *Hansard* vizuri, tunasema ni kichaa cha mbwa, tunasema watu wenye kichaa cha mbwa. Hatuwezi kusema vichaa, kichaa hatuwezi kuweka katika wingi.

Mheshimiwa Spika, huduma ya chanjo ya kichaa cha mbwa inatakiwa inapatikana katika vituo vyote vya afya. Ni wajibu wa kila Halmashauri kuhakikisha kuwa chanjo hizo zinakuwapo katika vituo vya afya na hasa katika maeneo ambayo tatizo hili ni kubwa. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumewapunguzia wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kupata huduma kwenye hospitali za Wilaya na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo ni kwamba Halmashauri husika hutakiwa kuwasilisha Wizarani maombi ya dawa za chanjo ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa kulingana na mahitaji yake. Mara dawa hizo zinapokaribia kwisha, Halmashauri kupitia ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya hutakiwa kutoa marejesho ya matumizi ya chanjo walizopokea awali ikiambatana na barua kutoka ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa husika ya kuomba chanjo nyingine. Lengo la utaratibu huu ni kudhibiti matumizi ya chanjo hizo na kuhakikisha kuwa dawa za chanjo zinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, Mara nyingi tatizo la ukosekanaji wa huduma ya chanjo ya kichaa cha mbwa kwa baadhi ya vituo vya tiba, hutokana na upungufu wa baadhi ya

watendaji wa afya ngazi ya Wilaya na Mkoa kwa kutorejesha matumizi ya chanjo walizopatiwa awali.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii, kupitia Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa watendaji wa Idara ya Afya ngazi ya Mkoa na Wilaya kuzingatia taratibu zilizowekwa ili kuharakisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi zinapatikana. Aidha nawakumbusha wananchi kuzingatia umuhimu wa chanjo baada ya kuumwa na mbwa ili kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Pia niwasisitizie wafugaji wa mbwa kuhakikisha kuwa mbwa wao wanapatiwa chanjo kila inapobidi kufanya hivyo.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini, nina maswali mawili ya nyongeza. Siyo siri wananchi vijijini kupatwa na adha kubwa sana hasa kwa wale ambao wameumwa na mbwa mwenye kichaa; na kwa kuwa mbwa ni moja ya mifugo, kwa nini sasa Serikali haitilii manani kupeleka chanjo vijijini kama ilivyo mifugo mingine?

Kwa kuwa, mama mjamzito anapofikia wakati wa kujifungua hupelekwa hospitali haraka sana ili kuokoa maisha yake pamoja na mtoto.

Je, mtu anayeumwa na mbwa ni saa ngapi anatakiwa awe amefikishwa kwenye hospitali ili aweze kupata tiba ukizingatia kwamba mtu anaumwa na mbwa mwenye kichaa Chalinze, anatakiwa akapate tiba hospitali ya Amana Dar es salaam (ambapo nina ushahidi huo)?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, njia kubwa ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa kutoka kwa mbwa kwenda kwa mtu ni kumchanja yule mbwa, na ni kweli kabisa kwamba kama tutataka kupunguza kwa kiasi kikubwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa kwa binadamu ina maana lazima tuchanje wale mbwa wetu. Kwa maana hiyo, kama kweli alivyosema kwamba mbwa ni mojawapo ya mifugo, nafikiri Wizara ya mifugo inasikia. Kwa maana hiyo sasa, kama wale mbwa wenyewe, mimi ninavyofahamu wana kawaida kwamba watu wanaenda kule Wilayani kuchanja mbwa wao na pale inapoonekana kwamba kuna wale mbwa ambao wanatembea wenyewe hovyoy bila kuwa na mtu, mara nyingi huwa kuna zoezi la kuwaua wale mbwa.

Kwa hiyo kama nilivyosema, niwakumbushe tu kwamba wananchi wanatakiwa wawachanje, lakini na watalaam wa mifugo katika maeneo yale na wenyewe waende kuwahasisha wananchi na kuwafahamu wale mbwa wanaofugwa kule ili waweze kupatiwa chanjo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; mgonjwa anapokuwa ameumwa na mbwa kama mgonjwa mwingine yeyote awaye, mara anapojitambua kwamba ameumwa na mbwa, kitu cha kwanza kabla hata hajaenda hospitali, anatakiwa ile sehemu aliyumwa na mbwa aisafishe kwa maji mengi sana na sabuni nyingi ambayo hiyo sasa inakuwa ni ile *first aid*. Baada ya hapo sasa, mgonjwa huyo anatakiwa aende kituo cha

kutolea huduma ili aweze kwenda kupatiwa yale matibabu mengine. Lakini, vile vile ugonjwa unakuwa ni hatari zaidi kulingana na sehemu aliyomwa na ukubwa wa jeraha kinavyokuwa. Kwa hiyo, napenda nitoe wito tena kuwakumbusha wale wananchi wanaomwa na mbwa wazingatie hayo kabla hata hajaenda hospitali. Ahakikishe anaosha lile jeraha na sabuni na maji, halafu baadaye aende hospitali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, maelezo ya ziada kuhusu mbwa!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwa majibu mazuri. Lakini, napenda tu niongezee majibu katika maswali ya nyongeza mawili yaliyoulizwa na Mheshimiwa Maneno. Ni kweli kabisa kwamba mbwa ni sehemu ya mifugo na kwa takwimu tulizonazo hadi sasa hivi kuna mbwa milioni 4 katika nchi hii na Mkoa unaoongoza kwa kuwa na mbwa wengi ni Mkoa wa Iringa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kwamba si kila mbwa anapomwuma binadamu, basi yule mbwa atakuwa na ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Hadi sasa hivi Wizara yangu imeishasambaza chanjo za kichaa cha mbwa katika nchi nzima ambazo ni zaidi ya dozi 50,000. Kwa hiyo, ningependa nitoe wito kwa Halmashauri husika ambazo tayari zimaishapata hizo chanjo kwa ajili ya mbwa, ziendeele kuwachanja. Lakini pia, nitoe wito kwa wananchi wote, watunze mbwa wao, mbwa wasiendeele kuzurura hovyoy. Lakini, Halmashauri pia zisichukue hatua za kuwaua tu mbwa wanaozurura kwa sababu Halmashauri hizo zitakuwa zinavunja sheria Na.19 ya mwaka 2008 ya Ustawi wa Wanyama. Kwa hiyo, ni lazima wafuate taratibu zote za sheria katika kuwaua hao mbwa wanaozurura hovyoy. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba hao wanyama nao wanalindwa kwa mujibu wa sheria za nchi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Lo! Haya mambo makubwa haya!

Na. 112

### **Kifo cha Kijana Mtanzania Nchini India**

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, inasemekana kwamba kuna kijana wa Tanzania (Imran E. Mtui) ambaye aliuawa kikatili katika Mji wa Bangalore nchini India mwezi Januari, 2010; na kwamba sababu za kifo hicho hazijulikani:-

- (a) Je, Serikali kupitia vyombo vya upelelezi imetoa taarifa gani kuhusu kifo cha kijana huyo?
- (b) Je, Serikali ya India imetoa taarifa gani hadi leo kuhusu kifo hicho?



**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Serikali yetu kupokea taarifa ya kifo cha Mtanzania Imran E. Mtui, aliyekuwa mwanafunzi nchini India, Ubalizi wetu India ulifuatilia tukio hilo kwa kushirikiana na uongozo wa jeshi la Polisi la India. Kwa kifupi, mwili wa Marehemu Mtui ulikutwa kando kando ya reli majira ya saa 3 asubuhi Januari, 31 mwaka 2010, ukiwa na majeraha makubwa kichwani.

Mheshimiwa Spika, taarifa za awali za Polisi India zilidai kuwa Marehemu alijiua mwenyewe. Aidha, taarifa ya Madaktari wa India (*Post mortem report*) ilibaini kwamba marehemu alikufa kutokana na mshituko na kuvuja damu uliosababishwa na kusagwa kichwa na treni (*shock and hemorrhage as a result of crush injury sustained to the head*).

Mheshimiwa Spika, Serikali ya India, kupitia kwa Inspekta Jenerali wa Polisi imetuthibitishia kuwa wataalam wake wanaendelea na uchunguzi na wameahidi kutupatia matokeo ya uchunguzi huo pindi utakapokamilika. Mwili wa Marehemu ulisafirishwa na kurejeshwa nyumbani na Serikali yetu na napenda kumalizia kwa kutoa pole tena kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Imrani Mtui. (*Makofi*)

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Lakini, kabla ya hapo na mimi kwa niaba ya watu wa Mji Mkongwe, nатоa mkono wa pole kwa wazazi, ndugu, familia na Watanzania wote kutokana na kifo cha mwanafunzi wetu huyu Imran E. Mtui. Mungu ailaze mahala pema roho ya marehemu na sote tuamini kwamba *Inalilah Wainailah Rajuun*. Sasa, maswali yangu mawili madogo ya nyongeza:-

Kwa kuwa, inasemekana kwamba wapo baadhi ya wanafunzi walioathirika kisaikolojia katika chuo kile ambao walikuwa karibu na mwanafunzi marehemu Imran Mtui wamerejea nyumbani na wanasoma hapa ili baadaye wakafanye mitihani yao nchini India; na kwa kuwa mauaji na hujuma dhidi ya wanafunzi wetu wanaosoma nchi za nje yanakuwa yanatokea mara kwa mara.

Je, Serikali ina mikakati gani ambayo itahakikisha usalama wa wanafunzi wetu wote wanaosoma nchi za nje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa miaka miwili iliyopita wanafunzi waliuwawa nchini Marekani na tukaambiwa kwamba uchunguzi unaendelea na ripoti itatolewa; hadi hii leo miaka miwili hatuna ripoti ya uchunguzi uliofanyika nchini Marekani na leo katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba *IGP* wa India anaendelea na uchunguzi na ripoti itatolewa baadaye. (*Makofi*)

Je, Serikali inawaambia nini Watanzania kuhusu vifo hivi vilivyotokea kwa mauaji ya wanafunzi wawili Marekani pamoja na huyu ambaye uchunguzi wake unaendelea nchini India? Mheshimiwa Spika, ahsante sana! (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, wakati wanafunzi wanapokwenda kusoma nchi za nje, Serikali huwa inawasisitiza sana juu ya kwenda kuishi vizuri na wenyeji wao, pia kufuata sheria na taratibu za nchi husika, na tatu tumewashauri mara nyingi, kuepukana na mauaji haya, tumewashauri mara nyingi na nasisitiza tena kwamba wanafunzi wetu wanapotokea kutembea usiku, wasiende mmoja mmoja, wajaribu kwenda kwa kikundi, watu wawili na kuendelea ili lolote litakalotokea tuwe na ushahidi nalo.

Mara nyingi, mtu anakwenda peke yake, mfano kama marehemu Mtui alitoka peke yake nyumbani, akaenda zake; na taarifa nilizonazo ni kwamba mara nyingi alikuwa akitoka matembezi, hutoka na pikipiki. Siku hiyo hakutoka na pikipiki.

Kwa hiyo, hatujui kilichomsibu huko njiani na kwa sababu alikuwa peke yake. Kwa hiyo, Serikali inasisitiza na inatoa wito kwa wanafunzi wetu nje, wakienda kutembea basi angalau waende kwa kikundi ili angalau lolote litakalotokea tuweze angalau kupata ushahidi kutoka kwa hao wenzake watakaokuwa wamebakia.

Mheshimiwa Spika, ni kweli swali la pili kwamba uchunguzi wa mwanafunzi huyo wa India unaendelea na uchunguzi kuhusu Watanzania waliofariki kule Marekani unaendelea, na mpaka leo hatujapata maendeleo yoyote ya uchunguzi huu unavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, suala la mauaji yanatokea wakati mwingine kwa siri na kwa mazingira ya kutatanisha. Kwa hiyo, hata uchunguzi pamoja na utalaam ambao wenzetu wanao, inakuwa siyo rahisi kumaliza uchunguzi huu mara moja.

Lakini, kwa hawa miaka miwili iliyopita kama Mbunge alivyosema ni muda mrefu na tukitegemea kwa utalaam wa wenzetu tungeekuwa tumeishapata matokeo ya uchunguzi, lakini bado hatujapata matokeo haya.

Lakini tunafarijika kwamba bado uchunguzi unaendelea, na mimi juzi nilikuwa Marekani, nilipata taarifa kutoka kwa Balozi wetu, akasema bado uchunguzi unaendelea na faili la uchunguzi bado halijafungwa. Hii ni faraja kwamba bado wenzetu Marekani wanaendelea kufanya uchunguzi juu ya vifo vile vya Watanzania wenzetu wawili.

Mheshimiwa Spika, labda tu ningependa kuwasihi Watanzania waendeleo kuwa wavumilivu wakisubiri matokeo ya uchunguzi huu wa vifo hivi. (*Makofi*)

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Mbeya una hali ya hewa nzuri yenye ubaridi na mvua nyingi za kutosha na zinaruhusu kilimo cha matunda kama vile matofaa, parachichi, *peaches*, *plum* na kadhalika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kabambe wa kuhakikisha kilimo cha matunda katika Mkoa wa Mbeya kinakuwa na kuwaongezea kipato wananchi?

(b) Je, ni vyuo na taasisi gani za kilimo zinatoa mafunzo na kufanya utafiti kuhusu Kilimo cha Matunda?

(c) Je, kwa nini serikali haikipi kilimo cha matunda kipaumbele wakati kinaongeza lishe na fedha za kigeni?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mipango mbalimbali ya Kitaifa ya kuendeleza mazao ya bustani yakiwepo matunda. Mwaka 2009 Serikali ikishirikiana na Taasisi ya *Enterprise Work/Vita* kuendeleza kilimo cha matunda aina ya matofaa (*apples*), *peaches*, makarakara (*passion*) na maparachichi (*avocados*) katika Mikoa ya Iringa na Mbeya. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya *Tanzania Horticultural Association (TAHA)* na *Technoserve* inaendeleza shughuli zilizoanzishwa na *Enterprise Work/Vita* katika kuwaelimisha wakulima mbinu bora za uzalishaji wa matunda, ili kufikia kiwango cha ubora kinachokidhi soko la ndani na nje ya nchi. Mwaka 2009/2010 Serikali imeandaa mpango mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza mazao ya Bustani kwa kushirikisha sekta binafsi. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, Kituo cha mafunzo na utafiti wa Kilimo kilichopo Tengeru ni kituo mahsusi kinachotoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada na kufanya utafiti wa mazao ya bustani. Aidha, katika baadhi ya Mikoa na Wilaya vipo vyuo vya maendeleo ya Wananchi kama vile Chuo cha Ichenga kilichopo Njombe Mkoani Iringa ambacho hutoa elimu ya kilimo kuhusu uzalishaji wa matunda. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inakipa kipaumbele kilimo cha matunda kwa kutekeleza mipango ya uzalishaji wa miche bora ya matunda katika bustani za Serikali zilizopo Mpiji (Bagamoyo) Igurusi (Mbarali), Bugaga (Kasulu), Songa (Muheza) na Malindi na Jegetal (Lushoto).

Aidha, wakala wa mbegu za kilimo (*Agricultural Seed Agency (ASA)*) pamoja na majukumu mengine, wamepewa jukumu la kuzalisha miche bora ya miembe kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya wakulima wa Kanda ya Mashariki.

Serikali pia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazao ya bustani imeanzisha Baraza la Taifa la Kuendeleza Mazao ya bustani (*Horticultural Council of Tanzania (HODEC)*) mojawapo wa majukumu ya *HODEC* ni kuwaleta pamoja wadau wa

Serikali na sekta binafsi nchini kwa kuandaa mikakati ya kuendeleza tasnia ya mazao ya bustani (*Horticulture*).

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa, Serikali imetueleza hapa juu jitihada yake ya kuendeleza kilimo cha matunda hapa nchini kwa wingi. Na kwa kupitia wadau mbalimbali taasisi mbalimbali. Je, Waziri anaweza kuliambia Bunge hili sasa ni kiasi na ni ukubwa gani wa eneo la nchi hii linalimwa matunda? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lipo tatizo kubwa sana la uhaba wa wataalamu vijijini na hasa wataalamu wanaohusika na kilimo cha matunda. Lakini vilevile kuna uhaba mkubwa wa watafiti katika vyuo ambavyo amevitaja na hasa au watafiti wa matunda. Je, Serikali inatuambia nini, inachukua hatua gani ili kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, eneo linalolimwa matunda linatofautiana mwaka hadi Mwaka lakini kwa kuwa linahitaji takwimu basi nitamtafutia Mheshimiwa Mbunge ili niweze kumpatia takwimu hizo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la Pili ni kweli kabisa kuna uhaba wa wataalamu na Serikali katika programu yake ya kuendeleza wataalamu wa ugani kila mwaka inapeleka wanafunzi ili waweze kuchukua elimu ya ngazi mbalimbali kwa mfano *Diploma* na *Certificate* kwa ajili ya kuendeleza matunda. Katika vyuo ambavyo nimevitaja vya Tengeru na Ichenga vyuo hivi vinazalisha wataalamu pamoja na maofisa ugani ambao wanasaidia katika kuelimisha wakulima juu ya kilimo bora cha matunda.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu inapoteza pesa nyingi za kigeni kuagiza matunda ya *apples* kutoka nje wakati upo uwezekano wa matunda haya yakazalishwa kwa kiwango kinachotakiwa na tukapata mafanikio kama maeneo ya Lushoto, Mbeya na Iringa.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba mbegu hizi ambazo wananchi wengi wanapenda matunda haya zikazalishwa hapahapa ili kuokoa fedha za kigeni na hatimaye wakulima wetu wakapata faida katika zao hili.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba matofaa yanazalishwa kwa wingi na hasa katika maeneo ya Lushoto. Mwaka huu tumeanza kwa kasi kabisa kuzalisha miche ya miembe kusudi iweze kupandwa katika maeneo ya Mikoa ya Mashariki mwa Tanzania.

Kwa hiyo, nadhani wazo lake ni zuri kabisa, na matufaa haya yanayozalishwa Lushoto ni mazuri kabisa. Kwa hiyo, nadhani tutaweza kushirikiana na wataalamu wetu ili tuweze kuangalia uwezekano wa kuzalisha mbegu zaidi ili tuweze kupata matunda mazuri kama yale yanayotoka Afrika ya Kusini.

## **Kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji.**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa kwanza wa wakulima na nchi kwa ujumla, na kwamba Mikoa kama Shinyanga, Tabora, Singida na Dodoma hukumbwa na ukame mara kwa mara na mvua zisizo na uhakika:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani katika kuwa na skimu za umwagiliaji za uhakika?

(b) Je, kuna mkakati gani wa kutumia maji ya mto manonga yatumike vema kama kuchimba mabwawawa makubwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kilimo cha umwagiliaji kinayo nafasi kubwa ya kimkakati ya kuleta mapinduzi ya kijani na kukifanya kilimo kuwa cha kisiasa, kibiashara na kinachoweza kuchangia katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ili kufanikisha usalama na kujitosheleza kwa chakula.

Ili kufikia malengo haya Serikali imepanga kutekeleza mambo muhimu yafuatayo;-

(i) Kukamilisha mkakati wa Sheria ya umwagiliaji,

(ii) Kuendelea kutekeleza programu ya kuendeleza sekta ya Kilimo na kuongeza eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji kutoka hekta 326,492 za mwaka 2010 hadi hekta 600,000 ifikapo mwaka 2015. Lengo hili litafanikiwa kwa Serikali kushirikisha sekta binafsi katika kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji hasa wakulima wakubwa,

(iii) Kukarabati miundo mbinu ya skimu za zamani zilizochakaa na kujenga miradi mipya kwa ajili ya wakulima wadogo na wa kati.

(iv) Kujenga mabwawa mapya na kukarabati mabwawa yaliyochakaa ili kuvuna maji ya mvua,

(v) Kuhimiza matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zinazotumia maji kwa tija siyo kuyamwaga hovyotu,

(vi) Kutumia maji chini ya ardhi,

(vii) Kujenga uwezo wa taasisi zinazohusika na umwagiliaji katika ngazi ya Taifa, Halmashauri na Wakulima.

(viii) Kuimarisha mafunzo na utafiti katika fani ya umwagiliaji. Aidha hapa tunasisitiza hasa kurekebisha mitaala katika vyuo vyetu ili viweze kukidhi mahitaji yetu nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2000 na 2007, Serikali iliendeleza miradi ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 11,719 kupitia programu husishi ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji (*PIDP*) katika Mikoa kame ya Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Mwanza. miradi yote iliyojengwa inavuna maji kwa njia ya majaluba na kuwezesha kilimo cha msimu mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inachunguza uwezekano wa kujenga mabwawa katika skimu zilizojengwa likiwemo Bonde la mto manonga.

Mheshimiwa Spika, Mto Manonga unatenganisha mikoa ya Tabora (kupitia katika Wilaya za Nzega na Igunga) na Mkoa wa Shinyanga (Wilaya za Shinyanga Vijijini na Kishapu). Wizara yangu inafanya uchunguzi wa kujenga bwawa litakaloweza kuhifadhi maji ya kumwagilia skimu za Lyawelagwa (Nzega) na Nyida (Shinyanga). (*Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, maji ambayo yanaelekezwa katika Bonde la Mto Manonga huanzia katika Mikoa kama alivyosema Waziri haoni kwamba ujenzi wa mabwawa mawili tu ni kuyafanya yale maji mengi yaendelee kupotea bila kuvunwa kurahisisha ulimaji kwa umwagiliaji katika maeneo ya Mkoa wa Shinyanga, Tabora na Singida?

Mheshimiwa Spika, swali la Pili, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza mikakati ambayo ipo kwa ajili ya kuimarisha umwagiliaji. Lakini nchi hii inapata janga la njaa mara kwa mara. Je, Waziri anaweza kueleza inahitajika hekta ngapi zilimwe ili kuondokana na janga la njaa la mara kwa mara katika Mikoa mbali mbali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba Wizara yangu inafanya uchunguzi wa kujenga bwawa kubwa lakini siyo mwisho kwamba lazima liwe bwawa hilo tu. Hasa ukizingatia kwamba eneo kubwa hilo ambalo analizungumzia kati yake kuna barabara kubwa inayotoka Nzega kwenda Shinyanga.

Kwa hiyo, lazima tunapoanza utafiti wa kujenga bwawa mambo yote haya Miundo mbinu mingine iliyopo katika eneo hilo tujihakikishie kwamba haita athiriwa na mabwawa yatakayojengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utafiti huu utakwenda zaidi ya hapo utaonyesha maeneo mengine ambayo yanayofaa kujenga mabwawa katika Bonde zima la Manonga.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge, pia namshukuru kwa kunikumbusha kwamba ni bonde zima tunalichunguza na siyo bwawa moja au mawili tu. Kuhusu suala la hekta ngapi zilimwe ili tuweze kuzalisha mpunga na kujitosheleza.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba mwaka uliopita 2009 kama ninakumbuka vizuri tulizalisha tani 867,619 alituambia hapa Mheshimiwa David Mathayo David, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya nchi hii yalikuwa tani 712,390 na tulijitosheleza kwa 155, 229 lakini hiyo ni kutokana na mvua zilionyesha vizuri sana hasa katika Mkoa wa Morogoro ambako dalili zilionyesha vizuri hata bei ya mchele ilipungua kuliko mahindi. Sisi tulifanya utafiti chini ya mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na utafiti huo unatuonyesha tukiweza kulima hekta 405,400 mara mbili yaani tukiweka Miundombinu ya kuhakikisha kuwa tunalima mara mbili basi tutaweza kufanikisha kupata Mpunga utakaotoa mchele wa kuzalisha ziada.

Mheshimiwa Spika, tunaweza hata tukauza nchi za nje lakini pia katika *study* hiyo kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge nimewahi kusema kwamba ili tufikie hapo tunahitaji kuwa na uwekezaji wa shilingi takribani bilioni 30 kila mwaka. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:**Mheshimiwa Spika, kutokana majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba tunahitaji bilioni 30 kwa kila mwaka ziko bilioni 25 kila mwaka zinatolewa na Rais Kikwete kwa nini zisielekezwe huko ili kuondokana na tatizo la njaa badala ya kuzitoa hizi pesa ambapo *impact* yake haionekani hivi sasa. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**Mheshimiwa Spika, ni kwamba ushauri wa Kiongozi wa Upinzani tunauchukua kwamba ni ushauri mzuri. Tunakwenda katika Bajeti sasa basi ni vizuri mambo yote haya tuyaweke pamoja maana yake huu ni muda wa kupanga. (*Makofi*)

Na. 115

***Dawasco* Kufunga Mita kwa Watumiaji wa Maji Kilangalanga – Mlandizi**

**MHE. ZAYNAB M. VULU (K.n.y. DR. IBRAHIM S. MSABAHA)** aliuliza:-

Je, ni lini *DAWASCO* itafunga mita kwa watumiaji maji eneo la Kilangalanga – Mlandizi ili waondokane na adha ya Ankara za Maji za Makadirio?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikipokea malalamiko ya mara kwa mara yanayohusu “ankara hewa” za maji. Ili kutatua tatizo na kero hii. Serikali kupitia *DAWASA* inateleleza mradi wa kuboresha huduma ya usambazaji maji katika maeneo

ya Mlandizi, Kimara na Mji wa Kibaha kwa kukarabati mabomba ya maji kwa gharama ya shilingi bilioni 12.5 na kuwaunganishia dira wateja wote ifikapo tarehe 31 Julai 2010.

Mheshimiwa Spika, eneo la Kilangalanga – Mlandizi *DAWASCO* ina wateja 54 ambao tayari wote wamefungiwa dira ya maji. Aidha, vioski vyote vinavyoendeshwa na Serikali ya Kijiji vitakuwa vimefungiwa dira ifikapo tarehe 30 Juni, 2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuleta kero zao Wizarani napenda kuwashauri Wananchi wote kuwa huru kupeleka kero zao pia Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*).

Aidha napenda pia kuwaarifu kuwa Sheria iliyounda *EWURA* inaruhusu pia kuwepo kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati vyombo vyote hivi vinaweza kusaidia kufanya usuluhishi na kutatua kero, naomba wananchi tuvitumie. (*Makofi*)

**MHE. ZAYNAB M. VULU:**Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwekaji wa mita unasaidia ukusanyaji wa ankara na kumsaidia mteja kujua matumizi na ulipaji wake wa deni. Je, Serikali haioni kucheleweshea bili yake ni kumbebeshea mzigo ambao hastahili kuwa nao?

Mheshimiwa Spika, swali la Pili kwa kuwa Serikali leo imetamka kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, 210 na tarehe 31 Julai mwaka huu itakuwa imekamilisha zoezi lake la kufunga mita.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kueleza zoezi hilo litaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema suluhu ya kero hii ya ankara za maji ni kuweka mita za maji na ndiyo maana tunajitahidi kuweka mita za maji kwa wateja wetu.

Kwa hiyo, ni kweli kabisa kuchelewesha kupeleka ankara kunamletea matatizo mteja lakini kama nilivyosema ukisha mwekea mita hata huu ucheleweshaji nao utakuwa umekwisha. Maana kutakuwa na usomaji wa hapo hapo na kutoa majibu kuliko utaratibu ambao unaendelea wa mahala pengine kwa kukadiria kwa hiyo zoezi hili ndiyo itakuwa ni suluhu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niseme pia kwamba zoezi hili siyo kwamba labda litaanza lini tumeshaanza mchakato. Vifaa vinatafutwa na niseme kwamba zoezi hili sasa linaendelea. (*Makofi*)

Na. 116

### **Kujenga Chuo cha Veta Wilayani Kiteto**

**MHE. BENEDICT OLE NANGORO** aliuliza:-



Kwa kuwa chuo cha *VETA* kinahitajika sana Wilayani Kiteto na kwamba eneo la kujenga chuo hicho limeshatafutwa na kupatikana.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga Chuo cha *VETA* Wilayani Kiteto?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, Mbunge wa Kiteto, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kiteto ni moja kati ya Wilaya 28 zilizopewa nafasi ya kwanza katika mpango wa ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya. Nachukua nafasi hii kuipongeza Wilaya hiyo kwa kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza mchakato wa ujenzi wa vyuo hivyo kwa kuanza usanifu wa michoro, kutengeneza gharama za ujenzi na kupata ushauri elekezi. Kazi hizo zote zikikamilika na fedha zikipatikana ujenzi utaanza mara moja. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

- (a) Je, Serikali ingeliweza kutuambia waziwazi kwamba kazi hii ya kuandaa michoro ambayo tumeambiwa kwamba mchakato umeshaanza ni lini hasa itakamilika na fedha ya kuanza ujenzi kupatikana?
- (b) Kwa kuwa *study* za kiufundi hutofautiana mahitaji yake kati ya Wilaya na Wilaya; ni lini Serikali itafanya maandalizi ya kubainisha *study* zitakazofundishwa katika chuo hicho cha *VETA* mara kitakapojengwa Wilayani Kiteto?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimezungumzia kwamba, mchakato wa ujenzi umeshaanza, tunapozungumzia usanifu ni pamoja na kubaini mahitaji katika kila eneo. Ufundi unaokusudiwa kujengwa hutofautiana kutoka Wilaya moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi 28 vilitengewa fedha za kuanzia mchakato huu na pale utakapokamilika, kwa umoja wao, vyuo hivyo vitaanza. Yanahitajika mabilioni ya fedha, nataka niseme tu katika bajeti iliyotengwa mwaka 2009/2010, kazi zake zote zimeshakamilika. Hivi ninavyozungumza, hata Mbunge akipenda kuona michoro inayokusudiwa kujengwa Kiteto namkaribisha ofisini kwetu.

## **Serikali Kujenga Shule za Vipaji Maalum Kigoma**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Kwa kuwa upo ushahidi wa kutosha kwamba Mkoa wa Kigoma una Vijana wengi wenye vipaji maalum na hasa wanasayansi waliobobea katika fani ya fizikia, hesabu, kemia na baiolojia:-

- (a) Je, ni kwa nini Serikali haifikirii kujenga shule maalum kwa ajili ya vijana hao?
- (b) Je, Serikali ipo tayari kushirikiana na Mkoa wa Kigoma kuendeleza mkakati huo muhimu wa Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzungwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina shule za vipaji maalum ambazo hudahili wanafunzi waliofaulu vizuri zaidi katika mitihani ya Darasa la Saba na Kidato cha Nne. Shule hizi hutoa fursa kwa mikoa yote kwa uwiano sawa, ambapo kila mkoa hutengewa nafasi arobaini kwa ajili ya wasichana na wavulana.

(b) Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni ujenzi wa maabara katika shule za sekondari zilizoko kwenye Kata, upatikanaji wa vitabu vya kutosha, ujenzi wa nyumba za walimu na kuimarisha shule zilizopo kwa kujenga mazingira mazuri zaidi ya kujifunzia na kufundishia.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza:-

(a) Kwanza, nilitaka kujua hizo nafasi arobaini ni kwa shule za sekondari vijana wanaofuzu Kidato cha Nne na wanaofuzu Shule za Msingi kwa maana ya kuwa sasa 80, 40 au ni 20; naona hili jibu la (a) liko jumla mno, nilitaka kujua hiyo arobaini maana yake nini?

(b) Ukiangalia msingi wa swali lenyewe, nilitaka kujua kwa Mkoa wa Kigoma ni vijana wangapi waliofuzu Kidato cha Nne ambao walipelekwa katika hizo shule maalum, ukizingatia hoja yangu ya msingi kwamba Mkoa wa Kigoma upo ushahidi wa wazi kwamba kuna vijana wengi wenye vipaji katika masomo ya sayansi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi nilieleza

kwamba, kila Mkoa hupatiwa nafasi 40; 20 kwa wasichana na 20 kwa wavulana kila mwaka tangu shule hizo zilipoanza.

Mheshimiwa Spika, nafasi hizo hutolewa kwa kushirikiana na Kamati ambayo iko chini ya Katibu Tawala na Afisa Elimu akiwa ni Katibu. Kwa Kanuni zetu, Mheshimiwa Mbunge anapaswa kuwa Mjumbe katika Kamati ile ya *selection*.

Mheshimiwa Spika, kuweza kumpatia takwimu ya wanafunzi wangapi, naomba tafadhali tuwasiliane niweze kumwonesha maana ni ndefu na hajanieleza anahitaji kuanzia mwaka gani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia haifichiki kwamba, kila Mkoa unao wanafunzi wenye vipaji, kwa hiyo, niwapongeze wenzetu wa Kigoma, lakini nchi nzima wapo wanafunzi wenye uwezo mkubwa na tunazo shule nane ambazo zinapokea wanafunzi wasichana kwa wavulana wenye uwezo mkubwa sana.

Na. 118

### **Wananchi Kuchukua Sheria Mkononi Mwao**

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna tabia ya baadhi ya wananchi kuchukua sheria mkononi mwao kwa kuwapiga na hata kuwachoma moto mpaka kufa wale wanaowashaku kuwa ni majambazi na vibaka huku watoto wadogo wakishuhudia mambo hayo:-

- (a) Je, Serikali imejipangaje kumaliza tatizo hilo?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba tabia hiyo isipokomeshwa haraka tutajenga Taifa lenye watu wakatili?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila mtu anayo haki ya kuishi; na pia Ibara ya 12 ya Katiba hiyo, inahimiza kuheshimiwa kwa utu wa mtu. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 15 ya Katiba hiyo, kila mtu anayetuhumiwa kutenda kosa lolote la jinai, hupaswa kuhukumiwa na Mahakama kwa mujibu wa sheria na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali huchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watu wanaoua wenzao kwa vipigo au kuwachoma moto kwa tuhuma za wizi, mauaji na makosa mengine. Sheria itachukua mkondo wake dhidi ya mtu yeyote anayejihusisha na vitendo vya kuadhibu mtuhumiwa kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, ili kukomesha tabia hii mbaya, Serikali pamoja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watu wanaochukua sheria mikononi mwao, inashirikiana na wadau mbalimbali hususan wale wanaojihusisha na haki za binadamu katika kutoa elimu ya haki za binadamu nchini kote.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, natoa wito kwa wananchi wote kutokuchukua sheria mikononi na wawe na imani na vyombo vya dola vyenye dhamana ya kutoa haki na watambue kuwa kitendo cha kuchukua sheria mikononi ni kosa la jinai.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Waziri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa kilio kikubwa cha wananchi mpaka wao inawapasa wachukue Sheria mikononi ni kutokana na kutokuwa na imani na vyombo vya dola ambavyo wanawakabidhi wale wanaowatuhumu:-

(a) Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi kwamba hivyo vyombo vya dola vinaweza kufanya kazi vizuri ili wale watuhumiwa wasionekane wakiranda tena mitaani warudishe imani kwa wananchi na vyombo vyao?

(b) Kwa kuwa wanaofanya kosa hilo la kuwaadhibu wananchi kwa kuchukua Sheria mikononi huonekana katika vyombo vya habari kama runinga wakitenda kosa hilo; je, Serikali inasubiri ushahidi gani ili tuone wakitoa adhabu kwa hao wanaotenda kosa hilo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona tumefika mwisho wa muda wa maswali, lakini tulianza na Taarifa nyingi sana zilizowasilishwa Mezani, kwa hiyo nafidia muda huo.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwamba watuhumiwa wengi huwa baadaye wanaachiwa wanaonekana wakirandaranda mitaani, nataka niseme tu kila Mtanzania au Mwananchi anayo haki ya kuonekana ana makosa mahakamani. Anapokamatwa mtu anakuwa ni mtuhumiwa, hajawa mhalifu tayari, mhalifu ni yule ambaye Mahakama imeshasema kwamba huyu amefanya kosa. Kwa hiyo, mtu ambaye anatuhumiwa anazo haki zake; ana uhuru wa kawaida na ilimradi atafika Mahakamani siku anayotakiwa, ana haki ya kuwa nje kwa dhamana.

Mheshimiwa Spika, pili, hawa wanaofanya vitendo hivi vya kuwachoma watu moto au kuwaua kuonekana kwenye vyombo vya habari kama runinga na kadhalika; ukweli ni kwamba, kinachotakiwa kumshtaki mtu ni ushahidi ambao utathibitishwa mahakamani, kama unadhani picha za vyombo hivyo zinaweza kuwa ndiyo ushahidi wa kuthibitisha mahakamani katika taratibu zetu za kisheria hivyo sivyo; ushahidi madhubuti utolewe, usiokuwa na wasiwasi kwamba, fulani kafanya kitu hiki na watu waliomwona wanasema tumemwona anafanya kitu hiki. Ushahidi uwe dhahiri, usiwe ushahidi kwa sababu picha imeonekana kule ukasema picha ile basi lazima kafanya, hapana. Lazima

asimame mtu aape mahakamani aseme mimi niliona kitendo hicho kilifanyika. Basi huo ndiyo ushahidi madhubuti unaohitajika.

Na. 119

### **Ujenzi wa Soko la Holili**

**MHE. BASIL P. MRAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kuwa itajenga soko Holili Wilayani Rombo mpakani na nchi ya Kenya:-

Je, ni lini mradi huo utanza hasa kwa kuzingatia kuwa huko Holili viwanja vinagawiwa kwa wawekezaji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kumjibu Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Masoko (*AMSDP*), yenye makao yake Jijini Arusha, ilitoa fursa kwa Wananchi wa Rombo na Halmashauri yao kuchagua eneo moja kati ya maeneo matatu yanayofaa kujenga soko. Maeneo hayo yalikuwa ni Rombo Mjini, Tarakea na Holili. Katika kutekeleza hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, ilichagua eneo la Tarakea kujenga soko hilo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa soko hilo limekwishajengwa na linaendelea kutumika na wananchi wa maeneo hayo. Kwa misingi hiyo, ahadi iliyotolewa na Serikali ya kujenga soko Wilayani Rombo imetekelezwa.

Mheshimiwa Spika, endapo Halmashauri inaona kuwa soko la Tarakea ambalo liko umbali wa takriban kilomita hamsini kutoka Holili, halikidhi mahitaji ya wananchi. Nashauri Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ijumuishe katika mipango yao, ujenzi wa soko eneo la Holili kupitia mpango wa miradi ya Halmashauri ya Wilaya. Jukumu la Halmashauri ni kuainisha vyanzo vya fedha vya kufanikisha ujenzi wa soko eneo la Holili. Vyanzo hivyo ni pamoja na Mfuko wa Miradi ya Serikali inayotekelezwa Wilayani Rombo, Wahisani wa Maendeleo na mapato ya Halmashauri yenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mramba, kwa jinsi anavyotumia uzoefu na ujuzi wake alioupata katika Bunge hili na ndani ya Serikali kuwasaidia wapiga kura wake wa Rombo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano wa kitaalam katika suala hili kila itakapotakiwa kufanya hivyo.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, namheshimu na namshukuru sana Naibu Waziri kwa jibu lake zuri.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba, maendeleo katika eneo la Holili ambacho ni kituo cha mpakani, yakiendelea kuachiwa Halmashauri ambayo siyo Halmashauri tajiri, wakati ambapo upande wa pili mpakani kunaitwa Taveta; hivi sasa tunavyozungumza wanajenga Kiwanja cha Ndege, wanajenga Kituo cha Forodha, wanajenga Ofisi za Uhamiaji, wanaunganisha barabara ya lami kutoka Arusha - Moshi mpaka Mombasa, wanavuta hata maji ya upande wa Tanzania ili wayatumie kwa maendeleo yao ya kijiji cha upande wa pili:-

Je, Waziri Mkuu haoni kwamba ingependeza vizuri zaidi hasa kwa kuzingatia biashara huria itakayoanza mwezi Julai, kwamba Serikali nzima iratibu maendeleo ya Kijiji kile ili yalingane na maendeleo ya upande wa pili?

**SPIKA:** Mheshimiwa unamuuliza Waziri wa Viwanda siyo Waziri Mkuu.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, Waziri wa Viwanda haoni kwamba ingependeza kama Serikali kwa ujumla ingefanya shughuli hiyo kwa pamoja badala ya kuiachia Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mramba kwamba, eneo la Holili ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu hususan tunapoingia kwenye Soko la Pamoja la Afrika Mashariki kuanzia mwezi wa saba.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye vile vile, Halmashauri ya Rombo inaweza isiwe na uwezo wa kuendeleza eneo la Holili likafikia kiwango ambacho kinaweza kikaendana na eneo la Taveta kule Kenya.

Mheshimiwa Spika, maadam nimeshasema hapa kwamba, Mheshimiwa Mramba ni mzoefu katika Serikali na katika Bunge hili, napenda nimshauri Mheshimiwa Mramba ajaribu kutumia uzoefu wake kuwasiliana na sisi katika Wizara yetu, tujaribu kuainisha vyanzo vingine vya mapato na vile vya Halmashauri ya Rombo ili tuweze kuona namna ya kuweza kujenga eneo la Holili liweze kuwa na kiwango ambacho kinaweza kikafanya Tanzania ikanufaika na biashara ya Kimataifa hususan kuanzia mwaka huu tutakapotumia soko la pamoja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa Waziri Mkuu akiwa kwenye ziara Mkoani Mtwara Tarehe 18 – 24 Novemba 2009 aliona umuhimu wa Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi kuwa ya lami kutokana na sababu za kiuchumi:-

Je, ni lini Barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi, yenye urefu wa kilomita 211 ni Barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Mtwara. Kati ya hizo, kilomita 15 ni za lami. Kutokana na umuhimu wa Barabara hii kiuchumi, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2010/2011, itaitengea fedha Barabara hii kwa ajili ya kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu na hatimaye Barabara hiyo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa sasa, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali kwa kiwango cha changarawe ili kuhakikisha inapitika wakati wote.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yenye kutia matumaini. Hata hivyo, nina maswali madogo mawili:-

Kwa kuwa Waziri anakiri na anakubaliana na mimi kwamba, Barabara hii ina umuhimu mkubwa kiuchumi na ndiyo inayoziunganisha Barabara zote za Mkoa:-

- (a) Je, kigezo hiki hakiwezi kuifanya sasa Barabara hii ipandishwe hadhi kuwa ya Kitaifa?
- (b) Kwa kuwa Barabara hii sasa hivi ina hali mbaya sana; ni mbovu na hasa baada ya mvua za masika; kati ya Mtwara na Tandahimba ni kilomita tisini lakini inachukua saa nne au zaidi kwa kutumia gari; je, kuna mpango wowote wa dharura umepangwa na Wizara kuhakikisha Barabara hiyo inapitika wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa pongezi alizotupa. Nami nimrudishie pongezi, kwa jinsi alivyo makini kusimamia maendeleo ya Jimbo lake na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuipandisha daraja Barabara hii ili iwe ya Kitaifa kutokana na umuhimu wake, tuseme tu kwamba, sasa hivi tunao mwongozo na vigezo ambavyo tunavitumia kwa ajili ya kupandisha barabara katika madaraja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kwamba, sasa hivi maadam tumeshaanza kuiingiza Barabara hii katika kuitengeneza katika kiwango cha lami, tufikie hapo kwanza kwa sababu hata kuiweka barabara katika daraja fulani, kusema kweli ni utaratibu tu wa kuhakikisha kwamba iwe inasimamiwa kwa ukaribu zaidi. Barabara ikijengwa kwa kiwango cha lami inaweza kuitwa Barabara ya Taifa, kwa sababu ya umuhimu wake huo. Vigezo tunavyovitumia kwa sasa hivi ni hivyo tulivyonavyo.

Kuhusu hali mbaya ya barabara ilivyo hivi sasa, mimi nataka nikubaliane naye kwamba, kwa sasa hivi barabara nyingi hapa nchini zimeharibiwa na mvua zilizonyesha kwa wingi katika kipindi hiki na katika kipindi hiki Serikali imeendelea kujitahidi kutenga fedha kwa ajili ya kurekebisha maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba, katika mwaka huu wa fedha, barabara hii imetengewa shilingi bilioni 2.1 ambazo zinatakiwa tufanye matengenezo katika vipande vya kilomita mbili kutoka *Mtwara Airport* mpaka Naliendele, kilomita nne, kutoka Barabara za Newala Mjini na kilomita tatu Masasi mpaka Mpeta. Sasa hizi ni jitihada zote za kuhakikisha barabara hii inatengenezwa vizuri. Niahidi tu kwamba, tutaendelea kusimamia yale maeneo mengine korofi kama nilivyokuwa nimesema kwa sababu barabara hii inasimamiwa na *TANROAD* Mkoa wa Mtwara, iendeleo kusimamiwa na kujengwa na kadiri itakavyowezekana iweze kupitika wakati wote. (*Makofi*)

Na. 121

### **Riba za Mabenki Kutazamwa Upya**

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina nia ya kutazama upya suala la riba za mabenki kwa lengo la kupunguza tofauti kubwa baina ya riba za kukopeshea na riba za kukopea ili kuweka mazingira mazuri ya kujenga tabia ya kujiwekea upatikanaji wa mikopo:-

- (a) Je, juhudi hizo zimefikia wapi?
- (b) Je, ni benki zipi zilikubaliana na azma hiyo ya Serikali?
- (c) Je, lengo la kujenga mazingira au tabia ya kujiwekea akiba na upatikanaji wa mikopo limefikia kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-



Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali ambazo zimeweza kusaidia kupunguza tofauti iliyokuwepo baina ya riba ya amana na ile ya mikopo. Juhudi hizo ni kama zifuatazo:-

- (i) Kuweka kiwango cha ongezeko la ujazi wa fedha kinachowiana na mahitaji halisi ya uchumi ili kudhibiti mfumko wa bei ambao ni mhimili mkubwa wa mfumo wa riba.
- (ii) Kuanzisha mchakato wa kuunda chombo cha uwekaji wa kumbukumbu za wakopaji kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taafia za historia, uaminifu na uadilifu wa wakopaji.
- (iii) Kupunguza idadi ya minada ya dhamana za Serikali na hati fungani. Hatua hii imesaidia riba za dhamana na zile za hati fungani kushuka; hivyo, kuchangia kushusha riba za kukopeshea zinazotolewa na benki za biashara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi hizo, tofauti kati ya riba za amana na riba za mikopo zimepungua ingawa siyo kwa kiwango kikubwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu inafuata mfumo wa soko huria, jukumu la Serikali ni kuandaa mazingira yatakayotuwzesha riba katika benki za biashara kushuka. Aidha, kwa kupitia Benki Kuu, Serikali inaendelea kuzishawishi Benki za Biashara kuwa na muundo wa riba unaozingatia mwenendo wa riba katika soko la dhamana za Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, uwekaji wa akiba katika Benki za Biashara umekuwa wa kuridhisha. Hali hii imejitokeza kutokana na mazingira yaliyojengwa na Serikali. Ingawa jitihada zaidi zinahitajika katika kuihamasisha jamii, hasa kwa wale wanaojishughulisha na sekta isiyo rasmi ili waweze kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uwekaji wa akiba. Akiba ya sekta binafsi kwenye benki zetu imeongezeka kutoka 3,353 bilioni mwaka 2005 na kufikia 7,171.3 bilioni mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo, Serikali imejenga mazingira kwa kuanzisha mfuko wa kudhamini mikopo kwa ajili ya miradi midogo na ya kati na mfumo maalum wa kudhamini mikopo kwa ajili ya kuuza mazao nje ya nchi yatokanayo na kilimo. Aidha, mfuko maalum ujulikanao kama mabilioni ya JK umeanzishwa kwa lengo la kuwakopesha wananchi ili waweze kukuza biashara zao na hatimaye kuinua maisha yao. Serikali itaendeleza juhudi hizi ili wananchi wengi zaidi wafaidike nazo.

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Benki Kuu kama *regulator* hakuna kitengo kinachoshughulikia mikopo midogo midogo kwa maana

ya *microfinance*. Je, utaratibu huu anaosema Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hautawasaidia wakopaji wadogo wadogo pamoja na wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokizungumza Mheshimiwa Idd Azzan, lakini kama utakumbuka katika majibu yangu yaliyopita, nilisema kwamba, Benki Kuu inaangalia utaratibu mzima ili kuweza ku-*monitor* hii mikopo na wakopaji wadogo wadogo. Ushauri alioutoa tutauzingatia na tutaufanyia kazi.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68; naomba urejee Kanuni ya 37 unipe mwongozo wako. Kanuni ya 37 kifungu cha (7) kinasema: “Taarifa zinazowasilishwa Bungeni na Kamati yoyote ya Kudumu, Kamati Teule, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pamoja na mapendekezo ya matumizi ya nyongeza za fedha, zitatengewa muda maalum kujadiliwa Bungeni bila hoja kutolewa.” Taarifa za Kamati zilizowasilishwa hapa ulisema kwamba, kwa sababu hoja haikutolewa, kwa hiyo, Wabunge hatutakuwa na nafasi ya kuzihoji; lakini Kanuni ya (7) inatuongoza vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Swali hili nitalitolea mwongozo saa 11.00 jioni; tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Sasa ni matangazo tukianza na wageni kama kawaida. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kwanza ni wageni wa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, ambao ni wanafunzi 16 wa Vitivo mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Dodoma, ambao wanatoka Jimbo la Sengerema, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Jaruma Joseph. Naomba wanafunzi wa UDOM kutoka Wilaya ya Sengerema wasimame na Mwenyekiti wao apunge mkono. Ahsante, karibuni sana. Mbunge wenu anafanya kazi nzuri hapa Bungeni; kwa hiyo, tunashukuru. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mheshimiwa Aggrey Mwanri, ambao ni wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), wakiongozwa na Ndugu Prosper Jackson. Wale wa kutoka Jimbo Mheshimiwa Mwanri; karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, anaitwa Ndugu Suzan Kiwele; yule pale ahsante sana. Karibu sana.

Wageni wa Mheshimiwa Col. Saleh Farrah ni rafiki wa familia ambao ni Bwana Chipegwa Chitojo na Bi. Emmy Chitojo. Hawa ni Wakurugenzi wa *Wende Holiday Resort*. Nadhani sehemu ambayo Waheshimiwa Wabunge mnaifahamu sana kwa sababu naambiwa huduma zake ni za kisasa.

Wageni wa Wabunge wa Mkoa wa Kagera ambao ni Ndugu Goreth Elias Bosco, Katibu wa Fedha na Mipango Umoja wa Vijana CCM Karagwe, ambaye pia ni Katibu wa SACCOS ya akina mama Wilaya ya Karagwe. Naomba wasimame; wale pale pamoja na Ndugu Evodia Dominick, ambaye ni Katibu wa Uhamasishaji Chipukizi Umoja wa Vijana CCM Wilaya ya Karagwe. Ahsante sana, karibuni mmetoka mbali. Natumaini Wabunge wa Wilaya ya Karagwe wanawatunza vizuri hapa Dodoma. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Halima Mdee ni wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), wakiongozwa na Ndugu Richard Mtui. Wapo wageni wengine pia wa Mheshimiwa Halima Mdee kutoka Taasisi ya *Mwalimu Forum* ambao ni Ndugu Reonald Toja, Ndugu Nassoro Issa Mohamed na Ndugu Paul John Mephu. Karibuni sana, tunawatakia mema katika mafunzo na masomo. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, ambao ni Wenyeviti na Makatibu 35 wa Jumuiya ya Wazazi kutoka Kata zote 10 za Jimbo la Kinondoni wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Ndugu Stanley Mkandawile. Wale pale karibuni. Tunafurahi kwamba, mnamunga mkono Mheshimiwa Mbunge aliyepo. Basi endeleeni hivyo hivyo mpaka mwisho, siyo tena muachie katikati. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Manju Msambya ambao ni Alhaji Yahaya Omari Rajab Kalolwa, Mwenyekiti wa Wazazi Mkoa wa Kigoma; naomba asimame tafadhali, ahsante sana. Pamoja na Ndugu Ans Juma Bakila, Katibu wa Wazazi wa Mkoa wa Kigoma. Karibuni sana na pole na safari ya mbali yenye matatizo.

Wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja ambao ni Mzee John Chilipweli, Mwalimu Mstaafu na Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kimara; Mzee Ali Mnyamike, Mwenyekiti wa CCM Tawi la Kibo na Mwenyekiti wa Shina; pamoja na Ndugu Moshi Kaftanyi, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Makubuli Kibangu; yule pale. Pia amewahi kuwa Mwenyekiti wa CCM Tawi la Mwongozo. Karibuni sana ndugu zangu wageni wa Mheshimiwa Keenja.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ambao ni Waheshimiwa Madiwani Wanawake 11 kutoka Wilaya ya Igunga, wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Igunga, Ndugu Mary Ziropa; wale pale, ahsante sana. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, tunafurahi kuwaona hapa na bila shaka tutapata nafasi ya kuonana baada ya shughuli hizi za Bunge, kwa sababu sisi Wabunge wote wa Tabora tulipewa taarifa kuhusu ujio wenu.

Wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ambao wanafanya kazi za kufundisha Shule za Sekondari Mikoa ya Singida, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Tanga, Mbeya na Morogoro, kwa kujitolea chini ya Mpango wa *US Peace Corps*; siwaoni wageni hawa, basi tunawakaribisha popote walipo.

Wageni wa Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro ni wanafunzi wa mwaka wa pili *Masters Degree* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambao ni Ndugu

Emmanuel Saitoti na Ndugu Thomas Eric; wale pale ahsante sana. Hii inadhihirisha kwamba, watoto wa wafugaji pia wanaweza kufika mbali sana kwenye masomo, wako kwenye *Masters Degree*. Ahsante, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ambao ni Ndugu Mwalimu Juma, huyu ni Mheshimiwa Diwani wa Wadi ya Dunga Zanzibar; yule pale, karibu sana Mheshimiwa Diwani. Pia yupo Ndugu Hassan Mwinyi, Mweka Hazina Wilaya ya Kati Zanzibar. Ahsante sana. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Zanzibar. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa wageni, sasa tuna matangazo ya kazi zetu. Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo wakutane. Hakuniomba ridhaa huyu, lakini basi ngoja niruhusu saa tano leo kwa lengo la kukutana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), saa tano katika Ukumbi wa Msekwa B.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane leo saa saba katika Ukumbi wa *Basement*, saa saba mchana.

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ameniomba nitangaze kikao ambacho nimekiidhinisha saa 6.00 mchana, Ukumbi Namba 231, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala. Kikao hiki ni muhimu sana; kuna Maafisa Waandamizi tumewaita kutoka Dar es Salaam kwa jambo ambalo lina umuhimu wa kipekee kwa taifa. Tafadhali Wajumbe wote wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama mkutane pale Ukumbi Namba 231 saa 6.00 mchana.

Mheshimiwa John M. Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali, mkutane saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement B*.

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, mkutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba mchana.

Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Miundombinu, mkutane saa saba mchana katika Ukumbi wa *Basement*. Kutakuwa na mgongano hapa, lakini nadhani Katibu anaweza kusaidia ili wote muweze kufanya mkutano.

Matangazo ya ziada; Waheshimiwa Wabunge, CAG ameleta nakala za taarifa za hesabu mbalimbali zile tulizopata kwa Kiingereza, kwa Kiswahili pamoja CD ambazo zitapatikana kwenye visanduku vya barua. Kwa hakika, jamani kama watumishi wote wangukuwa wanafanya kazi kama huyu CAG, nadhani mambo yangukuwa mazuri. Hebu fikirieni taarifa zile zilivyo nene, tayari ametafsiri katika Kiswahili na zote zimewekwa kwenye CD. Naomba mfano huu uigwe kwa sababu kama linawezekana kwa wenzetu,

nadhani Wizara zote zinaweza. Ni kweli upande wa CAG maslahi kidogo ni *alhamdulillah*, lakini pamoja na hayo tunapongeza sana jitihada hizo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya semina ya kesho, Ofisi ya Waziri Mkuu imeandaa tisheti maalum kwa ajili ya semina ya Kanuni za Sheria Mpya ya Matumizi ya Fedha katika uchaguzi. Tisheti zinapatikana kwa utaratibu maalum pale kwenye chumba cha nyaraka, *ground floor*, Jengo la Utawala. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, zipo tisheti za kutosha na wakati wowote mnaweza kuzipata pale chumba cha nyaraka. Huu ndiyo mwisho wa matangazo. Namwomba sasa Katibu atuelekeze kwenye hatua inayofuata.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010 (*The Mining Bill, 2010*)**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotamka jana wakati wa kuahirisha Bunge, ninao wachangiaji watano, ambao ndiyo watamalizia katika Muswada huu wa Sheria ya Madini. Nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa John Shibuda. Kwa sasa nitaanza na Mheshimiwa Balozi Dkt. Getrude Mongella, atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Dkt. Ngasongwa ajiandae.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Muswada huu wa Madini, ambao umepata hamasa kubwa tangu wakati wa maandilizi mpaka hivi sasa. Katika Muswada huu, itakuwa ni ukosefu wa fadhila kama na mimi sitawatambua kama walivyofanya wenzangu, wale ambao wameandaa Muswada huu tangu mwanzo mpaka kutufikisha hapa tulipofika tukiwemo na sisi Waheshimiwa Wabunge ambao tumekuwa tukichangia mawazo.

Jambo kubwa ambalo limejitokeza katika Bunge hili ambalo tutalimaliza mwezi Julai ni kwamba, tumejenga uwezo mkubwa wa kusoma Miswada, wa kutafakari, wa kuchambua na mara nyingine kazi hii tunapoifanya, kuna watu wanafikiria ya kwamba, Wabunge wanajiandaa kuupinga Muswada. Tunafanya kazi yetu iliyotuleta katika Bunge na kazi ambayo tunategemea tuiboreshe zaidi endapo wapiga kura katika majimbo yetu wataturudisha, kwa sababu sasa tuna uzoefu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la madini duniani lina historia ndefu sana na limepita katika hatua mbalimbali. Wanaosoma historia mtaona historia yake Latin America, mtaona historia ya Afrika na ukoloni umekuja kwa sababu ya watu kutaka kugawana madini yaliyopo. Tukatoka katika hatua hiyo, tumeingia katika hatua ya watu

kupambana katika maeneo yenye madini. Ukiangalia sehemu kubwa zenye mapambano ndani ya Bara la Afrika ni zile ambazo zina utajiri mkubwa, bahati mzuri katika Tanzania, tatizo hilo halikutukumba. Ukiangalia Sierra-Leone na Sudan, vita iliyoko Sudan siyo ya siasa tu ni vita ya mafuta na utajiri mkubwa ulioko ndani ya nchi ya Sudan. Sierra-Leone watu wamekufa kwa sababu ya almasi ziliko katika nchi ile. Congo kama hawatatafuta namna ya kudhibiti rasilimali na utajiri uliopo, vita hiyo itachukua muda mrefu; isipokuwa vita kama hizi mara nyingi zinajificha katika mgongo wa kusema ni siasa tu. Si kweli, vurugu nyingi ni watafutaji wa madini na utajiri uliopo.

Kwa hiyo, mimi naona Sheria hii kama mkombozi mkubwa, ambayo itatusaidia kutuongoza namna ya kudhibiti madini yetu ambayo kama hatungekuwa na Sheria hii, tungeweza kufika mahali tukafikia huko wenzetu walikofika. Sheria hii ilivyoandaliwa na ilivyohakikishwa na Kamati husika, itatuwezesha kabisa kuwa na utaratibu mzuri wa kusimamia. Suala hili la kusimamia rasilimali zetu si geni hata kidogo; tusilifanye geni. Ukisoma Maandiko Matakatifu ya Kiislamu na Kikristo, yanaonesha wazi Mungu alipotuumba binadamu na binadamu alikuwa kiumbe cha mwisho kuumbwa alisema kwamba, nenda ukatawale kwanza vitu vyote hivi vipe majina na binadamu akatoa majina kwa vitu vyote, lakini uvitawale na uvitumie kwa busara.

Kwa hiyo, tunachokifanya siyo kigeni; tunarudi huko, kama tunaamini dini kazi tuliopewa tangu tulipoumbwa, kusimamia vizuri matumizi. Huko nyuma ukiangalia katika Ripoti ya Bomani, utakuta ya kwamba, tulianza kukiuka matumizi mazuri ya rasilimali tuliopewa na Mwenyezi Mungu. Ukirejea pia katika siasa ya nchi hii tangu tulipopata uhuru, ilikuwa wazi kabisa, siasa ya ujamaa iliwekwa kwenye misingi ya kwamba, tutafanikiwa tu kwa kutumia misingi mikuu mine; watu, ardhi, maana yake siyo udongo tu na rasilimali iliyopo, siasa safi na uongozi bora.

Kwa hiyo, sasa hivi vyote katika Sheria hii tumevikamilisha ya kwamba, kuja kwa Sheria hii kunaonesha kwamba, tunataka turudishe usimamizi mzuri katika rasilimali kuu tulizonazo katika nchi hii. Ningependa tu kutoa angalizo katika historia, nchi hii misingi ya ujamaa imekuwa tunaonea aibu. Tunaona aibu kuisema, kuitamka, lakini nimefurahi katika mazungumzo ya watu wengi wamerejea huko. Unapozungumza suala la kujitegemea ni siasa ya ujamaa na kujitegemea. Tulikuwa tumetupa mbali. Unapozungumza ya kwamba, tuweze kuwa tunamiliki madini ambayo ndiyo chanzo kikuu cha *industrialization* na mambo mengine; ni hayo hayo.

Ninachotaka kuongeza ambacho kimekuwa kikitokea, lazima tukiangalie sana katika kutekeleza Sheria hii; ni suala zima la hadithi ya sungura. Sungura alikuwa anakimbizwa akaingia kwenye shimo. Kwa ujanja wa sungura yule aliyemkimbiza, akimshika mguu anacheka, anasema hapa umekosea; akimshika mzizi analia, unaniumiza. Sisi pia tumekuwa na akina sungura wajanja, wanataka wanaposhika mzizi sisi tuseme tunaumia na tunaposhika mzizi walie.

Kwa hiyo, nataka niseme tuangalie sana na tumeona katika mjadala huu tangu maandalizi yake, dalili hizi zipo za kusema hapa tunakosea na hapa sivyo. Hii Sheria tukishaipitisha tuko sahihi, tusije tukasikiliza mayowe ya sungura mjanja ya

kutudanganya tushike mzizi tuache kushika mguu kwa sababu hapo ndipo tutakapokuwa tumemuweza.

Ningenda niseme pia katika kutekeleza Sheria hii tuache woga. Nchi hii woga umekuwa mkubwa mno; utakuta sauti zetu mara nyingi zinatoka tunawaogopa wawekezaji, tunaogopa hiki na kile. Mimi nasema hebu tujaribu kufunga, hivi tukisema mbona Wachina waliweza, walijifungia miaka yote tukawacheka wanavaa suruali sare, wanafanya nini, sasa ni uchumi mkubwa duniani kuliko uchumi mwingine wowote. (*Makofi*)

Mawazo yetu hivi sasa tumerudi nyuma kuliko wakati tumejitawala, wakati tunazungumza juu ya kujitegemea. Kila mara tumepata maneno mfadhili, mwekezaji, basi imekuwa ni misamiati badala ya akili zetu. Hawa wataalam tunaowafundisha mashuleni, sasa hivi ningependekeza ya kwamba, katika kutekeleza Sheria hii, Waziri katika Bajeti ijayo atuletee jinsi utakavyokipanua Chuo cha Dar es Salaam, Kitivo cha Jiolojia. Huwezi kutekeleza bila kuwa *geologist* uliyebobea, huwezi kutekeleza vifungu vya 43, 45 na 11 vya Sheria hii kama huna watu watakaoweza kukaa kwenye meza na wawekezaji wanaokuja kuchimba, wakazungumza lugha ambayo ni sahihi, wakaangalia kwa upana na kwa undani ya kwamba, wana taarifa za kutosha kuweza kufanya maamuzi ya kuwekeza katika nchi hii. Kinachotuponza, wakati mwingine sisi tunangoja *briefing* kutoka nje.

*Briefing* tunamtafuta mtaalamu kutoka nje, ndiye akwambie kwamba shamba lako la mihogo, mihongo iliyoko ndani ni kiasi gani. Halafu apange bei na mimi sasa na-*negotiate* katika *level* hiyo. Kwa hiyo, ninaomba sasa katika kutekeleza Sheria hii, tupanue uwezo wa kujenga wataalam ambao ni Watanzania, ambao tutawaweka katika itikadi zetu waweze kujali maslahi ya Taifa hili kuliko kujali watu ambao wanatoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningepomba sasa niseme kuwa, Sheria naiunga mkono mia kwa mia. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na wengine wote. Haitoshi, bado tuna kazi kubwa katika kuandaa kanuni ambazo zitasimamia Sheria hii. Tuna kazi kubwa sana katika kuweka bajeti, kwa sababu tunafikiria pesa haziji au hatuwezi kuvuna bila kuwekeza katika uchimbaji wa madini. Ni kiasi kidogo sana tunachokiwekeza katika Sekta ya Madini, tunategemea wafadhili, wawekezaji na mambo yote hayo. Biashara haiendi hivyo; ni lazima tuwekeze; kwa hiyo, tunataka bajeti hii ipanuliwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa niliseme ni kwamba; ni lazima pia tuweke mkakati maalum wa kuhakikisha haya madini yanarudi mikononi mwetu Watanzania, kwa kupanua hisa za Watanzania iwe ni katika migodi. Wachimbaji wadogo, sijui wavuvi wadogo, wakulima wadogo ni *terminology* isiyotufikisha popote, yaani tuko na dhana nyembamba; tufike mahali katika kanuni tuoneshe wazi ni lini wachimbaji wadogo hawa wataweza kufika mahali wadhibiti madini ya nchi hii, tusipate tabu tena ya kutangatanga kutafuta wawekezaji kutoka nje. Pia ni vyema kila tunapopiga hatua, tusingalie hesabu tumevuna kiasi gani, lakini pia tuangalie walioko katika maeneo ya madini wamenufaika kiasi gani.

Nilikuwa naangalia takwimu za umaskini, ukitazama ukanda wote wenye madini katika nchi hii, ndiyo wenye *percent* za umaskini zinazoanzia asilimia 60 na kwenda juu; aibu. Hapa tumekuwa tukizungumzia wachungaji au wafugaji ni maskini, wana ng'ombe wengi, hawajui kuwatumia. Walioko kwenye madini, tazama takwimu za umaskini katika Wilaya ya Geita ni juu ya asilimia 66; hii ni aibu. Sasa hiyo dhahabu inachimbwa kutoka miguuni mwao na inapelekwa wao wanabaki palepale. Siwaonei wivu, natamani Ukerewe tungekuwa na dhahabu lakini sitaki, wakichimba tutatumbukia, hatuna nafasi kubwa kiasi hicho tutaendelea kuvua. Asilimia 66 ya Watu wa Geita ni maskini; sasa faida ya kuwa dhahabu ni kama hivi mnavyoshutumu wafugaji. Faida ya kuwa na dhahabu ni nini? Hilo litapaswa lijibiwe kwa makini zaidi; ni afadhali tukomboe sehemu na sehemu za nchi hii kutokana na umaskini na rasilimali zilizopo na hicho kilichobaki ndiyo tukipeleke kwenye maeneo mengine. (*Makofi*)

Pia nchi hii ni aibu kubaki katika nchi za mwisho kabisa katika maendeleo ya dunia kwa rasilimali tulizonazo. Kwa hiyo, tutapaswa kuwa makini, mradi tumeanza hii njia ya kudhibiti rasilimali tulizonazo; tujiulize katika kipindi kinachokuja cha Bunge. Kwanza, nashukuru ya kwamba, kipindi hiki tumefanya kazi kubwa sana; Sheria zote tulizozipitisha ni zile ambazo zinatupeleka hatua nyingine mbele. Wakati tunajenga ujamaa tulikosea kitu kimoja, Sheria hazikuambatana karibu sana na biashara, tuli-*misinterpret* biashara kuwa ni ubepari. Sasa hivi huwezi kufanya hivyo, Wachina wametufundisha na tumeona wanaanza kujenga ujamaa kwa kutumia uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru na niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Namwita sasa Mheshimiwa John Momose Cheyo, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Dkt. Juma Ngasongwa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hoja hii muhimu. Kwanza kabisa, nataka kutoa shukrani zangu za dhati kwamba, nilikuwa katika Kamati ya Mheshimiwa Bomani na kweli Wizara imechukua mambo mengi sana ambayo tulikuwa tumeyapendekeza kwenye Kamati hiyo. Kwa hiyo, hii ni ishara ya kuonesha kwamba, panapokuwa Serikali imetumia fedha nyingi kufanya utafiti juu ya jambo fulani, Serikali imeliangalia na inachukua ushauri ambao unafaa. Kwa hiyo, nakupongeza sana Waziri kwa kufanya jambo hilo.

Pia hii ni wazi kabisa Muswada huu umechangiwa na watu wengi sana na hili nataka kumpongeza Mwenyekiti na Kamati, kwa kuweza kufanya utaratibu watu wengi wakashiriki katika kuutunga Muswada huu. Kwa hiyo, ni Muswada wetu sote kwa sababu tumechangia kwa kirefu. Mimi nitajielekeza tu kwenye maeneo ambayo naona kwamba, yana wasiwasi na kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa watu, nitakazia zaidi sehemu ambayo tunaona kwamba hatujawatendea watu haki ya kutosha. Kwanza, sehemu ya fidia ambayo iko kwenye Sheria, kifungu cha 97.



Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mongella kwamba, sehemu zote zile ambazo madini haya yanatoka, ndiyo sehemu zenye umaskini wa kutupwa. Ni jambo ambalo halieleweki kwamba, mtu upande huu una dhahabu ambayo ni fedha, upande mwingine una umaskini. Mimi naona chanzo chake kikubwa pia ni jinsi Serikali inavyoona haya maeneo. Pakipatikana dhahabu, pakipatikana madini mengine, ndiyo kusema kwamba ardhi ile imepata thamani na kwa hiyo mtu ambaye anapaswa kupata faida ni yule ambaye amekutwa pale na siyo hivyo tu, madini yanachukua ardhi, madini yanakataza watu wasiweze kufanya shughuli za kilimo, hata za ufugaji na mambo mengine na kuna sehemu zingine hata wale wachimbaji wadogo wadogo imebidi wafukuzwe na kwa mamilioni. Hatutaki kukumbusha yaliyotokea Bulyankulu, jinsi watu walivyofukiwa ardhini kwa sababu ya kufukuzwa kuweka sehemu ya mtu mgeni kuja kuchimba dhahabu.

Kwa hiyo, nilitegemea kwamba, kama tulivyosema kwa Kamati ya Bomani kwamba, pawepo na utaratibu mzuri ambao utatuhakikishia kwamba, anayekutwa pale anapata fidia ambayo kweli itamfanya na yeye aone kwamba, Mungu kamsaidia kuwepo pale. Sheria hii inasema ni yale yale ya zamani. Mwanzoni nilishukuru nilipoona kwenye Sera, kipengele cha 5.8, Serikali inasema itatathmini, yaani Wizara ndiyo jukumu lake.

Mheshimiwa Spika, imetajwa kwenye Sera, *you will evaluate*, lakini imekuja sasa kwenye Sheria ni yale yale tu; kwanza, yule ambaye amepewa *mineral rights* yeye mwenyewe ndiyo atakwenda kuzungunza na wananchi pale halafu itafuata sheria na taratibu zingine. Sehemu na taratibu zingine, kwa mfano, mambo ya fidia kufuatana na Sheria ya Ardhi ni sawa sawa na kumpa mtu bure, hakuna lolote. Watu watakuja watasema vitu vyako vya kudumu ni vingapi, sijui kitu hiki, sijui mhogo, sijui miti ya kudumu, nyumba na vitu kama hivyo. Yule ambaye anapaswa kulipa fidia yeye ndiyo anayefanya tathmini. Hatujawatetea watu wetu vya kutosha, sisi tunafikiri kwamba, sheria hii ingeweka bayana kabisa kama Thailand anavyofanya, usipokubaliana na wananchi juu ya kuwapa fidia ambayo inafaa hupewi leseni. Vilevile kama Australia wanavyofanya; usipokubaliana na wananchi juu ya fedha ya kutosha na wao waweze kwenda mahali pazuri hupewi leseni. Hilo ningetegemea kuwa ndiyo jukumu la Wizara. Jukumu la Serikali kila wakati ni kutetea watu wake siyo kumtetea mtu ambaye anakuja kutuletea fedha au kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waziri kwa upande huu bado hujatutendea haki, hajafanya ya kutosha na amesema atahusisha sheria zingine. Mimi naona hayo ni maneno matamu tu; nataka wananchi kokote wanakonisikiliza, Sheria hii haijawasaidia. Bado hatutapata fedha ya kutosha. Nimeridhika kwamba, atakayepaswa kuwa na jukumu la kuwalipa siyo Serikali tena kama pale zamani; ni mwekezaji. Hiyo, angalau imesaidia, lakini bado kwenye thamani hatujafanya vya kutosha. Kwa hiyo, hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, mikataba; chanzo cha utafiti wote huu na ugomvi mkubwa uliopo ni juu ya mikataba ya madini. Nilikuwa naangalia watu ambao wanarekebisha hizi sheria ni wale wale ambao walitusaidia kwenye mikataba ambayo ni mibovu. Nimeshangaa kwamba, badala ya kutafuta sasa sheria hii ifunge kwamba hakuna

ulazima wa kuwa na mikataba, *a special mining agreement*, kama mikataba iliyopo hivi sasa, mikataba hii imetulia hasara. Kwa mfano, sasa hivi bei ya dhahabu imeongezeka lakini kwa sababu wakati ule mlipokubaliana bei ya dhahabu ilikuwa chini, huwezi ukasema kwamba upate *windfall tax*, tumefungwa na mikataba ambayo tumewezeza. Sasa hivi tangu tumekuwa na Kamati ya Bomani, nashukuru Wizara imeongeza sana makusanyo; kwa mfano, *royalties* na bei imepanda imefika karibu bilioni 60 kwa hivi sasa, tofauti na zamani ambapo tulikuwa tunachukua labda bilioni 30.

Kwa kugeuza hii sheria sasa tumesema badala ya kuwa na *net value*, tutumie *gross value*, mara moja fedha ambayo ingeweza kupatikana kwa Serikali inafika karibu bilioni 120. Kwa sababu ya *MDAs* ulizonazo, hakuna chochote ambacho tutakifanya kwa hivi sasa. Kwa hiyo, tunabakia na umaskini ule ule. Tumesema, kwa mfano, sasa hivi tutawapa *MDAs* au *agreement*, kwa sababu tunataka *physical stability*, hali ambayo ni sawa sawa na mapato yao. Ukweli ni kwamba, tunachotafuta hakipatikani. Kwanza, kama *physical stability* inategemea sana bei; bei ya dhahabu wakati ambao mnakubaliana katika *MDAs* hizi ilikuwa karibu dola 500 kwa kila *ounce*; leo ni 1200 na inaweza ikafika hata dola 1500. Sasa hiyo *physical stability* unayoitaifuta iko wapi; *already* mapato yana-*fluctuate* kufuatana na bei, lakini upande wa kodi tumebanwa; sasa sisi tukimbilie wapi? Mheshimiwa Mongella amesema tuko maskini, hatuna shuhuda hatuna nini, sehemu tunapochimba ni sawa.

Kama hatuwezi kukokotoa kodi tutafanya nini, tumekosa kitu gani, tunategemea sheria kama hii ingeweza kutusaidia. Pia tumejua kwamba, mlituahidi kwamba, makampuni mengi hata ile mikataba mibovu, kwa mfano, *15% addition allowance* kwa ajili ya uwezekaji itafutwa, lakini hujatupa ripoti ni kampuni ngapi ambazo zimekubali sasa kufuta yote hayo?

Naambiwa kwamba, kuna kampuni moja ambayo imekataa mpaka sijui mkubaliane juu ya *VAT*; kwa nini jambo hilo halifanyiki? Tutapata fedha kama hatuwezi kupata fedha kutoka kwenye vitu tulivyopewa na Mwenyezi Mungu kama vile madini? Cha kusikitisha, bado sijaona katika Muswada huu mambo ya benki, watu wote tumeng'ang'ania kwa ajili ya *MDAs* kwamba, watu lazima wapeleke fedha nje. Mwaka 2008 tumeonesha hapa jinsi gani ulimwengu umeweza kwenda chini, ume-*collapse*, kwa sababu ya *banking system*. Bado *MDAs* hizi zinakubali kwamba tupeleke fedha zetu nje. Hii inafanya hata namna ya kuweza kudhibiti uchumi kwa kupitia Gavana inakuwa ni vigumu lakini tumefungwa.

Mimi ningeshauri kwamba, sasa hivi labda indelee *negotiation* ili kuhakikisha kwamba, haya makampuni ambayo yalikuwa na mikataba hii ambayo nafikiri siyo mikataba ambayo imesaidia nchi hii na yenyewe ilegeze kidogo waoneshe kwamba, wana *good will* kwa nchi hii ambayo ni maskini, waachie baadhi ya vitu ambavyo tuliwapa bila kuweka fikra za kuisaidia nchi hii.

Mimi ningeshauri hilo; anzeni ku-*negotiate* ili tufike hapa. *Free carried interest* sioni kwa nini iwe *by negotiation*; umetuambia kwenye *section number (5)* hii ni mali ya Watanzania; sasa kwa nini tena unakwenda kubembeleza nichukue 10, 5, 2? Ile *original*

*version* ilikuwa sawa sawa kwamba, wewe kama Waziri ungesema 10% hii ndiyo itakuwa *free carried interest* kwa sababu nimekupa *mineral rights* na ninakupa *literally for free* wewe utengeneze mabilioni. Kwa nini uone aibu kusema kwamba, siwezi kuchukua 10%? Ninaona hii ni *weakness area* ambayo nina hakika tunaweza tukasaidia.

Mheshimiwa Spika, la tatu, nataka kuzungumzia juu ya makosa. Katika *section* ya 18 tumerudi tena kama *colonial laws*, ambapo mtu ukiwa na almasi unakwenda ndani ndiyo maana watu wetu walikuwa wanabugia almasi hata kumi ndani ya mdomo wanatembea. Tumerudia hapo kwamba, mtu ukikamatwa na almasi au madini yoyote unakwenda jela kwa miaka mitatu au unaweza kufungwa mpaka kifungo cha mwaka mmoja; mimi naona hii inaturudisha nyuma haitupeleki mbele. *Section* ya 18, Mheshimiwa Waziri unaweza kuisoma vizuri zaidi. Watu wa Maganzo wanaonisikiliza sasa wajiandae wataishia magerezani, kwa sababu wakichimba vyoo watakutana na *diamond*. Hili siyo jambo la kawaida. Kwa hiyo, ningependa iangaliwe hiyo *section* ya 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho na hapa sitaki ku-*touch* mambo mengine ambayo ameshayazungumza Mheshimiwa Kabwe Zitto.

Sisi tulifikiri kwamba, hata kwenye uongozi wa madini kungekuwa na Waziri ambaye anashughulikia madini tu; Wizara Maalum kwa ajili ya madini. Hiyo ni kwa sababu nchi yetu imepewa madini mengi ambayo yanaweza kutusaidia katika nchi kuimarisha jambo ambalo tulilizungumza; *a mineral authority* na bodi iwe imara zaidi. Tukifanya hivyo, tunaweza kufikiria kwamba, labda tunaweza tukasaidia nchi hii kwa kutumia madini ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu.

Mwisho kabisa, nataka kusesitiza kuwa, nafikiri bado tunaona aibu kutumia vitu ambavyo tumepewa na Mwenyezi Mungu. Nimeangalia *section* ya *uranium*, nilifikiri kwamba ungewekwa mkazo kabisa kwa mambo kama haya, Serikali ndiyo itakuwa wa kwanza katika kuhakikisha kwamba, tunatumia madini haya ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu. Nimeisoma hiyo *section* mambo yako kama vile madini mengine tu. Umezungumzia zaidi juu ya *export* ndiyo wa kuomba ruhusa; mimi naona bado kuna mambo mengi zaidi ambayo tunaweza kuyafanya katika kuiimarisha Wizara hii. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Pili, naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wake katika Wizara; kwanza, kwa kuuleta huu Muswada mbele ya Bunge, lakini pili ni kukubali vile vile kuufanyia marekebisho ya kuuboresha Muswada huu. Kama utakavyoona, Waheshimiwa Wabunge wameona kwamba, karatasi ya marekebisho ni kubwa kabisa. Hii inaonesha kazi nzuri iliyoifanya Kamati ya Shellukindo na wewe mwenyewe pamoja na wadau, maana hata mimi nilishiriki katika mjadala huu na kama mdau, tuliweza kuona mambo mazuri mengi yakiwekwa vizuri katika Muswada huu, jambo ambalo naona ni zuri kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani bado kuna mambo machache ambayo tungependa kuyaona yamebadilika. Kwa ujumla, Muswada huu mpya baada ya kuuleta mbele ya Kamati na hapa Bungeni na kuujadili, naweza kusema huu sasa ni Muswada mpya. Muswada huu mpya ni bora zaidi kwa sababu kwanza unatambua fursa ya Watanzania katika kumiliki madini yetu. Hili jambo ni zuri kwa sababu ni rasilimali yetu. Pili, ninatambua umuhimu wa sekta binafsi hasa kutoka nje, ambayo ina uwezo mkubwa wa kuwekeza katika sekta hii. Jambo hili ni zuri na ndiyo maana kile kifungu cha 43 kilizungumzwa sana kwenye Kamati, lakini tulielewana kwamba, mabadiliko madogo yamefanyika pale. Tulikubaliana kwamba ni muhimu kiwepo kwa sababu mwekezaji gani anaweza kuja katika nchi hii kuwekeza wakati hana uhakika kama mtaji wake utalindwa na kwamba baadaye atapata faida? Kama ni hivyo hawezi kuja, maana la sivyo huyu anakuwa ni mfadhili, lakini kama ni mwekezaji hawezi kuja.

Nataka kulisemea jambo hili na kuliunganisha na *document* moja niliyoipata pale kwenye mkutano inaitwa *Survey of Mining Company* Mwaka 2009/2010, ambayo inaonesha Tanzania kuna sehemu nyingine tumeshuka katika namna ya kutia wawekezaji wenyewe walipokuja kwenye mkutano wetu wa wadau walionesha wasiwasi huu kwamba kutokana na mabadiliko ya sheria hizi, kuna wasiwasi kwamba wawekezaji wakasitasita. Tukikubaliana na Muswada huu, nadhani sasa kutakuwa na *stability* katika *mining regime* ambayo itawezesha uwekezaji uwe mkubwa zaidi. Ndiyo maana katika mjalada kule kwenye Kamati mimi nilishauri na Waziri alikubali kwamba, lazima tuunganishe na ile Sheria ya *EPZ* ya Mwaka 2000 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 kwa sababu mle mnatoa *incentive* kwa ajili ya wawekezaji.

Sasa ingawa kwenye *mining sector* itabidi apate leseni, lakini haijulikani kama akipata hii leseni kwa kuilipia basi vile vile atapata fursa za uwekezaji. Hili hasa ni muhimu katika kifungu cha 59 ambako tunataka *processing, smelting* na *refining*. Pale lazima uwe na motisha fulani za kumwezesha huyu mtu kuwekeza katika sekta hii. Hii *area* ya kuongeza thamani ndani ya nchi ni muhimu sana. Lazima tuwe na motisha ambazo zitakuwepo. Kwa hiyo, sheria ile Waziri anasema ataifanyia kazi na napenda iunganishwe ili Watanzania waweze kunufaika.

Vile vile ninapenda kutilia mkazo suala la *free carried interest share*, mimi naliunga mkono kwa asilimia mia moja. Pia naunga mkono kwamba, kufanyike mazungumzo kwa sababu hoja siyo kwamba wewe una mali; mbona umekaa nayo miaka yote ulikuwa huitumii? Kuna wachumi huwa wanazungumza sana mambo ya *potential* kama ndiyo utajiri. Sasa tuna *potential* kubwa, kwa hiyo, huyu mtu ni tajiri. Hapana bwana utajiri mpaka utoe *potential* iwe tayari kwa kutumika. Ikiwa pale ndani ya ardhi haiwezi kuwa ya maana kwako mpaka itoke juu ya ardhi ili itumike. Kwa hiyo, jambo hili la kuchimba lazima tulitilie mkazo ili liweze kutumika.

Kwa hiyo, nakubali ku-*negotiate* ni jambo la kiungwana ili kuzungumza nao na kukubaliana. Mimi nina hakika wote watakubali watasema lazima Tanzania ishiriki na hili jambo siyo jipya Botswana wanafanya, Namibia wanafanya, Afrika Kusini wanafanya, kwa hiyo, tusipate hofu kwa suala la kuzungumza nao kwa sababu litatilia mkazo mambo yetu vizuri zaidi.

Kutokana na hili jambo sasa la kuwa na *Charity Shared Tanzania*, hapa tutakuwa na mali nyingi pamoja na kwamba, tumebadilisha Sheria ya *Treasury Registrar* tumeiboresha vizuri zaidi, lakini bado nadhani vyombo vyetu vya kushikilia hizi hisa vitakuwa *STAMICO* na *NDC*. Sasa hatuzungumzi sana Sheria humu, nafikiri huu ndiyo wakati muafaka kuipa jukumu zaidi *STAMICO* na kuipa fedha na uwezo, ndiyo chombo chetu cha kusimamia hizi rasilimali ambazo tutakuwa tumechukua *free carried interest shares*. Hizi lazima zisimamiwe na mtu wa kusimamia hiyo atakuwa *STAMICO* au *NDC*.

Sheria za *STAMICO* na *NDC* kwa sasa hazifai, ni sawa sawa na kusimamia mambo hayo. Kwa hiyo, lazima kuziboresha Sheria hizo. Zamani tulipokuwa viwanda, tulitaka sana tuiboresha Sheria ya *NDC*, lakini kila tukienda mbele ya Baraza la Mawaziri tulipata ugomo pale, kwa sababu nadhani tulikuwa bado hatujaanza kuelewana vizuri. Sasa nafikiri mnaweza kuelewana kwa sababu bila kutumia vyombo hivi hamuwezi, ninyi Serikali mtashikaje hizi *share*, hata mkisema *Treasury Registrar* ashike *share* zile bado hawezi, kwa sababu yeye si *manager* anashika kama karatasi tu. Mtu atakayefanya kazi ya *management* na *participation* kama *joint venture participants* lazima atakuwa *STAMICO* au *NDC* na hawa lazima muwaundie mazingira ya kufaa. Lazima muwape fedha na watalaam ambao wanafaa. Ninyi kwenye Wizara pale mnaweza kuendelea na mambo yenu yale ya kutoa leseni.

Hamuwezi kuwa na *economists* wa kiwango kikubwa kwa ajili ya ku-*manage resources*. Hawa lazima wabaki kwenye *NDC* ama *STAMICO*. Sasa kama hamuwapi kule rasilimali hizi, hawawezi kufanya vizuri kazi hizi na tutaendelea kupunjwa. Pateni uzoefu wa India na China. Dada yangu pale Mongella alikuwa anazungumza China kule walijifungia, hawakujifungia kwa tafsiri ya kujifungia kwa sababu walileta *investors* wakubwa sana, lakini wakaweka misingi ya ku-*invest* kwa maana hiyo wakawa-*control* na wakasimamia vizuri. Sasa usimamizi huu si wa Kiserikali, usimamizi huu ndiyo wa *Parastal Sector*, wa *NDC* na *STAMICO*, lazima hawa ndiyo muwape *authority* ya kutosha. Kule mbele Bomani alishauri hilo na hata Kamati imeshauri kuwepo na mamlaka ya madini na Mfuko wa Madini; hivi vyote mimi naviunga mkono lazima viwepo. *At the end of the day*, *STAMICO* na *NDC* ndiyo vitakuwa vyombo vyetu vya ku-*intervene in the economy* na vitatusaidia kusimamia uchumi wetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nataka nisemee wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu mimi natoka katika eneo ambalo wachimbaji wadogo wameleta mtengamano wa kiuchumi hasa pale Mahenge. Pale Mahenge uchimbaji wa *ruby* ndiyo unasaidia kuboresha uchumi. Mji wa Mahenge umezungukwa na mawe tu, kwa hiyo, tunalima mahindi kidogo. Mwaka huu nafikiri tutakuwa na *bumper crops* Wapogolo na Wandamba, Wasukuma wako kule bondeni zaidi wanalima zaidi mpunga siku hizi; jambo la ajabu kidogo lakini wanaendeleza hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini muhimu ni kwamba pale Mahenge hawa wachimbaji wadogo ni lazima lile eneo lao, na hii ninataka kusesitiza, maeneo haya ya wachimbaji wadogo ni lazima wakipewa wapewe mazuri, wasipewe pembezoni kwa sababu wachimbaji wadogo ndio wanaogundua madini kwa ujumla; lakini baadaye katika

kuwagawia, tunawapa maeneo ya pembezoni, hii sio sahihi. Tuwape maeneo mazuri kwa sababu hawa kama nilivyosema siku moja hapa Bungeni, kwamba bei ya mkulima, ndio pesa zake anazoweka mfukoni. Kwa hiyo, kwa mchimbaji hivyo hivyo, mchimbaji mdogo akichimba madini ndio anapata pesa, ndivyo anavyoendesha maisha yake. Kwa hiyo, ni lazima juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanakuwepo na wanakuwepo katika maeneo ambayo watapata madini ya kutosha, sio madini yakiwa mengi lazima apewe mchimbaji mkubwa, hapana bwana! Wapeni hawa, kwanza, wanafanya *income distribution* nzuri zaidi, kwa sababu wachimbaji wadogo nadhani wanafika milioni mbili hapa, sasa wale milioni mbili wakipata pesa nzuri zaidi, ndio una-*distribute income*. Lakini pili, unaongeza kipato na kwa hiyo unapambana na umaskini *more effectively* kuliko kuwapa pesa wakubwa tu peke yao. Kwa hiyo, jambo hili ni lazima tulitazame vizuri na mimi ninataka hili niliweke vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, hili la pili katika wachimbaji wadogo ndio la uboreshaji wa uchumi. Sera yetu ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, hapa ndio mahali pake kwa namna zote mbili; ya wakubwa, wa kati na wadogo. Sasa huu mfuko wa madini wa wachimbaji wadogo, hautoshi, wale wanahitaji sio mtaji tu, wanahitaji pia zana. Tulipitisha Sheria hapa ya *Leasing Finance*, sijui imefikia wapi katika utekelezaji wake? Maana tunapitisha Sheria hapa, zinaweza zikachukua miaka miwili hatujazitekeleza, sasa hii sio sawasawa. Ni lazima tupitische sheria halafu tuzifanyie *follow up*, ili utekelezwaji wake kwa wananchi upatikane. Ndio maana kuna mtu mmoja pale Mpinzani akasema kwamba hakuna *Local Contractors*, eeh, hakuna *Local Contractors* kwa sababu hamna *system* ya kuwazalisha na kuwa-*groom* na kuwaendeleza. Maana tatizo la hapa kwa mfano miundombinu, barabara na kadhalika, hakuna ma-*contractor* wa Kitanzania, wenye zana za kutosha kwa sababu hatuna utaratibu wa kuwakopesha hawa. Hawa Wachina wanaokuja hapa ambao wengine ni *very good* lakini wengine ni hovyoy tu. Kwa mfano, kama wale waliotengeneza barabara ya Manyoni pale, kwa sababu hawana zana, sasa *Leasing Finance* ile, ndio inasaidia. Mfuko huu mdogo wa madini ndio ungesaidia sana kuwapa hawa wachimbaji wadogo fedha kwa ajili ya mtaji na zana, bila zana za kisasa, hawawezi kuchimba madini *effectively*. Kwa hiyo, mimi nasema hili lifuatane na uamuzi wa uwezeshaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna mfuko huu wa uwezeshaji tumeuanzisha hapa, lakini hakuna hela. Mara ya kwanza tuliweka shilingi milioni 400 pale, lakini sasa hivi nimesikia hamna hata hela. Sasa kigugumizi kinatoka wapi? Hii ni Sera yetu ya msingi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Jamani wekeni fedha mle, Serikali nawaombeni, wekeni fedha, watu wakope kutoka mfuko huu wa madini, wakope pia kutoka katika mfuko wa uwezeshaji, sio ule wa mabilioni, mimi sizungumzi huo, mie nazungumzia ule uliokuwa Wizara ya Mipango zamani lakini sasa umehamia Wizara ya Fedha, ule ndio ninaouzungumzia ambao Mwenyekiti wake ni Mzee Kamba. Pale pawekewe nguvu zaidi kama sehemu ya kuwawezesha wananchi kiuchumi; la sivyo, tutakuwa tunazungumza Sera, lakini kuna *very big miss match* kati ya *policy* na *implementation*. Jambo ambalo sio sahihi, nafikiri sahihi zaidi ni kuwa na Sera ambazo zinatekelezeka. Nashukuru kwa kunipa fursa hii. (*Makofi*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuwa mchangiaji katika Muswada huu muhimu kwa uchumi wetu. Kama ada na mimi nianze kwa kuwapongeza wote waliohusika katika kuandaa Muswada huu, kuanzia Mheshimiwa Rais alipoteuwa Tume ya Jaji Bomani, Wizara husika na Kamati ya Bunge. Baada ya pongezi hizo, naomba nichangie Muswada huu na hasa kwa kusisitiza baadhi ya maeneo ambayo ninaona ni muhimu, pamoja na kwamba yameshazungumzwa na mimi vilevile niungane na wenzangu kuyasisitiza.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza, ni *duration* ya *license*. Mimi nataka nisisitize tu kwamba lilivyowekwa kwenye *Section 43* ya Muswada, kusema kweli ndivyo linavyopaswa kuwa tukizingatia kwamba kuna mambo mawili pale, ukubwa wa mashapu na *feasibility study* ya mwekezaji inasema nini, *whichever is shorter*. Kwa hiyo, hilo kwa upande wangu nilitaka nilisisitize.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulisisitiza ni lile la *free carried interest* kwa maana ya haki ya Serikali kuwa na hisa katika mgodi ambao mwekezaji wa nje anakuja kuwekeza. Kimsingi mimi naliona hili kama ni suala la Kisera na kama ni suala la Kisera, sioni kama ni suala la majadiliano. Sisi tupitithe Sera kwamba unapokuja kuwekeza kwenye madini Tanzania, Serikali itakuwa na asilimia kadhaa. Ziko nchi, mathalani Ghana, wanatumia utaratibu huo; wao ni 10% kwamba hiyo ndio asilimia ya Serikali ambayo yule mwekezaji anajua nikienda pale 10% ni hisa za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kulisema hili, nataka niliunganishe na *Section 109* ya Muswada, ambayo inasema kwamba Serikali itazungumza na mwenye mgodi juu ya hisa zitakazokuwa *listed* kwenye *stock exchange*. Lugha iliyotumika hapa ni *stock exchange*. Kwanza, ningependa tuwe wazi na tueleze ni *stock exchange* ipi? Kama tunataka *stock exchange* ya Dar-es-Salaam, basi tuseme ziwe *listed Dar-es-Salaam Stock Exchange, for purpose of clarity*. Lakini vilevile inawezekana tukasema *stock exchanges*, ili kutoa *flexibility* kwamba wanaweza waka-*list* Dar-es-Salaam kama ilivyo sasa wana-*list* Toronto, wana-*list* London, wanaweza waka-*list* Johannesburg na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la madini pamoja na kwamba sehemu ya mapato yake tunayoweza kuyapata kama Serikali ni yale yanayotokana na *royalty* (mrahaba), lakini vilevile sehemu kubwa ambayo inaweza ikatufaidisha kama nchi ni sehemu ya kodi. Sasa eneo la kodi linaweza tu kutuwezesha kupata mapato kama ule utaratibu wetu wa motisha kwa hawa wawekezaji unaenda vizuri na vivutio vinakuwa sio vingi sana kiasi cha kutufanya sisi vile vivutio vikianza kukokotolewa katika mapato, hesabu za mwekezaji zinaonesha hasara. Kwa mfano, kuna utaratibu wa kile tunachoita kuelewa kwamba mitambo inachakaa. Sasa uchakavu wa mitambo katika taratibu za kimahesabu ya kijasibu, huwa inatolewa kila mwaka, lakini hawa wawekezaji wengi hapa nchini katika *MDAs* zilizopo, baadhi yao wamepewa ku-*write off* uchakavu wa mitambo kwa 100% wanapoanza tu. Sasa ku-*write off* au ku-*depreciate* mitambo kwa 100%, ni hali ambayo inafanya yale mapato ambayo yanapatikana hayawezi yakaonesha faida katika kipindi cha muda mfupi. Taratibu zinazotumika sehemu nyingine na sisi tunaweza tukaiga, ni kwamba tuwe na utaratibu wa kuchakaza ile mitambo, yaani kuelewa ile sehemu ya mitambo inachakaa kwa umri wa ule mgodi, kwa kadri ule mgodi

unavyozalisha na mitambo inachakaa. Hivyo, kwa ile *write-off* kwa maana ya *depreciation* inakuwa ni sehemu ndogo tu na sio kama vile ambavyo tunafanya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma Serikali ilifanya makosa katika eneo la *fiscal incentive*, ikaweka 15% kwenye *unredeemable investment*, baadaye Serikali ikaja ikabadilisha sheria ikaiondoa ile *interest* kwenye *unredeemable investment*. Lakini mpaka leo kama alivyosema Mheshimiwa Cheyo, bado yako makampuni ambayo hayajakubali ile 15% iondolewe katika *MDA* ambayo ilikuwa imesainiwa na Serikali. Mimi hapa ningeiomba Serikali iendelee kuzungumza na hawa wawekezaji ili kusema kweli tufikie mahali ambapo tunasema ni *win situation*; wao wapate na sisi tupate.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la madini, naunga mkono kwa dhati kabisa uamuzi wa Serikali kuruhusu uchimbaji wa vito uwe mikononi mwa wananchi. Lakini kama walivyozungumza wazungumzaji waliotangulia, hawa wananchi hawawezi kufanya wenyewe bila kuwazeshwa. Matokeo yake, tutajikuta tuna tatizo kama lile la kwenye vitalu vya wawindaji. Tumepitisha sheria na taratibu hapa, kwamba vitalu vya uwindaji wapewe Watanzania kwa kadri inavyowezekana, lakini utakuta hawa hawa Watanzania kwa sababu hatuna mfumo wa kuwawezesha, wanarudi tena kwa wawindaji wa nje ili wawabebe na wanawatumia katika vitalu ambavyo wamepewa. Mimi sitashangaa, bila kuweka utaratibu wa kuwawezesha Watanzania katika kuchukua fursa hii, tutajikuta wanaenda tena huko huko nje kuwatafuta wabia wa nje ili waje wawasaidie kuwakwamua. Kwa hiyo, watu wa nje wataendelea ku-*play a bigger role* katika uchumi wetu na sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, suala la uwezeshaji ni la muhimu sana kwa hapa pamoja na mawazo yaliyotolewa mimi ningesema kwamba *TIB – Tanzania Investment Bank* – Benki ya Rasilimali ya Tanzania, kama ambavyo tumeipa jukumu la kuanzisha dirisha la kilimo ili kutoa mikopo nafuu kwa wakulima, tuipe na jukumu lingine; wakati tunaandaa taratibu za kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, basi tuanzishe na dirisha la sekta ya madini ili *TIB* iweze kukopesha hawa wananchi. Vinginevyo sera hii nzuri kama ilivyo, haitaweza kufanya yale ambayo tumeyakusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la uchenjuaji na usafishaji wa madini limezungumzwa na liko kwenye sheria. Mimi nataka kulisisitiza tu kwa maana ya kwamba bila kufanya hivyo, kwa maana ya *refining* na *smelting* hapa nchini, siku zote tutakuwa tunadanganywa. Kuna Kampuni ya *Mwananchi Gold Refinery* ilianzishwa pale Dar-es-Salaam, ni kwa nini Serikali isiitafutie ufumbuzi wa matatizo yake ile iwe ndio kiini cha kuanzisha kampuni kubwa ya ku-*refine gold* na pengine mambo mengine au madini mengine ambayo tunaweza tukayasafisha hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa ninazungumzia suala la wawekezaji wadogowadogo na kwa maana hiyo wawe ni Watanzania tu na hasa kwenye vito, nilikuwa nataka kuikumbusha Serikali kwamba, wakati huu tunapoizungumzia sheria hii, tayari katika eneo hili la uchimbaji wa vito, kuna wawekezaji wa nje na kwa sababu wapo



na walikuwepo kisheria, ni vizuri sheria hii ikafahamu hivyo na ikaweka utaratibu wa kisheria ambao utawafanya hawa wawekezaji wakati wanapoondoka kuwapisha wazalendo, waondoke kwa utaratibu ambao hautatuwekea kivuli kibaya katika mataifa ya nje; kwamba walikuja tukawakaribisha na sasa tunawafukuza kama vile hatuwataki kabisa, hapana. Sheria iweke utaratibu wa ku-*manage transition* vizuri bila ya kuleta mgogoro na mataifa ya nje na wale ambao walikuja kuwekeza hapa nchini kwa dhamira nzuri tu ya kuelewa kwamba Tanzania ni mahali pazuri pa kuweza kwenda kufanya *investment*.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na masoko yetu ya madini yanayoeleweka hapa hapa nchini, ni suala muhimu sana hasa kwa wachimbaji wadogo. Watachimba, watakuwa na hivyo vito, watakuwa na hayo madini, lakini bila ya kuwa na *organized marketing channels*, itakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, ninasisitiza kwamba sheria iweke utaratibu wa kuwawezesha hawa wachimbaji wadogo kuwa na utaratibu wa kuweza kujua akiwa na mali yake na dhahabu yake, ataiuza wapi, kwa watu ambao watawapa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda Kitengo cha Kusimamia Utaratibu wa Uchimbaji wa Madini Migodini pamoja na Mahesabu ya Makampuni ya Migodi – *Tanzania Mineral Audit Agency*. Kitengo hiki ni muhimu sana, kimefanya kazi nzuri, kabla ya hapo, Serikali ililazimika kutumia huduma za kampuni ya kutoka nje inayojulikana kwa jina la *Alex Stewart*. Hawa walikuwa ni kampuni ya nje na walikuwa wanalipwa pesa nyingi za kigeni. Serikali imeanzisha kitengo chake chenyewe, kinafanya kazi ile ile, tena kwa kutumia wazalendo wake, hapa mimi napenda kuipongeza na kuihimiza Serikali izidi kuwapa nguvu na ikiye nguvu kitengo hiki ili kiweze kutimiza kazi hii muhimu sana ya kukagua mazao ya madini na kuthibitisha mahesabu ya haya makampuni ili mwisho wa siku tunapojaribu kuangalia kwamba je, makampuni haya yanapata hasara au faida, tuweze kuwa na uhakika kabisa kwamba yanapata hasara au faida ya haki kwa sababu tuna watu wetu wanafanya kazi hiyo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, la msingi lingine ni *institutional capacity*. Imezungumzwa na wazungumzaji waliotangulia kwamba kama Serikali, bila kutengeneza au kujenga uwezo wa vyombo vyetu hususan *NDC* na *STAMICO*, hatuwezi kuisimamia vizuri sekta hii ya madini kwa maana ya zile hisa za Serikali. Hisa za Serikali ni lazima zipitishwe kwenye chombo muhimu ambacho kiko pale kufanya biashara na kina utaratibu na wataalamu wa kuweza kufanya kazi ile na sio Serikali, Serikali haifanyi biashara. Kwa hiyo, tunahitaji kuviendeleza vyombo hivi *STAMICO* na *NDC* ili viwe ndio vyombo ambavyo vitaisaidia Serikali kushikilia hizo hisa ambazo Serikali itakuwa imezichukua katika hawa wawekezaji wakubwa wanaokuja katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa sababu mengi yameshazungumzwa na wazungumzaji waliotangulia, mimi nimalizie tu kwa kusema kwamba sheria hii inatuondoa katika sheria iliyokuwepo ambayo ilikuwa na upungufu. Kwa kiasi kikubwa upungufu uliokuwepo, sheria hii imejaribu kuushughulikia.

Inawezekana kabisa hatujayamaliza yote, lakini kwa kiasi kikubwa, sheria hii imesaidia kuondoka pale tulipokuwa na upungufu mwingi, yale yaliyopo, tutaendelea kuyashughulikia kadri siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante kwa kuniruhusu kuzungumza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ooh, naona Mheshimiwa Shibuda amerudi, sasa nampa nafasi.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kushiriki kwa utimilifu katika kuchangia hoja ya Muswada huu. Wahenga husema “chelewa ufike”, nilikuwepo lakini nilikuwa sionekani tu katika mboni za macho yako. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuipongeza sana Serikali, kwa kuandaa Muswada ambao utabadilisha Sheria ya mwaka 1998 na kufuma Sheria Mpya ambayo itakuwa ni pambazuko jipya kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajielekeza katika hoja ya Muswada huu, napenda kutambua na kupongeza unyeyekevu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambao umejenga subira hadi Muswada huu ukakamilika kwa nenda rudi, nenda rudi, bila kuburuza Kamati na bila kushinikiza kwamba basi Kamati ya Chama ya Wabunge wa CCM tukutane tupitishie hata upungufu uliokuwepo. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa subira uliyoonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mbunge na Waziri Mkuu, amethibitisha ustaarabu wa kwamba tathmini ya uongozi sio ukipata madaraka, umejua kila kitu. Kwa hiyo, ametueleza na ametuonesha kwa vitendo, ametupa somo zuri sana. Muswada huu ulikuwa nenda rudi kwenye Kamati. Nasema tena Waziri Mkuu, alionesha subira na alitambua nia njema ya mawazo ya Watanzania na malalamiko ya Watanzania yaliyokuwa yamezungumzwa kupitia magazeti, vyombo vya habari na vikao mbalimbali, kwa hiyo, akaipa Kamati muda wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili, nitakuwa mchoyo wa fadhila, kama sitawaomba wananchi wa Mpanda Mashariki, wamrejeshe Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kura za kishindo, za maoni na za Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, haya ni mambo mazuri kuyasikiliza, Mheshimiwa AG muache kwanza asikilize. *(Kicheko)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kuwaomba wananchi wa Mpanda Mashariki, watambue kwamba Mheshimiwa Mizengo Pinda, ana sifa za kurejeshwa katika Bunge hili, kwanza ana kiu ya kusikiliza, ana kiu ya

kushaurika, ana kiu ya unyenyekevu, ambayo ni sifa kubwa sana kwa kiongozi kama yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ametoa ushirikiano mkubwa, napenda kuwakumbusha wananchi wa Mpanda Mashariki, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mbunge wenu ambaye ni Waziri Mkuu, ameshirikiana na Bunge na Mheshimiwa Spika, kuhakikisha dhuluma zilizokuwa zikitokea kwa wafugaji, wakulima, zinakomeshwa, kwa hiyo, nawaomba mumppe kura zote. Alizuia dhuluma kwa wafugaji, sasa naomba aendelee kuzuia dhuluma za mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Pinda ana hulka na silika ya baba wa Taifa. Hajikwezi, hongera sana na amethaminika na kusadikika kwa kauli na vitendo vya kujenga ustawi endelevu wa siasa na itikadi ya Chama cha Mapinduzi, pamoja na programu ya Chama tukielekea katika kujenga ujamaa na kujitegemea. Je, nani ana sifa kama hizo Mpanda Mashariki muanze kumletea hila? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wahenga husema, “mnyonge, mnyongeni, lakini haki yake mpeni”. Hivyo, naomba wananchi wa Mpanda Mashariki, watambue kwamba watakuwepo wazushi wenye hila na visa, watakuja na sifa bandia, hao ni makandarasi wa uwongo dhidi ya Mheshimiwa Pinda, naomba msiwakubalie.

Mheshimiwa Spika, wakale husema, “usione chaelea kina wenyewe”, naomba kutumia fursa hii, kuwaambia wananchi wa Urambo Mashariki, ajabu Mheshimiwa Pinda Mpanda Mashariki na Mheshimiwa Spika, Urambo Mashariki, ewe Mola ahsante sana kwa vile jua huwa linaanzia kuchomoza kutoka Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba wana Urambo Mashariki, watambue na kubainisha kwamba, kipindi hiki ni cha mazalia ya mbu, mbu hao wanang’ata kwa uwongo na uzushi, msipoangalia, mtaambulia matende kama mtampoteza Mbunge wenu, Mheshimiwa Samuel Sitta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili, wananchi wa Urambo, naomba pia mkubali kwamba kwa kuwa ni Spika, sauti yake husikilizwa, hivyo Serikali hutekeleza kwa hatua mahitaji ya Urambo Mashariki na utekelezaji umekuwa mkubwa. Lakini wanasema, “Nabii haaminiki kwao”, natambua ukiwa na jirani mlevi, ana hila na visa, kuuchafua usingizi wa mwenye nyumba. Kwa hiyo, nawaombeni wana Urambo, mpige vita wote watakaokuja kwa visingizio vya ujirani mwema kumbe kwa visa. Napenda kusema kwamba hakuna mtu binafsi mwenye mtaji wa kujenga vituo vya afya, kujenga visima, kujenga shule, kwa hiyo, hata Wabunge mnaotaka kuwalaumu wamewafanyia nini, jjulizeni na nyie mmechangia nini kwa ustawi wa maendeleo ya kaya zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia imani ya Chama cha Mapinduzi na Katiba na Kanuni za Chama, amesimama imara. Amesimama imara, kusimamia haki za

wafugaji, uzalendo wake, ni mkubwa na ninaomba wananchi wa Urambo Mashariki, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amelinda matakwa ya Katiba ya Nchi, kwa hiyo, mtu anayetaka kufikiria Mheshimiwa Spika ni mbabe, mwongo, someni Katiba ya nchi mtajua alikuwa analinda Katiba ya nchi na matakwa ya Katiba ya CCM yaliyoasisiwa na kilio na kiu ya TANU na AFRO-SHIRAZI, kwa maslahi ya maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umewezesha Bunge kuwa dobi wa kung'arisha Chama cha Mapinduzi na kung'arisha Serikali, kwa hiyo, nawaomba wenye hila mjiepushe maana "asiyejua maana haambiwi maana". Bunge ni kioo cha sura ya kulindwa na kutetea maslahi ya umma, kwa hiyo, nawapongeza Wabunge wote. Tumetekeleza wajibu wetu wa kulinda na kutetea maslahi ya umma kama tulivyokula kiapo cha kulinda na kutetea Katiba. Wale ambao wanakuja kila siku, wanajitangaza kwamba tunataka kuwang'oa Wabunge, Wabunge sio mihogo, nendeni mkang'oe mihogo mashambani. Aidha, napenda kuwaambia kwamba, Ubunge sio tunda mwitu, napenda kuwatahadharisha wanaotaka kuwang'oa Wabunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nijielekeze kwenye Muswada huu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nitachangia kwa ujumla kuhusu Muswada huu, napongeza Sheria hii, kwa sababu ni ibuko na pambazuko jipya la kutekeleza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Vile vile Sheria inajenga programu ya Chama iliyoasisiwa tangu enzi ya TANU na AFRO-SHIRAZI ya kwamba, ukombozi wa Watanzania upo ndani ya TANU na AFRO-SHIRAZI na ukaasisiwa na kurasimishwa na Chama cha Mapinduzi, hakuna Chama mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana makada wa Chama cha Mapinduzi ambao ni Mheshimiwa Ngeleja pamoja na Mheshimiwa Malima, watendaji wote pamoja na Kamati, kwa jinsi walivyoshiriki kuhakikisha kwamba tunakwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatahadharisha Watanzania na viongozi wangu wa Serikali kwamba hakuna Bwanyenye ambaye yupo tayari kumpa mtaji Boi wake ili ajitegemee lakini Bwanyenye yuko tayari kumpa Boi dawa ili apone aendelee kuosha nguo, toto iko kunya, safisha guo, nilipenda hili niliseme.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutanabaisha kwamba misaada yote tunayopata kutoka nje, ni sawasawa na dawa anayopewa Boi ili aendelee kumtumikia Bwana wake. Tusitake kujitegemea kwamba wawekezaji kutoka nje, ni msingi wa kujenga ujamaa na kujitegemea na ni msingi wa kutetea uhuru na maendeleo ya Watanzania, hakuna mtu anayeweza kukusaidia kwa misaada ya kutoka nje, hata baba husema, mwanangu nimekupa mtaji na wewe umezidi kuwa ombaomba, sembuse mtu asiyekuwa ni ndugu wa damu?

Mheshimiwa Spika Sheria hii ni mwendelezo wa kubadili tabia ya nchi, ya matumizi ya rasilimali zetu. Napongeza sana kwamba sheria hii ni mwenendo mpya kutumia rasilimali zetu kwa matumizi ya faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania au Tanganyika, tulikuwa ni malighafi ya kuendeleza viwanda vya Ulaya, sasa ninaomba madini ya Tanzania pamoja na pamba ya Tanzania ambayo pia ni madini ambayo inaitwa dhahabu nyeupe, tuilinde na tuitunze kwa faida ya Tanzania.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, dhahabu nyeupe ambayo ni mgodi, hivi karibuni umevamiwa na kanuni ambazo ni potofu. Mgodi wa dhahabu ambao unaitwa pamba nyeupe, hivi karibuni na hivi sasa unadhulumiwa na wauzaji wa madawa ambao hawana mfumo wowote badala ya mfumo wa *passbook* uliokuwepo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu tutembelee Mkoa wa Shinyanga, hususani Maswa kwenye kitovu cha bustani ya dhuluma mbalimbali, naomba uje utuondolee utalii wa kudhulumika wananchi wa Maswa.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii imefungua sura mpya ya kuaminika uzalendo wa Baraza la Mawaziri. Naomba muendeleo kuwa na kanuni ambazo zinalinda maslahi ya Katiba ya nchi na ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi. Nawaomba msimamie kuendeleza imani ya wananchi na itikadi ya wananchi kwa Chama cha Mapinduzi kwa sheria za mfano huu. Lakini kioo husadikisha sura ya binadamu, sheria husadikisha mfumo wa Serikali wa kuthamini maslahi ya umma. Sasa, Sheria hii imekidhi hayo, nakiri kwamba utafiti huimarisha nguvu za hoja.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawapongeza Waziri Ngeleja na nawaomba wananchi wa Sengerema, mrejesheni. Nampongeza Mheshimiwa Malima, mrejesheni, nampongeza Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti, jamaa huyu ni mtu mkomavu, arejeshwe, naomba hayo bila aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kutumia fursa hii, kushauri Bunge tujiamarishe ili tuwe na Kitengo cha Uandishi wa Sheria, ili tuelekane na nenda rudi, nenda rudi na tuelekane na hodhi ya uandishi wa sheria kuwa wa Idara moja tu chini ya AG.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Wanasheria wetu walioshiriki kuhakikisha kwamba tunakuwa na sheria bora. Tunahitaji kuwa na unyenyekevu mkubwa kwa Mawaziri wote kuwa katika mfumo wa Serikali. Tafakari njema zinapunguza fitina na hila za vyombo vya habari. Nawapongeza Waandishi wa Habari, kwa kuwa vipaza sauti vya wanyonge lakini na mjiepushe kuwa mawakala na muepukane na Waandishi wa Habari ambao ni makasuku wa hila na fitina. Ni kweli kwamba ukweli una adha kwa masikio lakini napenda kusema udalali wa uwongo ni jambo ambalo lazima mkomeshe kutuonea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kuishukuru Serikali kwa kutuongezea Jimbo la pili. Napenda kusema kwamba nashukuru sana kwa sababu mkia wa tembo ni mdogo lakini huondoa mauzi ya inzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru sana kwamba tumepata Jimbo la pili, nawashukuru wananchi wa Maswa, kwa moyo mmoja ambapo wamekuwa wakinipa ushirikiano katika Majimbo yote mawili, nami nawaahidi wananchi wa Maswa sitowakimbia. Nitashirikiana nao kuhakikisha kwamba tunapata Kulwa na Doto katika Majimbo yote mawili. Nawaomba sana wananchi wa Maswa muwe na subira, tusihujumiane kwa maslahi binafsi na nawaomba wananchi wote, msiwahujumu Wabunge kwa maslahi binafsi, tuwahujumu kwa maslahi ya Taifa na Chama cha Mapinduzi, tuhujumiane kwa namna tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, burudani ya uwongo na uzushi, ndugu zangu, sasa hivi haikwepeki. Washona mapambo ya uwongo wako wengi dhidi ya Wabunge. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Spika nimuombe Mheshimiwa Waziri ahimise pia utawala bora ma-DC na ma-DED, wawajibike ipasavyo. Tunapoulizwa Wabunge tumefanya nini na ma-DC waulizwe wamefanya nini kuimarisha utawala bora dhidi ya kero na ma- DED waulizwe wameshiriki vipi katika vijiji kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji bora wa utawala bora pamoja Sera za Chama cha Mapinduzi? Hata viongozi wenzangu wa Chama cha Mapinduzi na sie tujiulize, tumekifanyia nini Chama cha Mapinduzi, usimnyoshee kidole mwenzako wakati yako unajaribu kuyaficha kwa hila na visa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tafsiri ya baadhi ya kauli zako Mheshimiwa Shibuda, ni kwamba sasa umeacha kabisa kugombea Urais. *(Kicheko)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, mzigo ukitoka kichwani, huteremkia begani, bado nagombea urais, naomba mnichangie pesa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mtoa hoja, Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima, watachukua saa moja ambayo ndiyo haki yao, kwa mujibu wa Kanuni yaani dakika 60. Sasa nikitazama saa, naona hiyo itakuwa ni dakika kumi baada ya saa saba. Kwa maana hiyo, naomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), aweze kutoa hoja ya kutengua Kanuni ya 28(2) ili tuweze kuendelea hadi tusikilize majumuisho ya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ili Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, aweze kutoa ufafanuzi kwa hoja zilizotolewa na Wabunge, naomba kutoa hoja, kwa kutumia Kanuni ya 28(2) kwamba, Bunge lako likubali kutengua Kanuni hiyo, ili Waziri akamilishe majukumu yake hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu, ni kutengua Kanuni ya 28(2) ambayo inatuzimisha tufunge shughuli saa saba, hoja imetolewa na imeafikiwa, sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati na Madini, anazo dakika 20 za kutoa ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Ardhi, *Azza wajalla*, kwa nafasi na fadhila hii, kusimama katika nafasi hii, hapa nilipo, mbele ya Watanzania wenzangu. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa afya, nakushukuru wewe Mwenyezi Mungu, umenikirimu na kwa kadri ya uwezo wako, naomba uzidi kunikirimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba mimi na ndugu yangu William Mganga Ngeleja, tumepewa jukumu la kuongoza sekta hii ngumu sana na kwa zaidi ya miaka miwili sasa, tumekuwa tunafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ni ngumu, nzito lakini inafanywa kwa wepesi kwa sababu ya ushirikiano wa kipekee, tunaopewa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Makamu wa Rais na kwa imani yao kutupa dhamana hii. Pia shukrani za pekee nazitoa kwa Kiongozi Mkuu wa Shughuli zetu za Serikali za kila siku, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa ushirikiano wa kipekee wa kila siku tunaopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana. Kwa namna ya kipekee, tena nalisema hili kwa unyenyekevu wote na heshima kubwa, nawashukuru Wabunge wote. Kila tunaposimama hapa mbele yao kujibu hoja mbalimbali zinazokuja na tunapokutana nao nje, mimi lazima nikiri kwamba kila nikisimama hapa huwa natetemeka sana, imani na ushirikiano wenu katika kutekeleza majukumu haya ya kitaifa, ndiyo yanafanya kazi hii kuwa nyepesi, nakushukuruni sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nina deni la pekee, binafsi, kwa waajiri wangu, wapiga kura wa Mkuranga, wakati tunaanza awamu hii ya 2005, Wilaya yetu ilikuwa nyuma sana kiuchumi na kijamii lakini kwa sasa hivi ni Wilaya ya mfano katika hatua tulizopiga kiuchumi. Tunakusanya mapato mara tano mpaka sita tofauti na tulivyokuwa tunakusanya miaka mitano iliyopita na hiyo kwa namna moja ni kazi nzuri ya Mbunge. Lakini mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa wananchi wa Mkuranga, Mkurugenzi wa Wilaya na Viongozi wa Chama wa Wilayani, Kata mpaka Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa ruksa yako, niseme kwamba, naomba niishukuru familia yangu. Unakumbuka Spika, barafu wa moyo na juzi naomba niseme, kama miezi mitatu, amejifungua mtoto wa kike, kwa hiyo, imekuwa barafu juu ya barafu na mtoto wangu huyo Alia, Mungu ampe uhai wa muda mrefu na ndugu zangu Amani, Ramadhani Kitwana, Munamuhara Jumbe, Tamimu, Abasi na watoto wetu wote kwa ujumla, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhila hiyo kubwa ya familia yangu na Mama yangu mzazi.

Mheshimiwa Spika, hii ni Sheria ya kihistoria na imekuja wakati wa kipekee kwenye historia ya nchi yetu na Bunge letu. Tunakuja ku-*repeal*, kuondoa Sheria ambayo ilipitishwa na Wabunge wenzetu katika mwaka 1998 ambao walifanya kazi kubwa sana kama ambavyo tumefanya sisi lakini kwa nyakati tofauti. Mimi najua kwamba Sheria hiyo ya mwaka 1998, watu wamejaribu kuwa *very critical* kwa ile Sheria lakini wengi wetu hapa tunajua kazi iliyofanywa mwaka 1998 hasa ukizingatia kwamba tulikuwa tunaingia gizani sasa, Waingereza akina Mzee Andrew Chenge na Mzee Cheyo, walioboea kwenye Kiingereza cha *Oxford*, wanajua wana neno moja la Kiingereza wanasema *benefit of Hansard*.

Mheshimiwa Spika, *every thing is easy* unapokuwa na *benefit of Hansard*, kwa sababu *benefit of Hansard* maana yake una uwezo wa kujua kilichopita nyuma na kukizungumzia. Kwa hiyo, tumekaa, tunazungumzia Sheria ya mwaka 1998 na utekelezaji wake *from now* kwa sababu tuna *benefit of Hansard*, kwa hiyo, tunajua wapi tulipojikwaa, wapi tulipokwama, upungufu na kadhalika. Kwa hiyo, ninaamini kwamba hii Sheria ya Madini ya mwaka 2010 tunayokuja nayo ni Sheria nzuri *simply* kwa sababu tuna *benefit of Hansard* na Waswahili tunasema katika maana hiyo, kufanya kosa si kosa, kosa kurudia kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kwamba tumekaa na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini na wadau wote wa sekta ya madini. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri tumekaa nao katika nyakati mbalimbali tumejaribu kupitia maeneo haya mbalimbali maana tukubali kwamba ndani ya miaka kumi au kumi na mbili, Bunge hii na wale watakaokuwepo humu ndani watakuja tena kukosoa sheria hii tuliyoipitia *and that is part of historical process*. Lakini nashukuru Mwenyezi Mungu na nafahamu kwamba, sisi wote humu ndani ya Bunge *we have done our best* ili hii sheria ikidhi mahitaji ya nchi hii kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ya utangulizi, sasa naomba niseme yafuatayo kwa ruhusa ya Waziri wa Nishati na Madini. Katika masuala haya mbalimbali kuna moja limezungumzwa ambalo ni la uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Madini.

Mheshimiwa Spika, hili limezungumzwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Lucas Selelii. Hili la uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Madini kwa lengo la kuendeleza sekta ya madini na maendeleo ya nchi kwa ujumla ni jambo zuri na Serikali italifanyia kazi kwa wakati unaokuja sambamba na utekelezaji wa Sheria hii.



Mheshimiwa Spika, kuhusu jambo hili napenda pia nimtambue Mheshimiwa Pindi Chana ambaye pia alizungumza kwamba ule Mfuko kwa kadri unavyokwenda pia utahusu uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii ili baada ya miaka ishirini au thelathini, generations zijazo, watakapokuja kuuliza sekta ya madini ilichangiaje? Tutasema sekta ya madini ilichangia kwenye chuo cha madini, mahospitali na kadhalika na ni funds maalum ambazo zinakwenda kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, hili jambo Wabunge wamelisemea na mimi nadhani ni jambo zuri, Serikali tunalikubali na tulikuwa tunajaribu kuzungumzia kwenye Kamati kama *sources* zake zinatokana na *royalty* ambapo tumekubaliana, kimsingi siyo kodi, ni *rent*, kiuchumi huwezi, *royalty* ni kodi, *it is a rent*. Kwa hiyo, kama mgawo huo wa *royalty* kwa huko mbele ya safari kulingana na makubaliano yatakayofikiwa baina ya Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Uchumi na Idara nyingine za Serikali, naomba niseme tu kwamba tumelipitia na tunadhani huko mbele wakati wa utekelezaji wa mfuko huu, ni jambo ambalo Serikali itaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hili la kuwawezesha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo, kwa kuwapatia zana za kufanyia kazi, mitaji, masoko, elimu na kadhalika. Mimi labda niseme tu kwamba, hili ni jambo zuri, amelisema Mheshimiwa Mzee Juma Ngasongwa. Kwa kweli ni jambo zuri na linaeleweka na linakubalika. Lakini ni lazima pia tukubaliane kwamba, kwa wale wanaoifahamu vizuri Sekta ya Madini, kazi ya kuwahudumia wachimbaji wadogo wadogo siyo kazi ndogo, ni kazi kubwa kwa sababu kwenye maeneo mbalimbali, wachimbaji wadogo ni wengi.

Mheshimiwa Spika, pia yale mahitaji ya wachimbaji wadogo wadogo kwa kila eneo, ni mahitaji tofauti kulingana na *geographical and geological position* zile ambazo ziko pale lakini na mambo mengine. Kwa mfano, wachimbaji wadogo kwenye maeneo ambayo kuna umeme, ni tofauti kabisa na wachimbaji wadogo kwenye maeneo ambayo hakuna umeme, ule uwezekano wa upatikanaji wa umeme unaotokana na *grid*, unafanya kazi inakuwa na gharama ndogo zaidi kuliko ilivyo sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nilivyosema, tuna Mfuko wa Wachimbaji Wadogo ambao umekuwa *budgeted*, umetambuliwa na Bunge lako hili na kima chake tulichoanza nacho ni kidogo, lakini tunafikiria kwamba unaweza kupata *fund* kutoka maeneo mengine ya Serikali na mapato ni haya mapato yanayotokana na uchimbaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tukiri kwamba katika hili, wachimbaji wadogo wadogo, inatakiwa tuwaangalie kwa jicho maalum kwa sababu ya uwingi wao, lakini pia kwa mchango wa kiuchumi. Wachimbaji wadogo wanatusikia na kama walivyozungumziwa wachimbaji wadogo wa Busanda na wale wa kule kwa Mheshimiwa Lolensia J. M. Bukwimba, kwa Mheshimiwa George Simbachawene kule Winza na wale aliowasema Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na kadhalika. Nimekwenda naye Mheshimiwa Ole Sendeka Mererani, ni lazima Serikali tuangalie namna ya ku-*identify* na kuangalia matatizo yao, lakini pia lazima tupate ushirikiano wa kipekee kutoka kwa wachimbaji wadogo na watambue kwamba lazima tuwaweke katika

*cooperatives* za wachimbaji wadogo wadogo kwani huwezi kuwahudumia *individually* wachimbaji wadogo kwa mamilioni. Kwa hiyo, nataraji na wao wanaelewa tunachokisema, watajipanga vizuri na Serikali tutalifanyia kazi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Wakala wa Ukaguzi kuingizwa kwenye Sheria ya Madini, hii ameizungumzia Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Halima J. Mdee. Wakala wa Ukaguzi, umeanzishwa chini ya Sheria ya *Execute Agency Cap, 245* na majukumu yake yameainishwa kwenye *framework document* inayotokana na Sheria hiyo. Kwa hiyo, kazi kubwa ya Wakala wa Ukaguzi ni *auditing*, ni kazi ya Uhasibu lakini inafanywa maalum kwenye migodi. Kwa hiyo, nadhani tumeipokea na tutaangalia jinsi itakavyowiana na Sheria ya *TRA* na Sheria ya Kodi na kuangalia namna ambavyo hili la *TMA* litapata utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba niliseme kwa kituo kidogo ni hili la *Special Mining Licence*. Hili limezungumzwa kwa upana na ninamshukuru sana Kaka yangu, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, amelizungumza akaliweka vizuri sana kwamba kwa nini pana *element* ile ya *feasibility study versus* ukubwa wa mashapo na ninaomba nilitolee mfano tu kwa sababu hili sasa linaingiliana na suala la kuwa na kitu kinachoitwa *strategic minerals*.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana hasa Mheshimiwa William Shellukindo na Wanakamati wenzake wote na wale waliokuja kwenye Kamati, tumefanya kazi kama alivyosema kwa muda wa siku tano usiku na mchana, tulifika sehemu, tukasema ni lazima tupate namna ya kutambua *categories* tatu za uchimbaji na tukasema kuna uchimbaji mdogo ambao utakuwa *measured* kutoka dola 0-1,000,000, dola 0 maana yake anaweza kuanza mtu kwa nguvu zake mwenyewe lakini uchimbaji wa kati utatoka dola 1,000,000 -100,000,000 na halafu uchimbaji mkubwa sasa utatoka dola 100,000,000 kwenda juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, hapa tuna uchimbaji huu ambao unakuja sasa hivi na ambao utakumbwa na Sheria, uchimbaji wa madini ya *uranium*. *Uranium* kwa sasa hivi eneo ambalo linaonekana lina mashapo makubwa ni eneo la Namtumbo na maeneo ya Manyoni, kwa ujumla wake wakikamilisha *feasibility study* zile, Tanzania itakuwa ni nchi ya tano au ya sita kwa ukubwa wa mashapo ya *uranium* duniani na tunasubiri tupate hizo *feasibility study* zinazokuja na hiyo *investment schedule* lakini tunatarajia kwamba kazi hiyo itafanywa kati ya miaka 12 au 13 au 14. Sasa hizi ni *strategic minerals* na tunatarajia kwamba kwa sababu ya mahitaji ya *uranium* duniani *for another 20 or 30 years to come*, hiyo ndiyo itakuwa *the source of energy* kubwa kwa umeme *especially* kwenye *European Countries* na kadhalika, kwa hiyo, na sisi *we have a power to play*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasema *there are strategic minerals* kwa sababu ya *demand* na kwa sababu ya mambo mengi. Naomba nikubaliane na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa waliosema kwamba lazima Tanzania tutafute *participation* ya namna fulani kwenye *investments* za namna hii. Sasa kwa mfano *investment* hii ya Namtumbo, tunakadiria kwa

awali kwa sababu eneo la Likuyu kule Mkuju ambapo Madini haya yapo, ni mbali kidogo, kwa hiyo, kuna *investment* kubwa ambayo itafanywa ya miundombinu ya barabara, umeme na kadhalika, hii itaongeza *cost* ya ile *investment* kwenda kwenye 3,3050,000 *dollars*. Kwa hiyo, ni lazima Serikali tukubaliane kwamba tukaifanye *investment* hii kupitia *STAMICO* na *NDC*.

Mheshimiwa Spika, pia tunakubaliana na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga aliposema kwamba ni lazima tufike mahali ambapo hii *investment* iwe *listed* kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* kwa namna ambayo Mtanzania wa kawaida akiamua kwamba ana laki moja au laki mbili, aende akanunue hisa pale kwenye *Stock Exchange* na zitengwe hisa maalum ambazo hawa wawekezaji watajua kwamba ziko *available* kwa ajili ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nadhani ushiriki wetu kwa namna hiyo na tuki-*invest* Watanzania laki mbili au laki tatu kila mtu laki moja moja au laki mbili mbili, tutafikia huko na huo ni mfano waliofanya wenzetu huko Malaysia na kadhalika kuingia kwenye miradi ya namna hii isipokuwa Serikali tutaweka angalizo kwamba kabla hatujawaelekeza wananchi wetu kwenda kwenye *investments* za namna hii, lazima sisi kama Serikali tuwe na uhakika juu ya *element* ya *risk*, hatuwezi kuchukua mamilioni ya pesa za Watanzania, tukayatia kwenye *element* ambayo bado hatujapata uhakika nayo. Lakini tukishapata uhakika wa yale mashapo na uhakika wa *value* yake na kadhalika na ndiyo maana tulisema kwenye Kamati kwamba pana kazi kubwa ya Wataalamu wa Uchumi, *Geology* kutubainishia ukweli wa mashapo yale na *value* ya *feasibility study* na kadhalika. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba hii ni Sheria, tunaipasisha hapa leo na naona kwa sura za Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ni dhahiri kwamba Sheria inakaribia kupita akimaliza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini tunafahamu kwamba hii ni hatua ya kwanza ya kazi inayotakiwa kufanywa, kazi yenyewe ni kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Sheria hii na *impact assessment* yake inafanyiwa kazi kwa dhati kabisa ili tusilete mianya ya watu kutuingiza mjini na kadhalika. Kwa maana hiyo, tunatarajia pia tushirikiane na *STAMICO* na *NDC*, kwa Mamlaka walizopewa kisheria lakini pia kwa nyakati hizi sasa tunatarajia *STAMICO* na *NDC* wenyewe wanatambua kwamba wana nafasi maalum na ya kipekee kwa sasa hivi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niseme kwamba kuna masuala yaliyojitokeza ya mazingira ambayo yamesemwa na Mheshimiwa Prof. Mwalyosi na kuna masuala ya huduma za jamii kwenye maeneo ya migodi. Naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mama yangu Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella na wengine waliosema tusiogope kwenda na masuala ya *social responsibility* kwenye hizi *investments* kubwa zinazofanywa.

Mheshimiwa Spika, tumesikia na tumepokea mifano ya *cooperate social responsibility* kutoka kwenye migodi mingine kama Namibia, Mali na kadhalika. Kwa hiyo, siyo kitu ambacho tunakwenda nacho sisi *as a first*, hapana, ni mambo ambayo yamefanyika katika nchi nyingine nyingi. Naomba nikuhakikishie kwamba na sisi

tutaliangalia kwa jicho la karibu na tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambayo ni hisia za Watanzania waliopo huko nje. Kwa hiyo, ni kazi kubwa ambayo mmetupa na ni jambo ambalo linawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa pongezi walizotoa kwenye hili suala la ununuzi wa huduma za bidhaa za ndani. Tulifika sehemu na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Ngeleja, aliweka msimamo wake bila ku-*bunch* katika hili pamoja na kwamba wapo watu wengine waliliona kwamba hili jambo ni zito. Lakini nyanya, kuku, nyama, hivi kweli vitu hivi sijui labda Mzee Cheyo, lakini hivi Wasukuma pale hamuwezi kulima nyanya zikaingia ndani ya mgodi mkipewa utaalamu na nafasi maalum? Kwa nini mpaka nyanya na vitu kama hivyo vitoke nje ya nchi? Kwa kweli tulifika sehemu tukasema hapana! Tunakubali kwamba pana masuala ya viwango na pana masuala ya *quality and quantity* na kadhalika lakini sasa *that is one of the challenges* ambazo Watanzania sasa watatakiwa kuboresha huduma hizi ili ziweze kukidhi mahitaji ya wenzetu wawekezaji na wao tumewaomba wawe *flexible* katika hili.

Mheshimiwa Spika, tutafanyia kazi suala la elimu kwa umma na hili suala la leseni kutolewa bila kushirikisha Serikali za Vijiji, utaratibu wa sasa ni kwamba tukitoe leseni, yule anayepata leseni yake lazima aende kwenye Mamlaka husika huko chini akajisalimishe, atambuliwe na ajieleze. Kuna tabia ambayo imeonekana kwamba tunapotoa hizi leseni, wakati mwingine watu wakifika tu wanaanza kuchimba kwenye shamba la mtu na kadhalika na hii tumeisikia hata Manyoni na maeneo mengine, kwa kweli inaleta *chaos* kidogo. Lakini labda niseme kabla hata ya Sheria hii, Waziri Ngeleja na mimi tulikwenda maeneo mbalimbali ya Tanzania kwenda kuliweka suala hili sawa ili lijulikane kabisa kwamba leseni siyo sababu ya mtu kuingia tu kwenye shamba la mtu na kumfanyia fujo kisha unasema una leseni yako, hapana! Ni lazima uende pale utambue kwamba pana *surface rights* lakini pia pana Mamlaka ya Halmashauri na vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima na taadhima, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, nimshukuru Mheshimiwa William Mganga Ngeleja kwa kunipa nafasi hii pia kwa niaba yake ya kusema machache na mimi nitamke kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa ni zamu ya mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri, kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa majaaliwa yake, kwa kulijaalia Bunge hili Tukufu kufikia hatua hii tuliyofikia.

Mheshimiwa Spika, salamu za pongezi na shukrani kwako wewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyevitwa wa Kamati za Bunge, Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla na wadau mbalimbali ambao wameshiriki kutayarisha Muswada huu. Pongezi hizo zimewasilishwa kwa niaba yangu na kwa niaba ya Serikali kwa ujumla na Mheshimiwa Naibu Waziri, tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kama ilivyo kawaida, kuwatambua wale ambao wamechangia baada ya maelezo na ufafanuzi na hoja ambazo zilikuwa zimechangiwa na hatimaye Mheshimiwa Naibu Waziri kazitolea ufafanuzi, jambo ambalo namshukuru sana na ameunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hoja hii imechangiwa na Wabunge takribani 84, waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 61 na waliochangia kwa kuzungumza ni Wabunge 23.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua hii, nianze kuwatambua Wabunge waliochangia kwa maandishi, nao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Hilda Cynthia Ngoye, Mheshimiwa John P. Lwanji na Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Mkiwa Adamu Kimwanga, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mheshimiwa Batilda J. Burian, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Lawrence Masha, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Eng. Lous Mhina, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Omar Said Musa, Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa George M. Lubeleje. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa kuongea ni hawa wafuatao: -

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, pia alifuatiwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Hamad R. Mohamed, Mheshimiwa

Zitto Kabwe, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Job Y. Ndugai. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Magalle John Shibuda na mwisho amemaliza Mheshimiwa Adamu K. Malima, Naibu Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia jana wakati nikiwasilisha Muswada huu, niliwapongeza wale ambao walituunga mkono wakiwemo Wabunge nje ya Kamati ya Nishati na Madini, napenda kuwatambua ikiwa ni nyongeza kwa wale ambao niliwatambua jana, nao ni Mheshimiwa George B. Simbachawene ambaye ushiriki wake katika Kamati, ulitusaidia sana kufikia hapa tulipo. Lakini pia nilisema Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, uwepo wake umetusaidia kwenye Kamati na pia Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, tunatambua mchango wake ambao ulituwezesha kurekebisha kasoro au kuboresha Muswada kwa jinsi ambavyo tulikubaliana.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kutumia fursa hii sasa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa. Lakini niseme tu kwamba ziko hoja ambazo zitakuwa zinajirudia na tutapenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa utaratibu wa kawaida, baada ya ufafanuzi huu, matayarisho ya jumla kwa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambazo zilikuwa zimetolewa na Wabunge tutazitambua rasmi hapo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kundwa Mamlaka ya Madini. Hoja hii tumeielezea vizuri na inavyoelekea ni kwamba tumekubaliana, Serikali inakwenda kuendelea kuifanyia kazi suala hili. Ni suala zito na kwa kimsingi, linahitaji pia maandalizi ambayo yatahitaji fedha, rasilimali watu na pia uzoefu wa nchi zingine. Kwa hivyo, ni jambo ambalo tumelifanyia kazi na tumelichukua na hii ilikuwa ni mojawapo ya hoja ambazo zilijitokeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Madini, ni hoja nzuri na Mheshimiwa Naibu Waziri ameisemea hili kidogo na niseme tu kwamba ni hoja ambayo tunaendelea kuifanyia kazi. Tunafahamu kuna nchi ambazo kwa kweli kupitia rasilimali hizi ambazo zinaisha, zimeshaanzisha utaratibu mzuri na kama sikosei na kama kumbukumbu zangu ziko sahihi, mojawapo ni nchi ya Trinidad and Tobago, ni hoja nzuri ambayo tutaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu Kifungu cha 17, madini ya vito ya *Tanzanite* ya Mererani kuwa maalum au *specified* na kuwekewa uzio. Suala hili tulishafanyia uamuzi na hivi sasa vipo katika maandalizi ya utekelezaji. Tayari Wizara yangu ilishaandaa tangazo la Serikali kutangaza kusitishwa kusafirishwa kwa *Tanzanite* ghafi kwenda nje ya nchi na tangazo hilo lipo kwa Mchapaji Mkuu wa Serikali ili

kuchapisha Kifungu cha 17 cha Muswada huu. Kwa hivyo, tukishakamilisha suala hili, Kifungu cha 17 cha Muswada huu kitatumika kutangaza *Tanzanite* kuwa madini maalum kwa kumpa Waziri mwenye Mamlaka kufanya hivyo kupitia Kanuni maalum. Kwa hivyo, ni kazi inayoendelea kwa kweli tumeshaanza mapema kidogo. Mheshimiwa Shellukindo na Kamati yake, atakubaliana na mimi kwamba tulivyokuwa Bagamoyo wakati tunajadili Muswada huu au maudhui ya Muswada huu, tuliwapa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba eneo la Mererani lilitengwa kuwa *Mererani Controlled Area*, kwa Kanuni ya *Mererani Controlled Area Regulation* ya mwaka 2004. Hata sasa Mererani kama ilivyo ni *controlled area* na linatakiwa kuwekewa uzio. Tunafahamu imechukua muda kuweka uzio kwa sababu pia ya bajeti zetu lakini ni jambo ambalo kimsingi tulishakubaliana na litaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Tume Huru ya Usuluhishi, ni jambo ambalo tumelitolea ufafanuzi, tutakwenda nalo, tatalifanyia kazi, ni jambo la kwetu na ni jambo lenye maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu vivutio ambavyo vinabagua Kampuni za ndani zinazotoa huduma katika migodi na hii ni hoja ambayo ilitolewa na wenzetu wa Kambi ya Upinzani. Niseme tu kwamba kwa haya ambayo nimeweza kuyangolea kwa sasa hivi, mfano, kuundwa kwa Mamlaka ya Madini, Serikali kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Madini, Kifungu cha 17 kutumika kuitangaza eneo la Mererani kama eneo maalum pamoja na kuanzishwa kwa Tume ya Usuluhishi wa migogoro, ni hoja ambazo zilitolewa kupitia Kamati ya Nishati na Madini iliyowakilishwa na Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati. Ziko hoja zingine ambazo zilikuwa ni za ushauri, tumezizingatia, hazina matatizo lakini tunaishukuru sana Kamati kwa kutushauri hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye Upinzani, kulikuwa na hoja ambazo zilijitokeza. Ya kwanza, ilikuwa ni hiyo kwamba vivutio vinabagua Kampuni za ndani zinazotoa huduma katika migodi. Lengo la Muswada huu wa Sheria, ni kuongeza fungamanisho la sekta ya madini ikiwa ni pamoja na kuhamasisha utumiaji wa huduma za ndani ya nchi, tumelisema, tumeeleza na kimsingi ni jambo ambalo sisi tunaendelea kulitekeleza. Kama tulivyosema, yale masuala ya fedha na mambo mengine, yatarekebishwa kwenye Sheria zinazohusika, lakini Kiserikali, mkakati wa pamoja wa kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyiwa kazi na linazingatiwa na linatekelezeka, unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mikataba maalum kuwa na vipengele vinavyotoa sharti la mgodi kutumia umeme kutoka *TANESCO*. Kimsingi ni hoja nzuri, lakini niseme tu kwamba sababu hii ni Sera ambayo tumeikubali kwamba tushirikiane na sekta binafsi, tutakapoweka masharti ya kuwalazimisha watumie umeme wa *TANESCO* wakati Serikali ina jukumu lake la kuhakikisha inaweka miundombinu itakayoweza wawekezaji kufanya shughuli zao bila ya bughudha tena bila ya wakati mwingine kuongezea gharama ambazo si za lazima endapo miundombinu ingekuwepo tunadhani kwamba haitakuwa jambo jema kulazimisha. Lakini hoja ni ya msingi, sasa Serikali inachofanya ni kuimarisha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sasa hivi tuna mradi ambao tunaita *North West Grid Extension*. Ni mradi ambao kwa mfano maeneo ya Geita na kuelekea Mkoa wa Magharibi, Mkoa wa Kagera, Kigoma pamoja na Rukwa haijaunganishwa na *grid* na kwa sababu tunadhani kwamba tumeshafanya *feasibility study* eneo ambalo tutachukua umeme kupeleka kule ni njia ile inayotoa umeme Mwanza. Sasa umeme unaotolewa Mwanza kwenda kufikia Geita, si mkubwa sana kuweza kuhimili kuusafirisha kwa safari ndefu ya kuelekea Kagera, Kigoma pamoja na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, tunachofanya sisi ni kuimarisha, tunatafuta fedha na tumeshaanza kujadiliana. Wapo wawekezaji ambao tuna mazungumzo na yako katika hatua nzuri, tuimarisha ile *grid* ya kutoka Geita, lakini tutakapochukua, tutachukua kuanzia Kahama tunaunganisha na Geita kwa sababu mpaka Shinyanga kuna ile *grid* yenye msongo mkubwa, tunaotoa pale umeme, tunausafirisha kuelekea, Kagera tunaushusha kuelekea Kigoma na hatimaye tuunganishe na Mkoa wa Rukwa. Ni mradi ambao Serikali imedhamiria kufanya na tuna hakika kwamba tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna mradi mkubwa, tunaimarisha miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Iringa kwenda Shinyanga. Tunaongeza kile kiwango cha uwezo wa kusafirisha umeme mwingi zaidi na matokeo yake, itakuwa sasa umeme huo utatumika kwa maeneo mengi zaidi na hata miradi mikubwa ambayo itahitaji umeme mwingi, itapata. Tuna mradi mwingine wa kutoa pale Morogoro lakini pia tunaanzia Chalinze hapa kwenda Mkoa wa Tanga, tutakwenda mpaka Moshi na hatimaye Arusha kwa ajili ya kuimarisha hiyo miundombinu, haya ni mambo ambayo yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini kulikuwa na hoja ya Waziri na Kamishna wa Madini, kuwa na madaraka mengi sana. Kwa heshima na taadhima, tunaomba nieleweke kwamba, kwa mujibu wa utendaji kazi wa Kamisheni ya Madini ndani ya Wizara ya Nishati Madini, Waziri na Kamishna, hizi ni Taasisi ndani ya Taasisi na si watu binafsi. Kwa nafasi hii, nimwondolee hofu Mheshimiwa Yono Kvela, wakati anachangia alidhani kwa kusema vile sitamwelewa vizuri. Nilikuelewa vizuri rafiki yangu na hili halimlengi mtu, ni jambo la utaratibu wa kawaida.

Kwa hiyo, hili tumelizingatia lakini niseme tu kwamba utendaji kazi wake, maamuzi yake hayafanywi na mtu mmoja kwa sababu kuna utaratibu wa kuamua mambo ndani ya Serikali. Lakini kulingana na taratibu za Kimataifa, Waziri na Kamishna ndio wenye dhamana ya usimamizi katika sekta ya Madini ila tunaangalia nchi zingine wanafanya nini. Sisi leo tuna miaka 10 na kitu kwenye sekta hii tangu tukaribishe uwekezaji mkubwa, lakini zipo nchi ambazo zinazidi miaka 100.

Mheshimiwa Spika, sasa tumejifunza pia tukaona kwamba hapa tulipo na hata tunapoongelea kwamba kwa kipindi cha mwaka 1997 tulipotunga Sera Mpya na sasa na tulivyotunga Sheria Mpya ya mwaka 1998 na sasa kuna nyakati tumeona sekta ya madini ilikuwa inakwenda juu lakini wakubwa kimsingi wasimamizi wake walikuwa ni hawa. Sasa Kamishna wa Madini kama Taasisi, ni chombo kilichoanzishwa mwaka 1926 na enzi zile kulikuwa na vyombo vya namna hiyo, kulikuwa na Makamishna watatu.



Alikuwepo Kamishna wa Madini, Kamishna wa Magereza na Kamishna wa Ardhi. Hizi ni Taasisi ambazo zina *develop* kulingana na muda. Kwa hiyo, unaweza kuona tulipofikia leo hapa, sheria hii na wasimamizi hawa, ndio waliotufikisha hapa mpaka tuna maendeleo tunayoona leo kutokana na mchango katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, lakini ukisoma Sheria hii pia utaona kwamba vipo vipengele ambavyo vinampunguzia Kamishna wa Madini kwa sasa, kwa mfano mojawapo ya eneo ambalo lilikuwa na usumbufu mkubwa, ni kuhusu kutoa leseni za wachimbaji wadogo. Mamlaka hayo sasa tumeondoa yasiwe ya Kamishna tu yanakwenda kufanywa na wale wanaoitwa *Zonal Mining Officers* ambao sasa hivi kwa mujibu wa muundo mpya wa Wizara ya Nishati na Madini kuanzia mwaka 2008, wanakuwa ni Makamishna Wasaidizi, hao ndio watakuwa na leseni hizo.

Sasa hilo ni mojawapo ya eneo ambapo tumepunguzia madaraka. Kwa hivyo, kwa kweli si jambo la kushangaza sana lakini makusudio yetu kama Taifa ya kuanzisha hii mamlaka, ni jambo ambalo litaendelea ili kumpunguzia mzigo Kamishna na Waziri ili hatimaye abaki na mambo ya Sera tu, kwa hivi sasa tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Mfuko Maalum wa Kuendeleza Uchimbaji wa Madini, kama nilivyosema ni jambo jema na Mheshimiwa Naibu Waziri aliligusia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nafasi ya Katibu Mkuu katika usimamizi wa sekta ya Madini, Sheria za Utumishi zimeweka bayana nafasi ya Makatibu Wakuu katika usimamizi wa shughuli za Serikali. Uteuzi wa kujaza nafasi zilizoainishwa katika miundo kwa ngazi zote ikiwa ni pamoja na ngazi za madaraka, hufanywa na Katibu Mkuu wa Wizara husika. Kwa hivyo, ni jambo la kiutendaji zaidi na ndiyo maana pengine unaweza kuona halijitokezi katika Sheria hii na si Sheria hii tu, mara nyingi, Sheria nyingi haziwataji Makatibu Wakuu kwa sababu pia *establishment* yao ipo kwa Sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya Kamishna kuiagiza *Civil Court* kutekeleza maamuzi wanayoyotoa, pengine ni matumizi ya neno tu la hapo lakini kimsingi tunachokisema ni kwamba utaratibu ulivyo sasa ni kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji na anachokifanya yeye ni chombo ambacho si Mahakama kwa namna ile ya Mahakama lakini wanasema *quasi-judiciary*, ni yale maamuzi, si ya kisheria sana lakini yanatakiwa yazingatie misingi ya kisheria lakini pia yanalenga kutoa haki na kutatua migogoro kwa kadri ambavyo inawezekana.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wakala wa Ukaguzi, Mheshimiwa Naibu Waziri amelisemea, hili ni jambo ambalo tunaendelea kulifanyia kazi hasa kwa kuzingatia kwamba kazi zake nyingi ni za *audit*. Sasa tunadhani ni mahali ambapo ni vyema tuangalie kwa kadri tunavyoendelea, watafiti wapo na wakishirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, Mamlaka ya Mapato Tanzania au watafiti kwa kuendelea kubaki katika Wizara ya Nishati na hasa Kamisheni ya Madini, ni jambo ambalo linaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja, sasa hizi ni zile za jumla ambazo zilichangiwa na wachangiaji mbalimbali, sehemu ya mrabaha irejeshwe kwenye maeneo ya migodi. Hili limechangiwa na Waheshimiwa wengi, kwa mfano, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka pamoja na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba. Lakini pia wamechangia, wachangiaji mchana huu akiwemo Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Shibuda, Mheshimiwa Dr. Balozi Mongella, lakini pia Mheshimiwa Dr. Alhaj Juma Ngasongwa.

Mheshimiwa Spika, hili ni suala zuri, tunalikubali kimsingi lakini tunachosema, kwa sasa uwezo wetu wa kifedha kufikia hatua hiyo, tunaamini kwamba twende taratibu hatua kwa hatua na sababu zake kuu si nyingi sana lakini moja ni kwamba, nchi yetu hii ili tuzifaidi vizuri rasilimali zetu zilizoko hapa, tunahitaji kuzifaidi kwa kutumia hatua mbili. Ya kwanza, ni kuimarisha ule uchumi mpana (*micro economy*), hapo ndio tunaangalia huduma hizo za miundombinu, huduma za kijamii, tunaangalia kwa mfano uimarishaji wa barabara zetu, tunaangalia uimarishaji wa Taasisi za Elimu, tunaangalia uimarishaji wa Taasisi za afya, tunaangalia uimarishaji wa mambo ambayo kimsingi yanaonekana ni ya kijamii zaidi kuliko kuwa *specific* katika eneo fulani. Sasa hiyo ni hatua ya kwanza. Leo mtu akiuliza kwamba kwani kwa kipindi hiki tangu tukaribishe uwekezaji mkubwa, Taifa limefaidika na nini? Kwa sababu tumekuwa tukishughulika na hii hatua ya kwanza ya uchumi mpaka si rahisi sana kutafsiri katika uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, lakini tutafikia hapo na imejitokeza kwa mfano uwezo wetu sasa hivi wa kuchangia katika Mfuko wa Maendeleo wa Barabara na wote tunakubaliana, ukilinganisha na miaka 10 au saba iliyopita na sasa, ni mkubwa lakini mojawapo ya vyanzo vya mapato ni Kamisheni ya Madini, ni Wizara ya Nishati na Madini na hasa sekta ya madini. Wote tunafahamu, mimi huwa napenda kutoa mfano, ni miaka 6 au 5 iliyopita, sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa, tulikuwa tunapitia kuzungukia nchi ya jirani, lakini leo kwa sababu ya uwezo wetu pamoja na mambo mengine kuimarishwa na mchango wa sekta ya madini, tunakimbia masaa 12 umeshafika Mwanza au umefika Dar es Salaam. Sasa ni mojawapo ya mafanikio haya. Leo zimebaki kilomita 20 tu hapa ambazo hazijawekewa lami, Serikali imepata wapi uwezo huo, mmojawapo ni huo. Miaka 3 au 2 iliyopita, tulikuja na sera ya kusema kila kijiji kiwe na zahanati lakini pia kila Kata kadri itakavyowezekana iwe na kituo cha afya. Uwezo huu wa kifedha za Kiserikali umetoka wapi, kwa nini haikutokea miaka 10 iliyopita? Pamoja na mambo mengine, hii ni mojawapo ya manufaa tunayopata kutoka kwenye sekta ya madini kwa sababu mchango wake umeimarika.

Mheshimiwa Spika, leo tunasema watoto wetu tuwapunguzie ada na tumeongeza uwezo wa kujenga shule za sekondari kwa kila Kata, pamoja na misaada kutoka kwenye Mifuko, vyanzo vingine ni sekta ya madini ambayo imechangia kiasi kikubwa. Hilo ni eneo la uchumi mpana si uchumi wa mtu mmoja mmoja ambapo kama tungefanya hivyo, tungeweza kuwa na *impact* lakini tunadhani kupata maendeleo ambayo ni endelevu,

tuanze kuimarisha uchumi mpana hatimaye tutakwenda kwenye uchumi wa maeneo au wa mtu mmoja mmoja. Kwa hivyo haya ni baadhi ya manufaa.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia mwaka 2008, tunafahamu sekta ya madini yenyewe tu imekuwa ni mchangiaji mkubwa katika mapato ambayo kama Serikali tumekuwa tukipata kutoka kwenye mauzo ya nje, bidhaa za nje pamoja na yote tunayouza nje ya nchi. Mpaka mwaka 2008, sekta ya madini ilikuwa ndiyo inaingizia Taifa kwa *foreign exchange* zaidi ya asilimia 50, kimsingi ilikuwa karibu asilimia 52. Sasa hizi zinakuja kujitafsiri katika bajeti zetu za ndani. Sasa haya ni manufaa katika hatua hiyo ya uchumi mpana. Sisi tunaamini kwamba tunakwenda, ukiondoa ajira, ukiondoa manufaa ya sasa ya wafanyakazi wanaofanya kazi katika migodi hii walio rasmi wanavyoweza kunufaika, tunaotoka kwenye maeneo ya madini, tunafahamu, huwa napenda kuwauliza wenzangu wanaoifahamu Nyamongo ya miaka saba iliyopita wanaweza kusimama leo wakatuambia kwamba ndio Nyamongo ya sasa? Wanaotoka Kahama miaka nane iliyopita, wanaweza kusema Kahama ya miaka nane na leo ni sawa? Wanaotoka Geita miaka 10 iliyopita, ni sawa sawa na Geita ya leo?

Mheshimiwa Spika, lakini achilia hiyo ongelea wachimbaji wadogo, leo tunasema wachimbaji wadogo hawajawekwa sawa sawa. Lakini ni nani asiyefahamu kwamba mji wa Arusha ulivyo sasa umechangiwa na sekta ya wachimbaji wadogo? Wako watu wananufaika na sekta hii, miji kama ya Mwanza, Kahama, sisi tunaamini kwamba sekta hii imekuwa ikiendelea kuchangia kwa kiwango kikubwa katika Taifa leo lakini tunasema twende kwa hatua na hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo linatufanya kwa sasa pengine si rahisi kutenga asilimia kuirudisha katika eneo *specific*, ni Katiba ya Nchi. Ukisoma Katiba ya Nchi yetu, Ibara ya 9, inasema:-

*“Lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au wa chochote kati ya vyombo vyake na udugu na amani kutokana na kufuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, ambayo inasisitiza utekelezaji wa misingi ya kijamaa kwa kuzingatia mazingira yaliyomo katika Jamhuri ya Muungano”.* Kwa hiyo, Mamlaka ya Nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha-

Mheshimiwa Spika, ukienda pale kwenye Ibara 9(c) inasema:-

*“kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine”.*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ibara ya 9(d) inasema:-

*“Kwamba maendeleo ya Uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja”.*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ibara ya 9(i) inasema:-

“*Kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada za kuondosha umaskini, ujinga na maradhi*”.

Mheshimiwa Spika, sasa unapofikia hapa, unasema tuanze kwanza na hii hatua ya kuimarisha uchumi mpana tutafikia hiyo hatua ya kwenda kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ibara ya 38 na 39 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo Serikali hii ndiyo inatekeleza kwa sababu baada ya Uchaguzi wa mwaka 2005 ndicho Chama kilichoshinda na hatimaye kikaunda Serikali, inaelekezwa tukaipitie Sera ya Madini lakini pia yameelekezwa mambo ya kutekeleza. Mabadiliko ya Sheria tunayofanya sasa, ni utekelezaji wa maelekezo tuliojiwekea katika kuongoza nchi hii. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge twende hatua kwa hatua, tutafikia hatua ya kuimarisha maeneo hayo. Lakini hii haimaanishi kwamba kusiwepo na eneo ambalo tutahakikisha kama madini yapo basi na wao waendeleo kunufaika kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna suala la uanzishwaji wa Mamlaka ya Madini, Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka wamechangia, hili tumelisemea. Pia suala la uanzishwaji wa chombo huru cha kutatua migogoro, tumelisemea.

Mheshimiwa Spika, Muswada unawapa Mawaziri na Makamishna Mamlaka makubwa nimelisemea, uanzishwaji wa Mfuko, Naibu Waziri amelisemea. Kuhusu wachimbaji wadogo, Mheshimiwa Naibu Waziri amelisemea hili, sitapenda kulirudia sana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuweka mkakati wa madini kuchimbwa na Serikali kupitia Taasisi zake. Hawa waliochangia hapa ni Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Lucas Selelii na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Katika hili, nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, tumetoka nalo katika Kamati lakini kimsingi tumeanza kuliongelea kabla. Ni jambo zuri na sisi tumejiwekea mkakati wa utekelezaji na hii ni *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni jambo la msingi na linahitaji maamuzi ya msingi, Serikali itaendelea kulifanyia kazi kwa minajili ya kufikia hatua ambayo kweli katika yale madini ambayo ni *strategic*, kwa nini yasiwe yanamilikiwa na Serikali ama kupitia *STAMICO* au Shirika lingine kama *NDC* ambalo ni Shirika la Maendeleo la Taifa. Ni hoja ya msingi, inahitaji maamuzi ya msingi kwa manufaa ya Taifa letu. Kwa hiyo ni hoja ambayo tunaichukua, tutaendelea kuifanyia kazi. Lakini hata hivyo kwa sasa maeneo mengi yenye madini kama ya chuma, mkaa wa mawe, madini kama ya Arusha kule Lake Natron ya *Soda Ash*, ni madini ambayo bado mpaka sasa yako chini ya Taasisi za Kiserikali. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini ya vito kufanywa na Watanzania peke yetu, tumeshaelezea na hii kwa kweli ni utekelezaji wa Sera yetu ya mwaka jana ambayo imeshaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, masuala ya mazingira yameelezwa na Mheshimiwa Prof. Mwalyosi na Waheshimiwa wengine, wanataka kujua sheria hii inafanya *reflection* kiasi gani kuhusu suala la mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuna vipengele ambavyo vimeainishwa katika baadhi ya mambo. Ukiupitia Muswada ule tumezingatia ingawaje tunafahamu kwamba msimamizi Mkuu wa Mazingira ni Wizara ya Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais (Mazingira) lakini kwa pamoja tunafanya kazi na kiutekelezaji tunakwenda pamoja.

Masuala ya fidia kwa wanaopisha Mheshimiwa Naibu Waziri kalisemea na niseme tu kwamba utaratibu wa kufidia unakuja. Tunakwenda kurekebisha Sheria ya Ardhi lakini kikubwa ni kwamba itatumika *formula* ambayo inatumika sasa ambayo ina manufaa. Nimekusikiliza vizuri Mheshimiwa Cheyo ukisema kwamba Sheria hii hasa kwa wananchi watakaokuwa wanapisha haijaka sawa sana. Sisi tunasema naheshimu sana mtazamo wake lakini nakuhakikishia kwamba kwa mabadiliko yanayokuja sasa *formula* itakayotumika ni nzuri kwa sababu inatambua thamani ya ardhi kwa mtu ambaye ana haki ya kukaa pale na kuitumia.

Tunafahamu madini ni rasilimali ya Taifa lakini kwa formula ile itaendelea kumnufaisha. Ndiyo maana hata kwa sasa kwa kuzingatia Sheria iliyopo ya sasa hivi ya ardhi, pamoja na kwamba tulikuwa tuna matatizo lakini ukilinganisha na hali ilivyokuwa kidogo kama miaka kumi kabla ya Sheria haijarekebisha, sasa hivi manung'uniko yamepungua kwa sababu utaratibu wa kukokotoa mahesabu ya fidia umeboreshwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhusu huduma za jamii Mheshimiwa Naibu Waziri amelielezea. Bodi ya Ushauri ya Madini, tumekubaliana kwamba pengine pale ambapo Bodi hii itamshauri Waziri na kwa sababu kwa sasa hivi inavyoonekana hata akishauriwa anaweza auchukue ushauri au asiuchukue, tunaiboresha hiyo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Waziri naye anawajibika kwa kutoa sababu kwa nini ushauri huo hajautekeleza. Hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu viwango vya Mrabaha na mgawanyo wa mrabaha kwenda kwenye maeneo ya uchimbaji. Hili nimelisemea na kimsingi nadhani tunaelewa vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la leseni za uchimbaji mkubwa limesemewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kama nilivyosema hoja zinajirudia lakini tunatambua. Usimamizi, ukerembaji na urekebishaji wa mazingira limechangiwa na Waheshimiwa wengi sana. Mheshimiwa Chaurembo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mwalyosi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Batilda Buriani, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Hilda Ngoye na Mheshimiwa Khamis lakini yote ni masuala ambayo kimsingi tumeshayafanyia kazi na tumeyazingatia na tunaamini kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna hili moja ambalo Mheshimiwa Cheyo na Waheshimiwa wengine wamelisemea la kwenda ku-*negotiate* hizi *free carried interest* na Mheshimiwa Kaboyonga umetukumbusha pale kwenye *listing* tutazingatia. Lakini hili la kusema kwa nini tukajadiliane? Sisi tunasema Sera zetu zinatambua ushiriki wa sekta binafsi. Lakini maana yake nini kutambua, kisheria huwa tunasema usiseme tu kwamba haki inatendeka lakini uoneshe kwamba kweli mchakato ule haki imekuwa ikitendeka. Sasa hili ni kwamba makusudi mazima ya kwa nini tunakwenda kujadiliana katika hili kwanza, ni kujenga mazingira ya uhusiano wa karibu. Hatutaki tufikie mahali tuone kwamba hawa ni maadui zetu na hawa si wenzetu. Tunasema hivyo kwa sababu mengi yanaweza kusemwa katika sekta ya madini hata sasa, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba na *records* zitaendelea kubaki kwamba sekta ya madini sasa imetunufaisha kuliko miaka kumi iliyopita. Naheshimu mawazo ya kila mmoja lakini kusema kwamba kila siku tumekuwa tukiibiwa si kweli.

Mheshimiwa Spika, eneo mojawapo ambalo pengine hatujaliweka vizuri sana ni msisitizo kwa mfano, kwenye mrahaba unatolewa kwenye madini na dhahabu asilimia tatu. Ni wananchi wengi sana wameaminishwa na labda pengine ni changamoto kwetu, hatujaeleza vizuri sana kwamba unaposema asilimia tatu ya mrabaha maana yake ni kwamba asilimia 97 inachukuliwa na mwekezaji. Hili si jambo la kweli hata kidogo. Ukweli ni kwamba unaongelea habari ya uwekezaji mkubwa mabilioni ya fedha ambayo kimsingi hayatoki mfukoni au kwenye mapipa ya fedha ni mkopo kutoka kwenye taasisi ya fedha ambazo kule kuna *interest* tena kubwa tu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wakija hapa hata kama mgodi hauja-*break even* haujaanza kutengeneza faida bado sisi kuna kodi ambazo tunakuwa tukiwatoza, bado kuna ushuru mbalimbali. Lakini tuisahau ukweli ya mchango wa haya makampuni au wawekezaji wakubwa na hapa simaanishi wawekezaji wa nje tu hata wa ndani. Kwenye ajira leo hii tunasema kuna takribani ajira zaidi ya 13,000 rasmi zinazotambulika acha zile ambazo si rasmi. Nenda kaangalie ile kodi ya mfanyakazi inayoingia katika taasisi zetu za kifedha utakuja kuona mchango wa hizi kampuni ama wawekezaji wakubwa ni kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, pamoja na dunia tunapongea hili suala tuliangalie kwa mtazamo mpana zaidi. Tusiseme kwamba tumechukua asilimia tatu, asilimia 97 amechukua, si jambo sahihi hili na naomba sana ndugu zetu waandishi wa habari mtusaidie na sisi Serikali yetu tunamkakati wa kuelimisha umma tuliweke sawa hili. Unaposema asilimia tatu humaanishi anachukua asilimia 97. Zipo gharama nyingi sana hapa katikati.

Kwa hiyo hili twende vizuri kwa kulielewa na tusifikie mahala sisi kama nchi tukawa na msimamo wa kusema hawa jamaa hawajatufanyia kitu. Kwa kuzingatia haya ambayo nimeyasema haiwezekani kabisa tukafikia *conclusion* tukasema hatuwahitaji wawekezaji wakubwa hata kidogo. Ndiyo maana tunasema hata hili la watu kusema na

naamini si Waheshimiwa Wabunge na sikumbuki nani kasema lakini kumekuwa na hisia za kusema hata tukifunga migodi.

Mheshimiwa Spika, kusema ukweli ni kwamba Taifa hili limekuwepo kwa muda mwingi na madini yetu haya leo tukisema hata wakiondoka, sisi miaka yote hii tulikuwa tunafanya nini kweli. Kwa hiyo, ni changamoto ambazo tumekuwa nazo na ni jambo la wakati huu sasa na ni jambo ambalo limefanyiwa kazi kwa muda ule. Kwa hiyo ni jambo la kulifanyia kazi sisi wawekezaji wa nje na hata wa ndani tushirikiane kama *partners* kwa sababu wote tuna maslahi na tunashughulikia jambo moja. Tunachopigania hapa na hata mabadiliko ya Sera na Sheria hii tunayoipendekeza ni kwa sababu ya kufikia ile hatua inayoitwa *win win situation*. Kwamba kuwe na mizania inayokaribiana kuwa sawa katika kufaidi hii keki ya rasilimali hii ambayo iko hapa.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa ujumla kwamba yapo mengi yamesemwa na sisi kwa upande wetu tumezingatia ushauri wa mambo mbalimbali ambayo yamependekezwa na nataka niahidi kwamba kwa ushauri ambao tumeelekezwa na Bunge lako Tukufu wa kiutekelezaji nataka tuwahakikishie tu kwamba tutaendelea kujitahidi kwa kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atazidi kutujalia, tutatumia maarifa yetu yote, tutatumia akili na uzoefu wetu wote kuhakikisha kwamba Taifa linaendelea kuneemeka na sekta hii ya madini ikiwa ni pamoja na uimarishaji wa sekta zingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nirudie kutambua michango ya Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuongea hapa, walipata fursa ya kuandika lakini kwa nyakati tofauti tofauti mmekuwa mkitushauri kuboresha Sheria hii. Serikali ni sikivu, tumeshirikiana na wadau wote kuhakikisha kwamba Muswada huu unafika hatua tulipofikia.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuwashukuru sana wadau wote ambao wametoa maoni yao na hata wale ambao walikwenda mbele zaidi wakadhani kwamba Muswada huu unaegemea upande mwingine ukweli ni kwamba tunachokitengeneza hapa ni kwa maslahi ya pande zote mbili. Natambua mchango wako Mheshimiwa Diana Chilolo nauheshimu sana, tumeusoma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyawazwa tungependa kupata nafasi ya kusoma mchango wake lakini sina hakika kama Kanuni zinaruhusu, ukamsema mtu kupitia Bunge hili. Mheshimiwa Nyawazwa amemfagilia sana Mheshimiwa Adam Malima, iko kwenye mchango na iko kwenye *Hansard* na kwa sababu hazitofautishi, Mheshimiwa Nyawazwa ameomba kwamba wananchi wa Mkuranga wamkumbuke Mheshimiwa Adam Kigoma Malima wakati utakapofika. Sasa sina hakika kama limo ndani ya Kanuni lakini kwa sababu limeandikwa hata nisipolisema sasa litaingia kwenye *Hansard* na kumbukumbu zitakuja kusema. Yale ya pili uliyoyasema kuhusu Sengerema naendelea kukushukuru sana, lakini nawashukuru wote kwa kutuunga mkono. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shibuda alikuwa msemaji wa mwisho, amemsema Mheshimiwa Spika, amemsema Mheshimiwa Rais na amemsema Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na sisi na Waheshimiwa Wabunge wote na umelisema Taifa lako. Tunaheshimu mchango wako tutaendelea kuzingatia haya ambayo tunasema.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kusema Watanzania wawe na imani, hii ni Sheria yao kwa manufaa yao, wawekezaji wawe na imani, ni Sheria yetu kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunaendelea kuivuna rasilimali hii kwa manufaa ya uwekezaji lakini pia kwa manufaa ya Watanzania. Wako Watanzania wanatutazama leo wakitaka kujua rasimali hizi tunazisimamia vipi kwa manufaa ya Taifa letu. Kwa hiyo naomba nirudie kama nilivyosema jana ulimwengu utuelewe kwa namna yoyote ile Tanzania kuja na Sheria hii haikusudii ku-*undermine* umuhimu wa uwekezaji katika sekta binafsi. Haiwezekani hata kidogo, na ndiyo maana nikasema manufaa ambayo tumeshayapata na tunaona sekta binafsi inaendelea kuwa injini ya uchumi wetu. Lakini kwa sababu tumejifunza mambo mengi na nirudie kusema kwa sababu hata tulipo sasa hata kwa mabadiliko haya ukijilinganisha na yanayatokea katika nchi zingine sisi hatuko katika upande ambako ni chini ya wastani na kimsingi bado tungependa kwenda hatua ya juu kidogo. Lakini kwa kuanza nadhani tunakwenda vizuri. Tunawahakikishia kwamba tunaendelea kushirikiana na sekta binafsi kwa kadri inavyowezekana kuhakikisha kwamba rasilimali hizi tunazivuna kwa maslahi ya wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, niwashukuru sana wananchi wa Sengerema kwa kuendelea kuniunga mkono na hata katika Muswada huu kwa sababu ni jambo ambalo pia tunalifahamu, rafiki zangu kule wanajua, mambo mengi yamesemwa lakini naendelea kuwashukuru kwa ushirikiano wanaonipa. Mheshimiwa Naibu Waziri hongera sana kwa kazi zako, wakati tunakimbizana na Muswada wakati mwingine ulikuwa unajigawa sehemu mbili. Unakuja hapa kujibu maswali lakini kule Mheshimiwa Shellukindo na wengine wanakusubiri. Lakini tumefanikiwa kufikia pazuri. Narudia kutambua mchango wa Mheshimiwa Chenge, ametusaidia sana, nisipoyasema haya nitakuwa namnyima anachokistahili. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa mwongozo wako, umetusaidia na hata pale tulipojisikia kwamba *pressure* inapanda na kushuka ulitupa matumaini na kuendelea kufanya kazi.

Hivyo hivyo, kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, lakini naishukuru sana Kamati mmetuunga mkono mkasimama. Mwanasheria Mkuu na timu yako nafahamu wewe binafsi lakini Mwandishi Mkuu wa Serikali (*CPD*) pamoja na wataalam wetu wa kutoka Serikalini na hasa kutoka Ofisini kwako na hata mahali pengine ambapo inafikia sisi tunasubiri tuletewe mawazo ya wadau wote hamwezi kuanza kuandika, wapo watu wanaotumia muda wa masaa yote usiku mzima, sisi wakati mwingine tunasubiri kuletewa taarifa. Tunamshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi aliyofanya na yeye ndiyo alikuwa jemedari wa wataalam katika mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba hapa tulipofikia tunakwenda na tumefikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, pia kuna Kamishna wa Madini Dr. Kafumu, tunamfahamu amekuwa na sisi pamoja na wataalam wetu kwa ujumla na niseme hili kwa niaba ya



wenzangu, kwa sababu kujadili Muswada huu halikuwa jambo la mazungumzo rasmi tu, wakati mwingine kwenye *corridor* wakati mwingine *canteen*. Endapo kumetokea jambo lolote ambapo pengine kibinadam tumewatendea sivyo, naomba kwa niaba ya wenzangu mtuwie radhi sana. Lengo lilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunafikia muafaka tunaendelea kuhakikisha kwamba Muswada huu unafika hapa na unajadiliwa kwa kina.

Mheshimiwa Spika, sitasahau tena kumshukuru mke wangu Blandina na familia yetu, bila yeye nisingekuwa chochote na naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutusimamia na kutuongoza. Mchakato huu umepitia sehemu kubwa na kuna nyakati ambapo yeye ndiye hasa alikuwa mwongozaji wa shughuli hizi kwenye utaratibu wa Kiserikali. Bila mwongozo wake, ushauri wake na uzoefu wake katika sekta hii pengine tusingefika hapa tulipofika, tunamshukuru sana. Tuombeane kwa ujumla Mwenyezi Mungu azidi kutubariki, aibariki Tanzania lakini tuwahakikishie kwamba utekelezaji wa Sheria hii ambayo tunakusudia kuitunga utaitoa Tanzania hapa ilipo na kuisogeza kwenye hatua inayofuata.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba Waheshimiwa Wabunge tuiptishe Sheria kwa pamoja, tumeitunga wenyewe kwa maslahi yetu, kwa maslahi ya wawekezaji wakubwa na wadogo wandani na nje ya nchi. Tuendeleo kushirikiana tulisukume na tujenge taifa letu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi uliyofanyika. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono lakini kwa kuwa kuna taratibu za kuweza kupitisha na kwa kuwa muda hatuna kufanya saa hizi, kwa hiyo nitamwita Katibu baadaye tuingie katika hatua hiyo.

Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa muda umepita, kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.15 mchana Bunge liliahirishwa  
mpaka Saa 11.00 jioni)  
(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa wakati huu sasa, labda nitoe tangazo moja tu.

Mwongozo wangu kuhusu Kanuni ya 37, kuhusu taarifa zinazowasilishwa mezani, nitautoa baadaye tukiongezeka kidogo na hasa kwa sababu aliyetoa hoja hayupo, ala, ndiyo anaingia sasa. Lakini, bado tuna muda.

Tulivyositisha shughuli za Bunge ilikuwa tayari hoja imekwishaungwa mkono na kilichobaki kwa mujibu wa Kanuni zetu inabidi Katibu atusomee kwa usahihi zaidi ili tuingie katika hatua hii.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010 (*The Mining Bill, 2010*)

Ibara ya 1

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

Ibara ya 3

Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niseme kidogo tu. Kwenye Ibara ya 8(4), mstari wa 3, kutoka chini kwenye *schedule of amendments* kuna neno *amounting not*. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha ya Kiingereza, napendekeza badala ya kuwa *amounting*, tuseme *amount to not more*, kama ilivyo sasa mpaka mwisho.

**MWENYEKITI:** Iliyopo ni *not less!*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Itakuwa *amounting to not more than*, kama ilivyo, maana huwezi ukasema *amounting not*.

**MWENYEKITI:** *Yah!* Mheshimiwa Waziri, sahihisho hilo la sarufi...

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sahihisho hilo tunalikubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, langu ni kifungu hicho hicho cha 8, katika ukurasa wa 3 wa marekebisho. Ile sentensi ya mwisho pale inayosema “*may be granted a mineral right upon rectifying the default*”. Hapa nadhani kwa mujibu wa *interpretation* wametumia *mineral rights* ndiyo ambayo iko katika *interpretation*. Halafu, *rectifying the fault*, siyo *default*. Nadhani tuelewane hilo. Ni rekebisho ambalo tumekubaliana, isipokuwa ni hivyo vikosa vidogo vidogo.

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa William, naona pale juu kwenye 5... “*all Directors of the Partnership or Board of Corporate which is in default*”, kwa hiyo sijui ndiyo mtiririko unasema kwa kuwa yuko *in default* arekebishe ile *default*. Au nilivyoelewa mimi...

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Sasa inabadilika inakuwa ni *fault*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hapa ni *fault*?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Ndiyo! Nadhani Mheshimiwa Chenge, utanisaidia hapa...

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Shellukindo kwa maana kwamba *fault* ndiyo kitendo chenyewe cha kosa, lakini *default* kukosea. Kwa hilo, naamini kwamba Mheshimiwa Shellukindo yuko sahihi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachozungumzia ni *default* wala siyo *fault*. Kwa hiyo, maneno yaliyotumika hapo ni sawa sawa, ni *default and not fault*.

**MWENYEKITI:** Nilidhani hivyo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo hiyo ya 8(4), sentensi ya mwisho na ukisoma kwenye mtiririko kuanzia mstari wa pili kutoka mwisho: “*In the case of one person on the aggregate in the case of more than one person*”. Sasa badala ya *that* iwe *than!* Nafikiri kwamba labda imekosewa hapo. Pale ilipoandika *that one person*, nafikiri ni *than one person*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, kwenye orodha ya masahihisho hapa ukurasa wa 2, sentensi ya chini pale. Labda Mwanasheria Mkuu atusaidie... *more than, Yah, it's*

*more likely* kuwa *than* kuliko *that* kama anavyosema Mheshimiwa. *So*, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ni *than*, nakubaliana na Mheshimiwa Ole-Sendeka.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 9

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 9, nataka tu nipate ufafanuzi. Ibara hii ya 9 zaidi ibara ndogo ya 2, ina msisitizo wa kujaribu kuzuia watu ku-*transfer mineral rights* bila kuwa na *consent* ya *Authority* au ya Waziri. Lakini, ile ya (a) inataka kwamba yule anaye-*guarantee* yuko *approved and known* na Waziri. (b) *a bank*. Sasa *bank* siku hizi inaweza kuwa ni *off shore bank*, inaweza kuwa *anywhere*. Ingingekuwa vizuri pia kwamba *whatever bank* kama inavyosemwa hapa, iwe pia ni *approved bank like all other personalities* ambazo zimetajwa katika sheria hii, kuliko kuicha wazi hivi. Ukiacha wazi, ndiyo kusema tunaliwa hapa. *They can go off shore bank*, wanakabidhi *rights* zenu zote *and there is no follow-up*.

**MWENYEKITI:** Unazungumzia 3(b)? Kwa maana nyingine benki...

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uki-*follow* (a) *to an affiliate*, lakini *approved by licensing Authority*. Ikienda kwenye (b) hakuna *approval of licensing Authority*. *So it can be a bank, can be anything including off shore bank*. Kwa hiyo, ikienda *off shore bank, traceability* ya mali zenu mlizonazo ndiyo zimepotea hivyo na siku hizi *there is so much turn over banks, they change, the names are different*. Hata baadhi ya *Mining Companies they own banks* na sidhani kwamba nahitaji kueleza zaidi. Kwa hiyo, nasema *why don't they add also...they should also have an approval of the licensing Authority!*

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa ni *approved bank* kusudi kukwepa hicho anachozungumzia Mheshimiwa Cheyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10

**MHE. CHARLES M. KAJEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakwenda katika kifungu kidogo (e), ukiangalia katika *schedule of amendment*. Inasema: “*Which guarantee procurement of goods and services*”. Nafikiri kwamba labda tungeongeza neno *competitively available*. *Competitively* nafikiri ni neno ambalo lingetusaidia sana katika kuweza kuwa na uhakika kwamba ni kitu gani tunafanya hapa.

**MWENYEKITI:** Wewe unawatetea wenye migodi sasa!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa kawaida wa manunuzi na kwa utaratibu wa uandishi wa sheria, hatuhitaji kusema hivyo kwamba *competitively* kwa sababu sisi tunachosisitiza hapa ni *procurement* ya bidhaa na huduma ndani ya nchi.

**MHE. CHARLES M. KAJEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaongelea, kwa mfano; makampuni ambayo yanatoka nje, sasa ni lazima vile vile tuangalie kwamba tunalinganisha *quality* ya *services* zetu, *goods* zetu na katika sehemu zingine ambazo wanatoka. Sasa tukiweza kuwa-*limit* tu kwamba lazima wachukue hapa hapa bila kujali *quality, quantity* na *timely delivery* ya hizi *goods and services* tutakuwa hatufanyi nanihi nzuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajeje, lakini kwa kuweka maneno hayo, unawapatia kisingizio hasa hawa *Special Mining License* wawe wanasema bidhaa zenu siyo *competitive* kwa mujibu wa sheria. Sasa itaua hata hiyo maana ya kuweza kupata *local* nanihi. Nadhani tungekubali ilivyo, inawalinda zaidi watu wetu kwa sababu hawa watu wakorofi sana. Mara nyingine kwenye matunda unasikia wanaweza kusema embe ni kubwa mno, siyo mbaya, hii embe yenu ni kubwa mno, hatuitaki. Sasa, vitu kama hivyo vya kupima *size* ya embe, chungwa na vitu vya namna hiyo, ni ujanja tu wa kukwepa kununua matunda au vitu vingine.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena. Kwenye kifungu cha 10(2) mstari wa pili toka chini. Hilo neno *depends* nashauri lisomeke *a mineral rights holder depending on the type of minerals and the level of investment*”.

**MWENYEKITI:** Nilidhani ndivyo ilivyo hii, au illibadilishwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *schedule* ina...

**MWENYEKITI:** Ooh, kwenye *schedule of amendment*! Kwenye Muswada kumbe ilikuwa sawa, badiliko ndilo limeharibu tena.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Kwa hiyo, *it should be...*

**MWENYEKITI:** *You are right.*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho cha 10(2) kama kilivyoboreshwa kwenye *schedule of amendment*, lakini kifungu hiki hakionyeshi lile suala la *listing at a stock exchange*. Tutakuja kukuta tutakapofika kifungu 109 ambacho kinapingana na kifungu cha 10(2). Kwa hiyo, nadhani kwamba tunahitaji kukiboresha kifungu cha 10(2) ili ile *element* ya *listing* ihamie kwenye 10(2) na kuiondoa kwenye 109. Kwa sababu, ukizisoma zote kwa pamoja, ama moja inakuwa ni *redundant* au ina-*contradict*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sijui umeipata vizuri hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Zitto kwa sababu tumekuwa naye kwa muda, hasa wakati wa maandalizi haya ya Muswada huu na hasa wakati Mkutano huu unaendelea. Sasa hapa, ninaelewa, kuna mahusiano, lakini tukifika huko, nitaelezea maudhui ya kifungu cha 109. Yako mambo ambayo kifungu cha 109 kime-*envisage*, lakini hayako *necessarily captured* hapa. Kwa hiyo, kuna mazingira fulani yanaweza kutokea, lakini tutaweza kuelezea.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hiki ni cha ujumla kuhusu *development agreement* na *specifics* ziko kwenye 109.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kutumia kifungu hiki cha 10, dhana hapa ni kumpa Waziri mamlaka ya kuweza kuingia katika mikataba maalum (*MDAs*). Sasa, kwanza kwa uzoefu ambao tumekuwa nao tangu tumekuwa na *MDAs*, nataka kuuliza tu, je, Waziri anaweza kutueleza hapa kama kuna uwezekano wa yale makampuni ambayo ni makubwa na ni mengi zaidi Kanda ya Ziwa kwamba yaka-*migrate* kutoka kwa *MDAs* walizonazo wakaja *in line* au kwa misingi ya sheria hii? Mbele ya safari utaona kwamba sheria hii inatupa *loyalty* nzuri zaidi kwa sababu sasa itakuwa *determined* kwa misingi ya *gross* kuliko *net* kama hivi sasa. Na tusipofanya hivyo, tutakuwa tunapoteza takriban bilioni 120. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili; nataka kufahamu, hapa tumesema hii *free carried interest* itakuwa *negotiated*. Lakini, hakuna *cover* ya sheria ambayo inasema *if in the case* hakuna makubaliano, *then what!* Kama nia na shabaha ni kwamba tupate *free carried interest*, lakini iko *based* kwa *negotiation*, zikifeli *negotiation*, *recourse* ni wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba, jambo hili katika sheria humu humu ndani kila wakati ambapo umeambiwa wewe kwamba unaweza kuruhusu au usiruhusu, umeambiwa *not be withheld*, kuna *coverage* hiyo. Lakini hapa hakuna *coverage* hiyo ambayo kama wewe ukishindwa ku-*negotiate*..., leo ni wewe mtu mzuri, labda mtu mwingine hawezi. Anakuwa *covered* vipi kwamba Tanzania *will still gate a free carried interest*, labda *how much* na nini... ndiyo inaweza ku-*differ*? Ningependa ufafanuzi kwa mambo haya mawili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuhusu *formula* mpya inahusu makampuni pia ambayo tayari yamewekeza na hilo la pili la *disputes* ambalo nilidhani labda kuna *dispute section* huku mbele inahusu *dispute* zote.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hili la kwanza, kama tunavyofahamu utaratibu wa utungaji wa Sheria, Sheria ni *forward looking*, tunaanzia hapa kusonga mbele. Lakini la pili; kama alivyosema Mheshimiwa Cheyo, hakuna kisichowezekana. Kwa hiyo, endapo mazingira yataruhusu na Serikali ikaona kuna *need* ya kufanya hivyo *spirit* ya *negotiation* itaendelea kutumika haizuiwi kwa sababu ni *concept* ya *negotiation* hapo, kwa hiyo, mazungumzo yanaweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ikifikia mahali kama ulivyosema tuna *clause* ya jumla lakini ku-*import* hapa *spirit* ya mahusiano mema hatutaki kuonyesha kwamba sisi tunakwenda na wawekezaji wetu kwa mashaka na kwa mazingira ya uhasama. Kwa hiyo, tunachotarajia ni kwamba kifungu hiki kimewekwa kikitajarajia kwamba tutaelewa na wataelewa *spirit* hiyo.

**MHE. JOHN M.CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ya kwanza ilivyokuja na Sheria ilikuwa *very clear* kuwa Waziri ata-*prescribe*, kwa hiyo, kama wewe unakuwa *offended* angalau uwe *in defence*. Sasa hivi kwa kuleta hii kuwa mtakwenda *negotiate*, kusema kweli ni sawa na kwamba mmefuta hiyo fursa ya kuwa na *free carried interest* kwa ujanja ujanja tu wa maneno. Naona tungerudi kuwa *whoever* ambaye ni *Authority* a-*prescribe*, sasa kama yule yuko *offended* ndiyo anaweza kwenda *through an arbitration of some description* lakini kwamba unaiacha *empty ended* hivi sioni kuwa tutapata *free carried interest*, na ujue ujeuri wa watu ambao una-*deal* nao siyo kwamba tunaanza tuna uzoefu.

**MWENYEKITI:** Ulichokuwa unataka Mheshimiwa John Cheyo ni kwamba masharti haya yawahusu wote, ndiyo hivyo. Kwa maana nyingine kwa kiwango kile Sheria hii itatofautiana na mikataba iliyopo, Sheria hii inatawala.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Cheyo kwa sababu yeye anasisitiza kwamba pengine tu-*prescribe* kiwango ambacho Serikali inaweza ku-*negotiate* lakini Serikali imetafakari sana hili katika kila mgodi mazingira hayatofanana. Lakini pia kwa nyakati tofauti uwezo wa Serikali kwas ababu haiishii tu kwenye *free carried interest*, tutakwenda zaidi ya hapo, sasa kwenye *free carried interest* tunaamini kwamba kuna mazingira ambayo

tunakuwa tuna–*negotiate* wakati mwekezaji naye ana *negotiate* vitu vingine, kwa sababu sisi tuna *negotiate free carried interest* na yeye kuna vitu vingine ana-*negotiate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ambayo yeye hatataka kukubaliana na sisi hatataka kuielewa *spirit* kwamba hapa kuna dhamira ya Serikali ya kutaka kushiriki lakini utaratibu wake umezungumzwa kwa njia njema. Kwa vyovyote vile mwekezaji aliye *serious* atalielewa hilo kwamba ni kwa kikwazo kwa upande wake katika kupata vitu vingine ambavyo ni *integrity* kwa njia ya mazungumzo. Kwa hiyo tunaamini kwamba hili litafanya kazi vizuri kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatutaki ipelekwe *message*, kama unavyosema ya ku-*impose* kwa sababu hapa tunavyosema huyu ni mwekezaji na tuna mtegemea na sisi tuna rasilimali zetu. Tunaamini katika *spirit* hii tutaweza kufikia *compromise* nzuri.

**MWENYEKITI:** Hebu atusaidie Mheshimiwa Andrew Chenge kwa sababu ninachokiona hapa anachodai Mheshimiwa John Cheyo kinakwenda zaidi ya hapo. Kinataka zile *regulations* utakazotunga Mheshimiwa Waziri yaani kanuni utakazotunga chini ya Sheria hii mpya ziwe na uhalali unaofuta *regime* yote iliyopo *is that right John* nilikuelewa hivyo, ingawa sasa unasimama mara ya tatu.

**MHE. JOHN M.CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *just for clarity* maana yake ile ya kwanza walivyoileta was *perfect* ilikuwa ukisoma section 2 ya hiyo *The Minister may by regulations prescribe the level of Government free carried interest* ndiyo inavyosema. Lakini walivyo-*change* sasa wame-*water down to a level which will not give a Government a free carried interest because* sasa ni mahusiano kati ya Waziri, tumeona *already* tuko hapa kwa sababu ya mikataba ambayo ilikuwa siri, ilikuwa ya mahusiano, ilikuwa na makubaliano ndiyo yametu-*land* kwenye *level* ambapo maslahi yetu kutoka kwenye madini hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo dhana, kwa hiyo, tutafute njia ambapo hii *business* ya mahusiano *person to person*, mimi siyo Mwanasheria, lakini nyie Wanasheria mniambie kuwa hii kweli inaweza kuwa uhalali wa kutunga Sheria katika Bunge hili ambalo linategemea mahusiano, maelewano, *is it real possible? I thought Sheria ought to be exact.*

**MWENYEKITI:** Hebu tumpate Mheshimiwa Chenge, nina *value* uzoefu wake kwenye mambo haya.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa sana Ndugu yangu Mheshimiwa John Cheyo, lakini nadhani kitu ambacho Kamati yako lazima ifahamu tumeanzia kwenye kifungu cha 10(1) kuweka msingi wa haki ya Serikali kupata *a free carried interest* kupitia mkataba ambao masharti yake sasa ndiyo lazima yazungumzwe, kifungu kidogo cha pili ndio kinatokana na yale ambayo yamewekwa katika kifungu kidogo cha kwanza, kule tumefanya marekebisho kama utakavyoona katika mstari wa sita pale *schedule of Amendments* inavyotuongoza.



Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *granting to the Government Free carried interest and state participation*. Sasa haya ndiyo wanataka wakazungumze *level* ya *participation* lakini iwapo mazungumzo hayatapatikana kwa sababu kiwango ambacho kitazungumzwa lazima ki- *form part* ya leseni maana yake ni kwamba hatapata leseni huo ndiyo ukweli na ndiyo maana *scheme* iliyopo ni kuhakikisha kwamba pande zote mbili zinapata maridhiano, lakini msingi ni kwamba *free carried interest* ambayo haitalipiwa na Serikali hiyo ni lazima ipatikane, kitu muhimu cha kuchungumza ni *level*, (kiwango) basi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyongeza ukiisoma *sub-section 2* ilivyorekebisha ile *wording* yake inakupa tafsiri ya lazima jambo hilo ingawaje litafanyika kwa mazungumzo. Unaongelea habari ya *free carried interest* mstari wa tatu unasema *shall be negotiated*, mwekezaji kimsingi hana hiyo *flexibility* ya kusema hapana, hiari hiyo ya kukataa haipo kwa sababu hata maneno haya tungetumia *may* tungeweza kumpa hiyo *flexibility* ya kusema *no*, anaweza kukataa lakini sisi tunakwenda kuongea, kukubaliana kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika mazingira fulani kama nilivyosema tuki- *prescribe* pengine angeweza kuwaambia sasa tuweke *minimum* lakini hiyo ina *danger* tukiweka *minimum* sasa, maana yake tunajifunga. Kwa hiyo, kuna *freedom* ndiyo maana tunasema bado iko *clear*, tunaamini kwamba itatusaidia kwa sababu ina-*import concept* ya *mandatory*.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu Mheshimiwa Cheyo hawezi tena kusimama na nina jaribu kumuelewa ili tutengeneze Sheria nzuri wasiwasi wake nadhani ambao nadhani na wengine naona wanakubali kwa kichwa ni kwamba Waheshimiwa Wabunge ukiwaambia Waziri *ata-negotiate* na muwekezaji wana pata sura ile mmejifungia pale *Kempisnki* ndani ya chumba. Ukishakubali palepale unaandika, sasa hilo ndiyo nadhani linaleta tabu haileti sura ya mfumo mzima kwamba *Attorney General*, ama mfumo mzima wa kutunga kama tunavyoandika mikataba, yaani kuna *subjectivity* yaani kuna Waziri anaweza akamtazama huyu, akasema huyu, akasema Australia ni nchi nzuri labda na mimi nitawekeza baadaye. Kwa hiyo hebu twende vizuri, ikawa tofauti na mwekezaji wa Canada na vitu vya namna hiyo, nadhani huo uhuru ndiyo unaweka wasiwasi hapa. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ambacho tunaanza nacho katika *negotiations* kama alivyosema Mzee Mandela wakati yuko bado kisiwani pale ni *bonafide* yaani ku-*negotiate in good faith*. Sasa maana ya kifungu hiki ni kama walivyoeleza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Chenge kwamba kinachotakiwa hapo ni kuweka *level percentage* ya ile *free carried interest* lakini *issue* ya *free carried interest* ni kitu ambacho kipo, sasa ni *level* gani Waziri amesema kwamba kuna hatari ya kuweka *level* kwa sababu migodi hii inatofautiana na kwa hiyo tunasema kwamba kila mgodi unaweza kuwa na ile *percentage* ambayo

haifanani na sioni nafasi ya Waziri kutumia *description* kwenye eneo hili kwa sababu labda tueleze ambayo hayasemwi kwenye Sheria mara nyingi na mniwie radhi kwa wale ambao wanasema kwamba tumekuwa na mikataba mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mikataba ile siyo mibovu kama mnavyofikiria ni mikataba ambayo ilikuwa *negotiated in good faith* lakini hili hapa ni jambo jipya halikuwemo kwenye Sheria ya zamani na ndiyo maana kwenye mikataba ile halipo. Kwa hiyo, nafikiri kwamba mapendekezo yalivyo katika marekebisho ni sahihi nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tukubaliane kwamba tuwaachie hii *issue* ile *level* ya *free carried interest* iwe *negotiated* na *negotiating team* ambayo kwa kweli nina hakika watakuwa ni watu kutoka sekta mbalimbali na siyo Waziri peke yake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sijui kama itasaidia ikiwa kama tunavyofanya kwa Mheshimiwa Waziri wa fedha *exemptions* lazima ziwe *gazetted*. Haya atakayo-*negotiate* Waziri wa Nishati kwa nini tusingeze pale kwenye hiyo hiyo *subsection 2*, kwamba akishamaliza *the negotiated agreement* itakuwa *published in the official gazette*. Ndiyo *transparency* sasa utasema tu mnasikilizana wawili yamekwisha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nimesimama kabla sijaruhusiwa. Labda ku-*gazette* lakini unajua *transparency* siyo utupu, uwazi siyo utupu *transparency*, siyo kwamba ni *nakedness*. Baadhi ya masharti ya mikataba hii yenyewe inasema sasa labda hapo tukisema u-*gazette* sitakuwa na tatizo lakini ku-*gazette* mikataba mzima nafikiri kutakuwa na tatizo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ndiyo hiyo *level* iliyotajwa nilikuwa nina maana.

**MHE. KAMBWE Z. ZITTO :** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuiondoa hoja ya Mheshimiwa Cheyo bado inasimama lakini naona kuwa mazungumzo yanayoendelea ni kama kwamba hii *negotiation* kati ya Waziri na *licence holders*. Mabadiliko yanasema *the Government and licence holders* maana mazungumzo yanayoendelea sasa hivi ni ya Waziri hapana ni *the Government* isije ikaonekana kwamba *spirit* tunampa kibali Waziri kwenda ku-*negotiate* mabadiliko yana sema *negotiated upon between the Government and Mineral Rights holders* lakini bado hoja ya Mheshimiwa Cheyo naomba iendelee kupatiwa majibu.

**MWENYEKITI:** Nilidhani unasaidia lakini, Mheshimiwa Karamagi hebu tuchote uzoefu hapa.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye hili ni kwamba, kwenye Mkataba wote unaweza ukasoma *Minister shall do this, Minister shall do this*. Lakini uzoefu wangu ni kwamba Waziri anakuja karibu na mwisho, huwa panakuwa na *Government negotiating team* ambayo ina-*negotiate* hivi vyote ambayo imechanganya Wizara mbalimbali na *Attorney General Office*, Waziri anakuwa wa mwisho ingawa huyu ndiye ameambiwa ni *authority* halafu baada ya hapo inakwenda katika *cabinet* ndiyo inapitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tunasema Waziri tu for *the sake* kwa sababu ndiyo *responsible for the Ministry*. Lakini kawaida yeye hakai, maana yake hapa wasiwasi wa Wabunge inaweza kuwa kweli kwamba wanafikiri Waziri ndiye atakwenda ku-*negotiate* kwenye chumba *Kempinski*, hapana Waziri anakuwa wa mwisho kabisa kwenye hii *process* yote ya *licence*.

**MWENYEKITI:** Hebu tumsikie Ole ili mjibu kwa pamoja.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo mtaalam sana wa masuala haya ya ku-*negotiate* lakini kwa jinsi ilivyo hapa ni kwamba kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano na kwa niaba Jamhuri basi Waziri anapewa dhamana hiyo. Sasa hili suala la *negotiating team* kama basi ni taratibu maana ukiendelea huku unaweza ukakuta basi pengine ushauri anaoupata ni ile *Mining Advisory Board*, kama basi kuna *role* nafasi ya *Government Negotiating team* kabla ya kwenda kwa Waziri basi itafutiwe utaratibu kama siyo kwenye Sheria basi kwenye kanuni atakazoiweka Waziri ili uwazi uendelee kuwepo na hilo lingine la uwazi alilolizungumza Mheshimiwa Mwenyekiti pale alipokuwa akiweka vizuri hata mimi naliunga mkono kwa hiyo, nilitaka hili lionekane kama siyo hapa basi kwenye kanuni atakazozitunga Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri a-*commit* Serikali katika hilo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Kabwe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tu kwa sababu naona kila Mjumbe wa Kamati yako anazungumza kana kwamba tunampa *power* Waziri. Kama nilivyosema hapo awali ukisoma 10(1) ndiyo inasema *Minister may* wala siyo *shall* kwa sababu jambo hili tumelizungumza sana kwenye Kamati ya Nishati na Madini na hata kuondoa neno Waziri kuliweka *Government was a purpose* ku-*make sure* kwamba tunalinda hilo ili asiwe ni mtu mmoja. Kwa hiyo, unatakiwa sasa kusoma moja ni *Minister may*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbili *the level of free carried interest* kwenye *Amendment* ukurasa wa tatu. *The level of free carried interest and State participation in any mining operations under a special Mining licence shall be negotiated upon between the Government and Mineral rights holder and not between the Minister*, kwa hiyo, tusiondoke hapa, kuna *spirit* inasema Waziri anakwenda ku-sign, naomba hilo liwe *clear* maana yake naona kila mtu anarejea Waziri, Waziri, Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hapa unajua ukiumwa na nyoka hata jani likigusa unaogopa. Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Cheyo inatokana na hofu ambayo hatuwezi kuipuuza haraka haraka, kwa hiyo, nafikiri twende na yote mawili. Ndugu yangu anajaribu kuonyesha kwamba *Government*, Waziri kwa hiyo tukiita *Government*, tukiita *Minister* bado hofu itabaki palepale tu, *the best that we can go with* ni kwenye kanuni wakati wa kutengeneza kanuni tuonyeshe bayana kwamba jambo litatengenezewa mfumo wa kuwa na *a Government negotiating team* ambayo itakuwa ime-take into account inter ministerial salt of setup akiwemo na *Attorney General* na wataalam na vitu vingine kama hivyo ili kutupa *comfort* kwamba jambo hili limesimamiwa vizuri katika *level* ya *negotiation*. ( *Makofi* )

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tukiiweka hivyo itatupa mwelekeo mzuri zaidi na tutakuwa *much more comfortable*.

**MWENYEKITI:** Nadhani, alichotusaidia hapa Waziri Mkuu kinatusogeza karibu ya pale ambapo Bunge zima lingekusudia, kwamba uhuru huu ukiachwa wazi hapa, kwanza *Government* ukiwa na Waziri Mbabe si anasaini tu, Ndiyo! Hivi Waziri akienda kusaini hao wanaolalamika wanakwenda wapi, *No, no, no!* Tumekuwa kwenye Serikali tunajua, unaweza ukasaini kwa niaba ya nchi na ukasema hiyo ndiyo *power* yangu, sasa mpaka ije kuwa mgogoro tayari nchi imekwishapata matatizo. Kwa hiyo, ni kweli kabisa tukiweka kwenye Kanuni kama anavyopendekeza Waziri Mkuu, inamfunga sasa huyo Waziri ingawa bahati mbaya pia anaweza ku-repeal *regulations*, lakini pengine Kamati ya Mheshimiwa Simbachawene hapo itamwona, afadhali hiyo kidogo. ( *Kicheko* )

( *Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake* )

Ibaya ya 11  
Ibara ya 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13  
Ibara ya 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15  
Ibara ya 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17

**MWENYEKITI:** Katibu tumia Kifungu, Ibara inahusu Katiba.

Kifungu cha 17

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu cha 18 kinazuia watu kuwa na madini *basically*, lakini utakumbuka katika historia tulikuwa na hiyo baadaye kwa ajili ya kurahisisha wachimbaji wadogo kwenda kuuza almasi zao na *industrial minerals*, hii *regulations* ilikuwa imekuwa-*relax*, lakini sheria hii sasa

inarudisha kwa ujumla hata bila kusema ni *mineral* gani, na kama ninavyoona hii *minerals* inaweza ikawa hata mchanga kufuatana na ile *broad definition* ya *minerals*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye hiyo *section* ukifika (4) ina-*prescribe* mpaka adhabu ambayo ni shilingi milioni kumi, *in the case of not exceeding ten million* kwa kuwa umekamatwa na kipande kimoja cha *diamond*, inawezekana labda cha mchanga, halafu *to imprisonment*, mbona watu wetu wote wataishia jela kwa kifungu hiki. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Wazungu wa zamani wali-*prescribe* ni *mineral* gani ambayo inakuwa na masharti makubwa kama haya, lakini *mineral* yoyote ile? Kweli hii dhana inawasaidia wachimbaji wadogo wadogo au ndiyo inawamaliza?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti pia naendelea kumshukuru Mheshimiwa Cheyo kwa sababu tulikuwa naye katika hatua mbalimbali hasa ya matayarisho ya mwisho ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa anachokisema Mheshimiwa Cheyo lakini ukweli ni kwamba anachokisema kiuhalisia kinaweza kutuletea matatizo, kwa sababu sisi tumejifunza sheria hii inakuja sasa kurekebisha kasoro ambazo tumezibaini. Tumesema haiwezekani ukawa na kitu ambacho hakina tafsiri ya madini huku kwenye *interpretation clause* halafu ikaangukia kwenye adhabu ambazo zinatajwa hapa haiwezekani. Uzoefu kama anavyosema kwamba pengine wachimbaji wadogo wataishia magerezani nadhani ni kauli ya kutisha sana lakini si hivyo, kwa sababu pia wachimbaji wadogo wamekuwa wakiuza madini yao kwa *centres* ambazo zimekuwa na wanunuzi, hatutarajii tu kwamba mtu atembeee na madini bila kuwepo na sababu yoyote haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili ni kwamba hii imelengwa kuzuia madini ambayo yanapita pembeni na tunadhani kwamba mojawapo ya hatua za kuzuia hilo ni pamoja na kuweka kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu adhabu kwamba ni kubwa sana, ndiyo maana tumesema isizidi milioni kumi, kwa hivyo inawezekana kwa anayeamua ikawa chini ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuliweka sawa tu hili kwamba limezingatia uzoefu, lakini pia lina nia ya kuzuia upitishaji wa madini njia za panya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Jamani, nadhani ni kweli, tukijenga kwenye sheria dhana ambayo ni haki ya kiraia ya kila Mtanzania kuwa na *diamond* wakati wowote na

asikamatwe, kwa sababu ukiwa na nia njema utafuata taratibu za ku-*acquire* hiyo *mineral*. Sasa tukitetea hali ambayo inaacha uhuru huo unakuwa uhuru kamili, naona kuna hatari ya ujambazi kuongezeka, maana yake ukiwa na *diamond* unasema unaniuliza nini kwa sababu naruhusiwa na sheria kuwa na *diamond*. Sasa hii ni sawa kweli?

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili tunaongelea kwa mfano, zile sehemu za Chunya ambapo ikinyesha mvua wale wananchi wakiamka nje ya nyumba zao wanakuta vipande vya dhahabu. Sasa katika hali hii tunawaweka katika *situation* gani maana wakipatikana na vipande vya dhahabu tayari watalipa milioni kumi kwa sababu hawana leseni.

**MWENYEKITI:** Lah! Ninyi mna bahati kweli dhahabu inaelea tu kila mahali. (*Kicheko*)

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Sina matatizo ikibaki hivi, isipokuwa ningependa kupata uhakiki kutoka kwa Waziri wakati wa kutengeneza Kanuni aweze kuiweka sawa ili kusudi kumlinda mtu ambaye kwa bahati ametokea kuwa ana madini kwa mfano; natoka eneo ambalo mgodi wa kwanza wa almasi ndiyo John Williamson alianzia huko Kizumbi na bado almasi hiyo ipo. Wakati mwingine mtu anapokuwa shambani kwakwe si ajabu kuokota kipande cha almasi, kwa mfano, wakati wa ujenzi wa barabara ya lami hii ya sasa hivi maeneo ya Shinyanga Kizumbi, Mwendesha Katapila mmoja aliokota kipande kikubwa sana cha almasi na alipoiuza alipata milioni moja. Sasa kwa sheria hii kile kitendo cha kuamua kwenda kuiuza anaweza akajikuta yuko tayari kifungoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilipenda tu kwa *nature* ya maeneo, mtu akibahatika kuwa na madini, hatua ya kwenda kuyauza asihesabiwe kuwa ametenda kosa la kuwa na madini, sheria itamlinda namna gani katika maana ya kanuni? Kwa hiyo, ningependa kwenye Kanuni hilo liwekwe sawa ili kusudi kuwalinda wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hebu tusaidie kwenye hilo tu, mtu anabahatika anachimba choo pale Shinyanga badala yake anakuta dhahabu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema Waheshimiwa Madaktari hawa wana jambo linalofanana. Sina hakika sana na Chunya Mheshimiwa Mwambalaswa angekuwepo angetusaidia, lakini zinaponyesha mvua siyo matukio ya kila wakati, vinginevyo kama unavyofahamu *rash* zingiongezeka kule, lakini naelewa hoja ya Mheshimiwa Siyame.

Mheshimiwa Mwenyekiti kama unavyofahamu kutunga sheria ambayo ni *very perfect*, ikaziba kila kitu, si jambo ambalo ni *practical*, lakini sisi tunaweka mizania, ni mara ngapi matukio ya namna hiyo, lile la mchanga lililohojiwa na Mheshimiwa Cheyo

limeelezewa kwenye kifungu kidogo cha pili ambalo ni mchanga na mambo ya chumvi. Lakini hili suala la mtu ameokota kipande chake tunadhani katika hali ya kawaida kama ni kuuza na anataka kuuza kwa namna ambayo watu wasimwelewe vibaya na mkono wa Serikali usigundue hilo, apitie kwa wale wenye vibali. Kwa sababu ni kitu ambacho ni *practical* ili ku-cover ajizuie na dhahama hii ambayo inaweza kumwangukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akipitia hawa wenye leseni au vibali inawezekana, lakini katika mazingira hayo ya kawaida si rahisi ku-*reflect* jambo kama hilo kwenye sheria kwamba tuseme itokee mtu bahati mbaya uta-*test* vipi kwamba uthibitisho wake kwamba huyu aliokota katika mazingira ambayo hakuwa mchimbaji, ilikuwa kwenye eneo lake, itatuongezea ugumu sana katika kusimamia na ndiyo maana tunasema hizo *avenues* labda zitumike kupitia kwa watu wengine ambao wanakuwa na vibali.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunapozungumza Dar es Salaam, kuna matapeli wakubwa sana wa madini, kuna watu ambao wanakuja kutoka nchi mbalimbali na hasa kutoka Russia na wananunua madini kinyume cha taratibu na wanapigwa kweli, wanaibiwa kweli, kwa hiyo kipengele hiki cha sheria napingana kabisa na Mheshimiwa Cheyo, kipengele hiki kinadhibiti ufahamu wa madini ambayo yameuzwa na kinadhibiti watu ambao wanafanya utapeli wa madini ambao sasa hivi umeshamiri sana Dar es Salaam, watu wanaibiwa mpaka milioni mia nane na kadhalika. Jambo ambalo tunapaswa kuliweka, kwanza kama viongozi ni lazima tukubali kwamba kuna baadhi ya maamuzi ambayo tunayafanya lazima yawe magumu ili watu wetu wafuate taratibu wasiwe *informal*, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili hii sheria inaishusha sasa ofisi ya Kamishna kutoka Dar es Salaam mpaka chini kunakuwa na *zonal*, kwa hiyo sisi Waheshimiwa Wabunge tuwashauri watu wetu kama anachimba choo akakutana na *diamond*, kama mvua imenyeshwa akakutana na dhahabu aende haraka kuripoti kwa *Zonal Commissioner* wa *levy*, au aende akaiuze kwa *license dealer*, kwa sababu akiuza kwa *license dealer* ndiyo sisi tunapata *royalty*, akiuza kimya kimya hatupati *royalty* ndiyo maana hasa ya hiki kipengele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kama ulivyosema hiki kipengele ni sawa na kinaondoa woga wa Mheshimiwa Cheyo kwa mambo ya *building materials* na chumvi kwa sababu *section* ya pili inakifuta, kwa hiyo, Bunge likipitishhe.

**MWENYEKITI:** Tumsikilize Mheshimiwa Cheyo kwanza maana yake ndiye aliyeanzisha hii hoja.



**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yote yale ambayo Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Zitto wameyazungumza nakubaliana nayo, tatizo la hapa in *possession*, umeipata, kwa kuwa umeshaipata *should not be unlawful, this is what I am saying*, hiyo ndiyo *worry* yangu tu. Mimi siyo mwanasheria lakini mnaweza mkatafuta wanasheria, kama unafanya biashara kimagendo na kadhalika, hiyo nakubali sheria lazima ichukue mkondo wake, lakini tunaishi katika mazingira ambayo ni halisi. Nenda leo Maganzo, utakuta watu lukuki wamechimba pale wana almasi na yeye anajua kwamba wachimbaji wadogo wadogo ambayo wamepewa *license* ni wangapi? Ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti tukienda kwa utaratibu huu Kishapu yote ile mtafunga watu wengi, ndiyo hali halisi. Kwa hiyo in *possession*, ule utaratibu wa kuuza sina tatizo nao, *you in possession*, ufanye nini sijui ufungwe?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hatuwezi kuwa wote Mahakimu na Majaji, utaratibu ni kwamba huyu mtu akikamatwa na hiyo, kama atakuwa amesema kwamba ameokota na Hakimu anajua kwamba sehemu za Maganzo watu wanaokota, atakachofanya sasa ni kwamba ataambiwa aende kuuza kwa utaratibu wa sheria, lakini huwezi kutunga ukaweka *exception* kwamba anaruhusiwa kwa sababu hii sheria sasa haitatekelezeka. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Zitto na nampongeza sana kwa hilo kwamba, hiyo ndiyo njia pekee ambayo itakufanya wewe upate mrahaba. Tunajua kwamba ni vizuri kuwatetea wananchi wetu, lakini ni vizuri kuwatetea wafuate sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba Mahakimu siyo vipofu na Majaji siyo vipofu, kama ataweka *defence* kwamba mimi hii nimeiokota, si utaangalia mazingira ya sehemu ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba, tuendeleo na *concept* ambayo Mheshimiwa Zitto ameiiweka.

**MWENYEKITI:** Nimalize orodha yangu ya wachangiaji, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikubaliane tu kwamba tunahitaji katika nchi watu waingie kwenye *formal sector* na katika eneo ambalo lilivurugika sana moja ni hili la madini, lakini vilevile tukubali kwamba katika nchi yetu si chini ya mikoa kumi na tisa ina madini ya aina mbalimbali yamesambaa na katika madini hayo yapo ya aina mbili, yapo *alluvia*, ambayo kuna *alluvial diamond, alluvial gold*, unaikuta inasambaa kwenye maji tu, na hata hawa

wachimbaji wakubwa walivyokuja watu wetu walizigundua hizo ndiyo wao wakaona hapa vile vile inawezekana kuna mwamba wenye madini chini. Lakini ukienda huko kwa shemeji zangu Mbeya ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kabisa kwamba ni kweli haya tunayoyasema, unajenga ofisi unakuta *Gold*, mita moja ama nusu mita unakuta *gold*, ama mita mbili unakuta *diamond*, sasa hao wanaookota na kwa sababu sasa hivi elimu imekuwa kubwa, watu wanajua *diamond* ni nini siyo kama zamani, anaichukua anajua hii ni almasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachokosekana hapa ni *structure* ya kumhakikishia yule aliyepata anakwenda kuipeleka wapi ili awe salama, hili nafikiri ndiyo jambo la kuliangalia vile vile. Nakubaliana kabisa kwamba tunahitaji ku-*formalise* biashara yetu iende vizuri lakini tusingahau kwamba maeneo mengi ya Tanzania yana dhahabu aina ya *alluvial*, kuna *diamond* aina *alluvial* ambayo watu wanaweza kuokota kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni vizuri katika kanuni za Waziri, kwanza ile *structure* niliyoizungunza jana ni muhimu sana, kuhakikisha kwamba kuna masoko huko chini, kwa hivyo *licensing authority* lazima Waziri aiweke *clear* na iwe inajulikana, inapatikana. Lakini ni wakati gani mtu mzima mwenye miaka 60, miaka 70 anaipata anapookota kitu chake, halafu tutegemee atakwenda mahakamani na mahakama tu kwa busara imwambie kwamba inamwachia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili ni tatizo, inatakiwa kufafanuliwa katika Kanuni za Waziri hapa, aweke kwamba *immediately* ukiipata hicho kitu basi kuwe na *timeframe* ya kumhakikishia kwamba anaki-*dispose* kwenye *authority* inayotakiwa akichelewa katika kipindi hicho nafikiri ndiyo hatua ichukuliwe, vinginevyo anavyosema Mheshimiwa Cheyo i nina uzoefu, nimeshazunguka sana huko miaka mingi tu, ni kweli watu wetu wengi sana wanazipata almasi na dhahabu katika misingi hiyo, sasa tusipokuwa makini katika kutengeneza sheria ni kweli. Lakini nakubaliana na alichokisema Mheshimiwa Zitto vile vile, kwamba utapeli umekuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri hii sheria ikahakikisha kabisa inadhibiti hayo maeneo, kwa hiyo, nafikiri katika kanuni za Waziri ambazo atatengeneza aeleze tu kwamba *immediately* akipata hiyo basi watu wa kuwatafuta kwa kuwauzia ni hawa. Nafikiri elimu hii ikitolewa kwa wingi halafu hii sheria inaweza kuchukua mkondo wake kama kawaida. Ahsante sana.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwakumbusha wenzangu na Bunge lako Tukufu kwamba huko nyuma tulikuwa na tatizo hili kwenye eneo la fedha za kigeni. Huko nyuma ilikuwa ukikutwa na dola mfukoni ni tatizo kubwa sana, leo hii humu ndani tukiangaliwa kwenye pochi zetu tuko wengi tu tuna dola mia moja, dola hamsini na vitu kama hivyo. Dhahabu ni *equivalent to foreign exchange*, tumekwishafungua maduka ya dola, tunakwenda kuuza dola pale unapotaka, unaangalia *exchange rate* ikoje, ikikupendeza unakwenda siku hiyo kubadilisha.

Sasa huyu mwenye dhahabu ambaye atakuwa amepata kwa njia yake na yeye aruhusiwe kuiuza kwa yule *authorized dealer* pale ambapo anaona bei inafaa wala sio kosa. Tukilifanya hili sio kosa, tukilifanya hili kosa, basi na wale wanao-*hold foreign expense* mfukoni mwao na wao vile vile ni kosa.

**MWENYEKITI:** Bado haijasaidia sana.

**MHE. JAMES LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuelezea tu wasiwasi wangu kama wenzangu walivyosema. Kuna baadhi ya maeneo hapa nchini ambako madini kama dhahabu Kahama kwa mfano, zinapatikana nje nje na inatokea huyu anayeokota anakaa kilomita 120, 160 kutoka pale ilipo Ofisi ya Madini. Utapeli ni mwingi siku hizi, watu wakishagundua kuwa yule ana dhahabu, wakimchongea kwa Mtendaji ni kesi kubwa. Sasa katika mazingira haya bila kuwa-*protect* hawa wananchi ambao ni *innocent* amejikuta tu amekutana na bahati halafu kesho anajikuta anaambiwa alipe shilingi milioni 10 au afungwe, sidhani kama sheria tunazozitunga ni kwa ajili ya kuwakomoa wananchi wetu maskini. Hapa napenda nipingane kabisa na Mheshimiwa Zitto. Anaowazungumzia ni matapeli walioko kule Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lembeli, siyo unapingana na Mheshimiwa Zitto.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wanaotengeneza dhahabu *fake* wa Dar es Salaam, sisi tunaowazungumzia hapa ni wananchi wa kawaida walioko kule Kahama, Chunya, Maganzo, Shinyanga tutafute namna ya kuwahakikishia hawa wananchi kwamba sheria hii haitakuwa inawakandamiza. Nashukuru.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kaboyonga ametoa *reference ya liberalization* ya dola, kinachoua uchumi wetu sasa hivi ni hiyo *liberazation*. Ukienda nchi nyingine leo hununui dola kama unavyonunua Tanzania. Hatuwezi kurudi nyuma kuendelea kui- *re-enact* ile sheria. Lakini *what is cleaning our economy* kwenye *currency* kwenye *Forex* ni *liberalization* ya dola. Kwa hiyo, hatuwezi kuruhusu makosa ambayo tumeyafanya kwenye *liberalization* ya dola tukiirejea kwenye dhahabu. Tunachozungumzia hapa ni mali za nchi ambazo hatuwezi tu kuachia watu tu wakauziana uziana tusipate *royalty* inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana Mheshimiwa Lembeli hakuwepo kwenye Kamati ya Nishati na Madini na kwake kuna mgodi, nilishangaa sana kwa nini hakuwepo kwenye Kamati ya Nishati na Madini wakati tunajadili kitu kama hiki. Suala kama hili tumelijadili kwa undani na kuweza kuona jinsi ya gani ya kuweka *water tight* kuhakikisha kwamba rasilimali zetu tunaweza tukazilinda vizuri. Nakubaliana kabisa kwamba lazima tuangalie kwenye kanuni jinsi gani wananchi wetu wa kawaida kabisa

kule chini ambako hamna *structure* jinsi gani ambavyo wanaweza kufaidika. Lakini tukiacha sheria wazi, tunakuwa tunakwenda kuwalinda matapeli wa Dar es Salaam ambao kila siku wanaharibu sifa ya nchi kwa kuwapiga watu kwa utapeli wa dhahabu.

**MWENYEKITI:** Mimi jamani nashauri tufuate mwongozo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye vitu kama hivi kwa sababu kwenye kanuni ukitaka kulichukulia jambo hilo ni jipesi zaidi kumlinda mwananchi ambaye sio tapeli, si basi tu amepata bahati tumwachie Waziri kwenye kanuni aliweke vizuri. Hapa tusibadili chochote. Lakini kwenye kanuni liwepo. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali imesikia na itaifanyia kazi kwenye kanuni. (*Makofi*)

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19(4) na hasa ukiangalia pale kwenye *part three - administration* kwenye *sub section (4)* kuna neno: “*the commissioner may by notice in the gazette designate any person to be any authorised officer for the purpose of all or any of the provision of this act.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia sasa huyu anayezungumza kama *authorised officer*, ukienda kwenye *definition* yake kwenye ukurasa wa nane utakuta kwamba *any authorised officer means, The Commission, the Chief Inspector* halafu pale inaendelea, *Public Officer appointed under sub section 19 or a personal designated as such by the Commissioner under sub section (4) of section 19*. Kwa sababu ukiangalia hapa jukumu baadaye utakalolikuta la huyu *authorised officer* huko kwenye kifungu cha 101 utakuta kuna chombo muhimu ambacho kilipaswa ki-*appear* katika *column* hii.

Chombo chenyewe ninachojaribu kuzungumzia hapa, mtakumbuka tuliunda *Tanzania Minerals Audit Agency*. Sasa hii *TMAA* role yake ilikuwa ni kwa mujibu *GN 362* inasema: *is to maximise the government revenue from the mining industry*, halafu ikaendelea *through effective monitoring and auditing of mining operation*, ikaendelea. Nikaamua tu kukuonyesha hilo ili kukuonyesha umuhimu wa *agency* hii ya *TMAA* na kwamba hawa wa *TMAA* hawatamkwi kama *authorising officers*. Kwa hiyo, hata katika kifungu hicho baadaye utakakikuta cha 101 hawatakuwa na mamlaka ya kuingia katika migodi ile kutimiza wajibu wao wa kuundwa kwao ili kuweza kufanya ukaguzi wa *monitoring* kwa ujumla kujua yale madini yanayozalishwa katika migodi mikubwa ni kiasi gani na thamani yake ni nini ili kuweza kuifikisha Serikali mahali pa kujua kama imepata kodi yake inayostahili.

Sasa swali langu ni kwamba, kwa maana hii ambapo Kamishina anapewa nafasi ya kumteua huyo *authorised officer*: Je, ni wapi ambapo mamlaka hii muhimu sana? Hii

*agency* itakapopata fursa ya kuwa na hadhi hii ya *authorising officer* ili waweze kuingia katika migodi hiyo isiwe ni Kamishna peke yake na mtu mmoja aliyeteua anayepata fursa ya kuingia huko. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Christopher Olle-Sendeka ambaye kama Waheshimiwa Wajumbe wengine wa Kamati yako niliowataja, tumekuwa naye kwenye mchakato huu mzima na bahati nzuri yeye ni Mjumbe wa Kamati. Tumeliongea sana hili, lakini ufupi ni kwamba kwa nini Wakala wa Ukaguzi kwa migodi haujitokezi hapa? Ni sababu moja kubwa, kwamba Wakala ule mwanzoni ulikuwa unaitwa *Gold Audit Program* kama kiwe kitengo cha ukaguzi chini ya Kamishna wa Madini walivyorithi kazi zilizokuwa zinafanywa na *Alex Stewarts* mwaka 2007. Kilichotokea ni kwamba, hapo katikati *Alex Stewarts* alikuwa anaondoka na hatukujua nani anachukua majukumu haya.

Kwa hiyo, Serikali ikachukua uamuzi wa kuwatumia watalaam wetu wa Wizara ya Nishati hasa *Commission* ya Madini, lakini kwa ujumla iliwachukua wafanyakazi waliokuwa kampuni ya *Alex Stewarts* wale wa Kitanzania ikawa sehemu ya kitengo chetu, wakaanza kufanya kazi zile ambazo kampuni ya *Alex Stewarts* ilikuwa inafanya ambazo zilikuwa za ukaguzi wa uwekezaji katika migodi. Sasa tumekwenda hivyo na hatimaye mwaka jana ikaanzishwa *agency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo moja ambalo Serikali imetafakari na ndiyo kilichosababisha tusiliweke hapa. Kwa hiyo, kazi zile ambazo zilikuwa zinafanywa na *Alex Stewarts* kimsingi zile kazi hazikuwa na mahusiano ya moja kwa moja. *Reporting authority* yake haikuwa ndani ya Wizara ya Nishati na Madini, ilikuwa kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi hasa Benki Kuu na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Sasa kwa hatua hii tuliyonayo sasa, Serikali inatafakari tuangalie pamoja na Benki Kuu ya Tanzania ama iwe kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa hiyo, ndiyo sababu iliyotufanya tusiiweke hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo tumeliongea kwa kiasi kikubwa sana Serikalini na tunatambua kazi zinazofanywa ni kazi za manufaa kwa Taifa. Kwa hiyo, siyo kwamba kwa sababu hayajitokezi hapa kwa namna yoyote ile labda Serikali haichukulii kwa uzito unaostahili, hapana. Ni jambo ambalo tunatafakari na kwa sababu *Agency* inaanzishwa kwa Sheria nyingine ile, "*The Executive Agencies Act*," bado tunasema iko fursa na tunaomba Kamati yako ituruhusu tuendeleo kutafakari vizuri ili tuangalie kama ni *TRA* ama ni Benki Kuu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nazungumzia katika sehemu hii ya *administration* ambako Kamishna anapewa fursa ya kumteua huyu *authorised officer*, sasa kama wote tunakubali juu ya umuhimu wa kuwa na Wakala huyu na kazi nzuri iliyofanywa na Wakala huyu na kimsingi kazi iliyofanywa kwa mujibu wa taarifa iliyokuwa imeletwa kwenye Kamati yetu ya Nishati na Madini, ni kazi nzuri sana, ni kazi ambayo imeweza kutusaidia kujua uhalisia wa mambo yanayoendelea pale. Sasa kama Wakala huyu hatapata uhalali katika sheria hii na kwamba majukumu haya yanakabidhiwa kwa Kamishna, utakapokwenda kwenye

kifungu cha 101 huko mbele na huyo *Authorised Officer*, huoni kwamba tunapunguza uwezo wa Serikali wa jicho kuweza kujua nini kinachoendelea katika migodi mbalimbali na ukizingatia kwamba migodi hii mikubwa sasa inaongezeka idadi yake na huku kuna kazi kubwa inayofanyika, na kwamba kwa nini tuna-*limit* kuwaweka watu wachache waende huko badala ya wakala huyu kuendelea kutufanyia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa nini nisikumbushe Serikali dhumuni la kuanzishwa kwa *TMAA* waijue vizuri. *The aim of TMAA is to maximize government revenue from the Mining Industry through effective monitoring and auditing of mining operations and insuring sound environmental management. TMAA is a successor of the mineral auditing section under the Ministry of Energy and Minerals which was responsible for undertaking gold auditing of the major gold mines in the country.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kama jukumu lote hili zito la ndani na nje huko ukiendelea baadaye kuangalia madhumuni yake kama ilivyo kwenye *GNE* utakuta umuhimu wa wakala huyu kuwepo ni mkubwa.

**MWENYEKITI:** Dakika tatu zimekwisha. Maelezo ni dakika tatu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anamjibu Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka amezungumza kwamba *TMAA* haiwezi kuwekwa hapa kwa sababu inaundwa na sheria nyingine. Lakini ndani ya sheria hii tumeiweka ile *Geological Survey Agency* ambayo nayo pia imeundwa kwa sheria nyingine. Ndani ya sheria hii tumeiweka *TRA* ambayo nayo pia umeundwa kwa sheria nyingine. Hakuna sababu yoyote ya msingi ya kutokuweka *TMAA* kwa sababu hiki ndiyo chombo ambacho kinahakikisha wawekezaji mitaji ambayo wanaweka, dhahabu au *Tanzanite* au chochote kile ambacho wanakichimba kinaweza kikawa na *transparent*. Hiki ndio chombo ambacho tumekiunda na *initiative* yao wenyewe Serikali wanamzaa mtoto halafu wanataka kumuua, wanataka kumnyima kazi za kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu yoyote ile ambayo Serikali inaweza ikaitoa kutokuweka *TMAA* hapa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kama sehemu ya *Authorising Officer*, naungana kabisa na Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba Wakala huyu ambaye tumemuweka kwa ajili ya ku-*Maximize Government Revenue* awekwe. Kwa nini huyu tu atoke? *Geological Survey* yupo kwa sababu anaonyesha kwamba kuna maeneo, *TRA* yupo. Lakini mtu ambaye anamwambia *TRA* kwamba huyu mwekezaji amedanganya au hajadanganya anaondolewa. Kuna kitu gani? Kuna *bad faith* hapa. Nilikuwa naomba kwamba Waziri akubali *TMAA* iwekwe kwenye mazingira yote ambayo yanatakiwa kuwepo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka pamoja na Mheshimiwa Kabwe Zitto. Kwanza hakuna sababu yoyote ya kwa nini sijui ikafiriwa kwamba *TMAA* hapa haonekani. Kama tulivyoeleza kwamba Serikali ilikuwa inatafakari kwa sababu jambo hili kiserikali tumeliongea sana tumezungumza sana. Mheshimiwa Kabwe Zitto amekwenda hatua mbele kidogo kwa sababu Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka

alikuwa anachoongea ni hawa *Authorised Officer*. Ukisoma kwenye *interpretation clause*, waliopo kule *Authorised Officer* ni wale wafanyakazi chini ya *Commissioner* wa Madini, wapo wengi ambao wanaweza kufanya shughuli. Lakini kwa hili ambalo linahusu *TMAA* nasema hakuna ubaya wowote kuwepo hapa. Lakini Serikali ilichokuwa inasema ni kuomba muda kwa sababu mchakato huu kwa nini unaendelea? Tulikuwa tunasema mtupe muda huo tuendele kutafakari, lakini sio kusema kwamba jambo hili haliwezi kuingia hapa, hatujasema hivyo. Serikali iko tayari kuliweka hapa.

**MWENYEKITI:** Kama Mheshimiwa Waziri anaweza kuteua Mtanzania yeyote wala siyo Mtanzania pengine *any person*, hivi *TMAA* ikiingia hapa kuna taabu gani jamani kuwa na *rights of inspection*?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubali kwamba tutafanya *reference* kwa *TMAA*.

**MWENYEKITI:** Tumsikilize Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuliona hili. Tunaweza tukalifanya vizuri na kwa ufanisi zaidi kwa waandishi wa Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kurudi kwenye kifungu cha nne ambacho kinahusiana na *definition of authorised officer* na ndiyo kule tukaingiza dhana nzima ya Wakala huu muhimu kwa shughuli hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *authorised officer*, utaona *means*, “*The Commissioner, Chief inspector, Inspector or a public officer appointed under section 19 or a personal designated as such by the commissioner,*” under sub section (4) of section 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Kamati yako ingelikubali sasa maelekezo kwa Serikali *agency* hii ikaingizwe kwenye sehemu ya *definition* ya *authorised officer*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nadhani hiyo inatuondolea tatizo lote kwa sababu anakuwa ni mmojawapo wa wale wanaoruhusiwa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuogopa tena kusema kwamba kifungu hicho kimeingizwa kinyemela, naomba tuifanye hiyo kazi sasa hivi.

Kwa msingi kwamba *authorised officer* kama ilivyo *means the Commissioner, Chief Inspector, Inspector or a public officer appointed under section 19 or a personal designated as such by the commissioner under sub section (4) of section 19 including Tanzania Mineral Audit Authority*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hapana, haikukaa vizuri hiyo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Nadhani atajwe kabla ya huyo *any other person* kwenye *or*, kwa sababu huwezi kusema huyo naye ni *designated* ile *TMAA* haiwezi kuwa ni *designated*. Kwa hiyo, itangulie huku. Ukifika pale *Inspector or TMAA*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 20

Kifungu cha 21

Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 24

Kifungu cha 25

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni tulizungumzia suala la kifungu cha 25 ambacho Waziri ametolea maelezo ambayo sisi tunadhani kwamba hatujaweza kuridhika nayo. Kwa sababu kifungu cha 25 kinazuia *information*, ndiyo kifungu ambacho kinatengeneza ile *secrecy* kwamba Mikataba ni siri kati ya Serikali na mwekezaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika mchango wetu kwamba tayari Serikali yetu imeshajiunga na *Exceptive Industry Transparency Initiative*, kwa hiyo, tulishauri mawasilisho ya Kambi ya Upinzani na tunarejea kushauri hapa katika vifungu kwamba kifungu cha 25 kifanyiwe marekebisho kwa ajili ya kuhakikisha kwamba taarifa ambazo zitatakiwa kwa ajili ya *exceptive Industry Transparency Initiative* zisibanwe na kifungu hiki kwa sababu ndiyo taarifa ambazo zitatufanya tufahamu ni kiasi gani ambacho makampuni yamelipa Serikali na ni kiasi gani ambacho imepokea kutoka kwa makampuni na kuondoa hili wingu la kuwa na wasiwasi wa kutokujua ni *revenue* kiasi gani ambalo Taifa letu linapata kutokana na sekta ya madini.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba katika hiki kifungu cha 25 itafutwe njia ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatusaidia hapa kwa ajili ya *reference* ya *information* itakayotakiwa kwa ajili ya *ITI* isikataliwe kutolewa kwa sababu jinsi kilivyo hapa hatutaweza kupata *information* kwa kuweza kujua kwamba ni mapato gani ambayo nchi inapata.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tulichosema na Mheshimiwa Zitto anajua, tumeongea sana kwenye Kamati ingawa kama alivyosema ni kati ya mambo ambayo pengine hatukufikia muafaka mzuri. Lakini tulisema kwanza suala lenyewe la *ITI*, hii tasnia ya uzinduaji, tumesema kwanza itatungiwa sheria yake ambapo moja nyingine tunaamini kwamba itatuwekea pia utaratibu wa namna ya kupata hizo *information* kupitia huo utaratibu. Lakini la pili tukasema kwa mazingira ya sasa tuliyonayo, kwa mfano kama mtu anataka labda taarifa kuhusu mkataba fulani, Bunge lako Tukufu hili lina utaratibu sasa hivi na Serikali mtu kama atahitaji taarifa fulani hilo tumeshasema utaratibu upo.

Lakini pili tukasema kwa huko mbele tunakokwenda, taarifa za mikataba ambayo ndio itakuwa inaingiwa, tutakuwa tunatoa baadhi ya taarifa hasa zile za msingi kwa Halmashauri katika maeneo ambayo migodi itakuwa imejengwa. Sasa sisi tukaamini kwamba katika hatua hiyo tutakuwa tumepiga hatua fulani katika kuendeleza hii *concept* ama hii dhana ya kuweka mambo wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulidhani kama tulielewana katika hilo ingawa sio kwa kiwango ambacho Mheshimiwa Zitto anakielezea, kwa hivi sisi tulielezea mtazamo wetu ulivyokuwa kwamba sheria hii ya *ITI* itakuja, lakini pia kuna fursa nyingine ambazo sasa hivi mtu anaweza kupata kama anataka taarifa kuhusu jambo fulani na inategemea pia ni taarifa gani kwa sababu nadhani ukienda mbele pale *sub-section* inayofuata imeelezea taarifa zile ambazo zinaweza kupatikana na kwa namna gani. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hatua tuliyokuwanayo haikuwa jambo baya sana kufikia hatua ambayo Mheshimiwa Zitto anasema.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokuwa tunakiomba ni katika ile *sub-section (2)* pale anaposema: “*nothing in sub-section one shall operate to prevent the disclosure of information where the disclosure is meant*”. Kuna zile (a), (b), (c), (d), (e) tuongeze *for the purpose of international obligations that the United Republic has committed to*. Hicho ndio tulikuwa tunakiomba kitokee. Ni *general statement*, lakini kwa watu ambao watakuwa wanataka *information for that purpose* na hapo *automatically ITI* itakuwa imeingia. *Just for the purpose of the international obligation that the United Republic has committed itself to*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni vizuri kuwa waangalifu sana kwenye maeneo haya, kwa sababu mambo haya ni ya biashara ambazo hata hizo *international obligations* wanaotafuta *informations* hizo, wanaweza kukuletea madhara makubwa sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri *disclosure, exceptions* ambazo zimepatikana kwenye *sub-section (2)* zile zinatoshia, kwa sababu hiyo *international obligations* zitapatikana hapo.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Bado hatujatengenezewa kadi, kwa hiyo, inabidi tuazime kadi za jirani zetu hapa. Pamoja na maelezo aliyokuwa ameyatoa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, lakini nilikuwa nadhani

vilevile kwamba hii *point* iliyotolewa na Upande wa Upinzani izingatiwe sana kwa sababu Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu anasema tuwe waangalifu kwa sababu haya ni mambo ya kibiashara, na kwamba inawezekana watu waliokuwa wanatafuta *information* katika haya mambo ya kibiashara wakawa wanatafuta njia za kuwasilina wenyewe kwa wenyewe na pia ikaathiri ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kilichokuwepo hapa ni kwamba na Waziri mwenyewe alitumbia katika Kamati na hata hapa kwamba hii *Extractive Industries Transparency Initiative*, Serikali yenyewe imeshaji-*commit*. Sasa unaji-*commit* kwa kitu ambacho unasema hapa kwamba kinaweza kikatuletea madhara? Kwa nini tuliji-*commit* nacho kwanza? Maelezo hayo yaliyotolewa naona bado hayajatosheleza kujibu hoja hii na nadhani bado tunahitaji kuwa na kifungu na kama tunaona alivyokipendekeza Mheshimiwa Zitto kwamba ni *too general*, basi kiwe *specific*, kiseme: “*International obligations made under Extracted Industry Transparency Initiative*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilimwona Mheshimiwa Zitto ameridhika, kwa hiyo, unayoyaongezea huwezi kuchukua uzito kushinda yeye. Kifungu hicho kinaafikiwa? (*Kicheko*)

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 26  
Kifungu cha 27

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 28

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 29

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30  
Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 32

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 33

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 34

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika lile jedwali la marekebisho. Kuna sehemu moja kwenye *clause* ya 34 kifungu (f), pale wanasema: “*State on the procurement plan,*” pale kwenye neno “*in*”, iwe “*in not on.*” Nilikuwa nanyoosha tu hicho kifungu.

**MWENYEKITI:** Nomba urudie.

**WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema ile “*on*” ingekuwa “*in.*” Yaani, “*in the procurement plan.*” *Not “on the procurement plan.”*

**MWENYEKITI:** Nadhani ni kweli. Ni *typographical* hiyo. *State: “in the plan”, not “on the plan”.* Sawa Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 35

Kifungu cha 36

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 37

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mstari wa mwisho inayosomoka *consultants to the satisfaction of, to the Minister,* nadhani neno *to,* pale limewekwa kwa makosa.

**MWENYEKITI:** Tuelekeze vizuri tafadhali. *Sub-section* ipi?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-section 37*.

**MWENYEKITI:** Ah! Kwenye *amendment*.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *amendment*, yes. Ule mstari wa mwisho unasomeka: “*on the consultants to the satisfaction of to the Minister*”. Kwa hiyo, neno “*to*” pale nadhani limewekwa kwa makosa.

**MWENYEKITI:** Ni kweli, ni *typographical error*. Ah! Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zambi yuko sahihi, lakini marekebisho yaliyoletwa na Serikali ndio yameleta mchanganyiko kidogo. Kwenye Muswada, naomba wote ambao tuna Muswada wenyewe ukurasa wa 32(2) amabcho kinasema: “*an application for a retention license shall be accompanied by studies and assessments by appropriate independent experts or consultants,*” sasa ndio inaendelea kutaja kwa masuala yapi. Sasa hapa, ukiweka maneno yale ambayo yamependekezwa kwenye *schedule of amendments*, ambapo Mheshimiwa Zambi ameingilia, tatizo unaliona pale, “*independent experts or consultants to the satisfaction of the Minister,*” haiendi kwa mtiririko wa Muswada ulivyo.

Tunachotakiwa kusema hapa, marekebisho haya kusudio lake ni kwamba “*an application for retention license shall be accompanied by studies and assessments by appropriate independent experts or consultants acceptable to the Minister on,*” sasa inaendelea kutaja hayo. Lazima hiyo ndio dhana nzima inayopendekezwa katika eneo hilo. Sasa tulilisema sana kwenye Kamati na nadhani tu ni kidogo *lapsus calamus, lapsus calamus* imeteleza tu kidogo. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nadhani *accepted* hii *version* ya Mheshimiwa Chenge inajibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalikubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 38

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 39

Kifungu cha 40

(Vifungu Vilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)

Kifungu cha 41

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki, kifungu kidogo kile cha nne ambapo ni masharti au vitu vitakavyoletwa mbele ya Meza kwenye majadiliano ili mtu akubaliwe kupewa *special mining license* hususan (a) na (b), mimi nachukulia kwamba tuna-*assume* taarifa itakayoletwa ni *very technical* ambayo iko *based on what they call due diligence exercise* ambayo kuna *feasibility results*, ambayo kuna *analytical work* imefanyika, kuna *statistical analysis* zimefanywa na *results* za kitaalamu hizi zinaletwa pale ili mtu huyu aji-*express* kwamba tumefanya haya kutokana na kazi hii, tunadhani mgodi wetu huu unaweza uka-*last* kwa miaka kadhaa. Tunaomba tupewe kibali hiki.

Sasa nilidhania inategemea sana sisi upande wetu *negotiating team* wana uzoefu na wana uelewa kiasi gani kuhusu hayo yanayoletwa kwenye Meza. Ni ile *technical know how* ya vitu hivyo vitakavyokuwa vinajadiliwa vimeletwa Mezani na swali langu kwenye mchango wangu wa maandishi ilikuwa ni hiyo kwamba utaalamu huo Mheshimiwa Waziri anatumia tunao, na kama tunao: Je, kutakuwa na *program* yoyote ya kuhakikisha kwamba wataalamu hawa wanapatikana haraka iwezekanavyo kuweza kuchambua na kukaa na wataalamu hawa kujadili vitu ana kwa ana na waka- *come up* na *results* ambazo sisi wote mwishoni tutakubaliana kwamba *yes, that was excellent?*

**MWENYEKITI:** Nadhani hili ni la Sera *rather than drafting*, sasa sijui...

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu halisi kwa swali la Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ni kwamba, Serikali imejiandaa na utaalamu huo upo. Lakini suala la utaalamu ni suala endelevu. Serikali kila wakati inaendelea kuboresha taaluma, uwezo kwa watumishi wake. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kila wakati Serikali inaendelea ku-*sharpen knowledge* kwa wafanyakazi wake.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye jedwali la marekebisho, kuna kifungu kipya cha (g) ambacho kinasema: *“Proposed plan on the procurement of goods and services available in Tanzania.”* Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kukubali kuingiza hiki kwa sababu ni kutambua juhudi zake za makusudi ambazo amewahi kuwaagiza wawekezaji wakubwa kwenye sekta ya madini, kuwataka wanunue bidhaa na huduma zinazopatikana Tanzania, kwa mfano nyama, maziwa na vitu kama hivyo, na hasa ukizingatia kwa mfano, kwenye migodi ile mikubwa ya dhahabu, Kanda ya Ziwa kuna maziwa mengi, kuna nyama ya kutosha, ni njia nzuri ya kuhakikisha kuwa tunafaidika na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu ni kwamba, katika Kanuni ingekuwa ni vizuri tusiishie kuona mpango wa ununuzi wa bidha na huduma zinazopatikana Tanzania, tuweke mazingira kwenye Kanuni ambayo yanawataka

wawekezaji hawa wakubwa, wananunua bidhaa hizi na huduma hizi kwa mujibu wa sheria ili kusudi tuwe na uhakika kwamba watafanya hivyo kuliko kuishia kwenye mpango, na mpango kuna wengine wanaweza wasiutekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua na wote tunafahamu kuna kiwanda cha maziwa kule Musoma, maziwa safi kabisa na baada ya miezi michache hivi, kuna juhudi kubwa inafanyika kuhakikisha kwamba kiwanda cha nyama cha Shinyanga kinafanya kazi. Kwa hiyo, migodi hii ndiyo itakuwa soko mojawapo la nyama itakayozalishwa hapo. Kwa hiyo, nilipenda hili lizingatiwe kwenye Kanuni ili kusudi mazao yanayopatikana Tanzania ni kweli yawe yananunuliwa na hao wawekezaji wakubwa. Ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Mlingwa kwa pongezi kwa Serikali. Kwanza ushauri tutauzingatia, lakini pili ni kwamba sharti hili, mpango huu ni sehemu ya leseni yake, maana yake ni kwamba atakapokuwa anapewa na sisi utekelezaji, tunaendelea kuliona kama sehemu ya vigezo ama masharti ya utekelezaji wa leseni yake. Asipofanya vile ni mojawapo ya uvunjifu wa leseni yake na matokeo yake yanajulikana.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niungane kuipongeza Serikali katika kifungu hiki kwa kuweka ufafanuzi mzuri wa mambo ambayo huyu mwombaji wa *special mining license* anapashwa awenayo. Lakini nilikuwa nataka kupendekeza vile vile katika hilo hilo la *regulations* au Kanuni zitakazokuja kutungwa kwamba katika kile kifungu kidogo, nafikiri baada ya *schedule*, kitakuwa ni (h) sasa. Yaani: *“Proposed plan with respect to the employment and training of cities of Tanzania and succession plan for expatriate employees if any as may be required by the employment of labour relations x.”*

Nilikuwa napendekeza tu kwa Mheshimiwa Waziri, watakapokuwa wanazingatia Kanuni kwamba Kanuni vilevile zifafanue ili tujue kwamba wanafungika ku-*train* watu wa kada zipi kwa muda gani na kwa viwango gani na wangapi vile vile, kwa sababu hizi ndizo faida ambazo Watanzania wanapashwa wazipate *including* ujuzi na maarifa pamoja na *experience* ambayo watakuwa wameipata baada ya kuzifanyia kazi. Kwa hiyo, naomba na hilo pia likadiriwe katika Kanuni. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ni *implied* kwenye *back plan* itakuwa *scrutinized*. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 42

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 44

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jedwali la marekebisho kuna kosa kidogo pale kwenye kifungu cha 44. Kwanza, ile D (iv) tuongeze 'd' pale kwenye *require* iwe *other matters as may be required*. Kakosa hako kangerekebishwa.

**MWENYEKITI:** Ni kweli.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazingatia.  
*(Kifungu kilichotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 45

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 46

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 47

Kifungu cha 48

Kifungu cha 49

Kifungu cha 50

Kifungu cha 51

Kifungu cha 52

Kifungu cha 53

Kifungu cha 54

Kifungu cha 55

Kifungu cha 56

Kifungu cha 57

Kifungu cha 58

Kifungu cha 59

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 60  
Kifungu cha 61  
Kifungu cha 62  
Kifungu cha 63  
Kifungu cha 64  
Kifungu cha 65  
Kifungu cha 66  
Kifungu cha 67  
Kifungu cha 68  
Kifungu cha 69  
Kifungu cha 70  
Kifungu cha 71  
Kifungu cha 72  
Kifungu cha 73  
Kifungu cha 74  
Kifungu cha 75  
Kifungu cha 76  
Kifungu cha 77  
Kifungu cha 78  
Kifungu cha 79  
Kifungu cha 80  
Kifungu cha 81  
Kifungu cha 82  
Kifungu cha 83  
Kifungu cha 84  
Kifungu cha 85  
Kifungu cha 86

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 87

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jussa, Ibara ya 87. Haya endelea.

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa tena fursa. Kifungu cha 87 katika hotuba yetu au maoni yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani tulipendekeza kwamba hii *gross value* ambayo ndiyo itatumika kupata *royalty* au kuhesabu *royalty* mapato ya *royalty*, basi kitumike au *gross value* ifanyiwe marejeo kwa zile *published reference* ya *price* kwa mawakala wanaoweka bei zinazoeleweka na tukatoa mfano wa *London Metal Exchange*.

Kwa hiyo, tunajua kwamba haitakuwa rahisi kugeuza katika kifungu kama sheria, lakini tunapendekeza vile vile kwamba katika Kanuni ambazo zitatumwa na Mheshimiwa Waziri, basi hii *reference* ya *gross value* itajwe kwamba itazingatia hizo *published reference price* ili kuisaidia Serikali, kwanza kuiondolea mzigo wa kutafuta



hizo thamani zenyewe, lakini la pili kuepuka *manipulation* ambayo inaweza ikafanywa na hawa waliokuwa wachimbaji wawekezaji katika sekta hiyo. Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Jussa kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wengine, ushauri huo ni mzuri, ni kati ya ushauri ambao tunaendelea kuufanyia kazi. Lakini kwa uhalisia ni kwamba sasa hivi hata kwenye *selling centers* za madini haya kujua bei ya madini kwa siku inajulikana kwa sababu sasa hivi dunia imeungana. Lakini ni ushauri mzuri, tumeupokea na tutaendelea kuufanyia kazi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mabadiliko makubwa ambayo tumeyafanya, ni kubadilisha kanuni ya kukokotoa mrahaba ambayo itatupatia mapato mengi sana kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Cheyo alivyozungumza iwapo pia tutawataka hao wengine waweze ku-*migrate*.

Lakini pia tulibadilisha hivyo kwa sababu hatukuwa na *control* na zile gharama zilizokuwa zinaondolewa katika kupata mrahaba na sasa hivi tumekwenda kwenye *gross value*, lakini hatuna *reference price* ambayo tutakuwa tunai-*refer*. Madhara yake ni nini? Madhara yake ni kwamba makampuni yanaweza kuwa yanauziana kwa *affiliates*, kwa hiyo unaweza kukuta kampuni ambayo inachimba Tanzania ikamwuzia *assist company* ambayo labda yuko Australia kwa bei ndogo tofauti na bei ya soko la dunia. Kwa hiyo matokeo yake tutapata mrahaba kidogo. Ndiyo sababu hapa tunapendekeza kwamba tuwe na *reference price* ambayo ni *published price*. *Anyway, we can choose any*. Sisi tumependekeza *London Metal Exchange*, lakini *you can choose any*.

Kwa hiyo, kusema kwamba mnayafanyia kazi, hapana. Hili ni suala la msingi sana kwa ajili ya ku-*maximize revenue* yetu. Kwa hiyo nilikuwa nadhani Mheshimiwa Waziri hili mngeweza tu kulikubali ili liweze kutusaidia na iwe rahisi kwa nyinyi wenyewe pia kuweza ku-*calculate* huo mrahaba.

**MWENYEKITI:** Lakini linatosha kwenye Kanuni, kwa sababu *London Metal Exchange* inaweza kubadilika ikawa *Zanzibar Metal Exchange*. Ndiyo, haya mambo lazima tuwe na biashara na sisi. Lazima tuwe na *actual accounts* zikae pale pengine Zanzibar. Imekaa vizuri, sasa ukiji-*commit* kwa London baada ya vizazi viwili baadhi ya sehemu za nchi yetu zinakuwa zina mvuto wa kuweka *exchange*, utakuwa umejibana. Kwa hiyo, ukiwa kwenye kanuni, unaweza kuweka.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haikuwa na nia ya kuji-*commit* kwa London peke yake na maelezo yako ni sahihi kabisa. Tuwe na *reference published price*. Wao wanaweza waka-*choose any*. Inaweza kuwa ni *Ujiji Metal Exchange*. Lakini cha msingi pawe na *published price* ambayo Wizara itakuwa inaitumia ili kuepuka hiyo kuuza bila kuwa na *arms lengths principles*. Hilo tu ndiyo ombi letu.

**MWENYEKITI:** Lakini ikae wapi sasa? Tusaidie hilo, sisi ikiwa kwenye kanuni...

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwenyekiti tuna *choice* mbili, ndani ya Muswada kwenye kipengele tunaweza tukasema *referring to publish prices* ndani ya kanuni Waziri akatengeneza kanuni ambazo na kwa sababu atakuwa na uwezo wa kuzifanyia *amendments from time to time* ataamua ni *price* ipi ambayo inatupa *favour* Tanzania kuliko nyingine yoyote. Lakini *reference* ya kwenye ile *provision* ingekuwa ni muhimu sana ili Waziri awe anafanya vile kwa mujibu wa Sheria. Maana yake tukiiacha hivi jinsi ilivyo tunaweza tukatumia bei za *affiliats* ambazo wanauziana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, suala hili kwanza lina maslahi kwetu, kwa sababu linatuongezea kiasi ambacho tunapata kutoka kwenye madini. Ndiyo maana tukasema tutalifanyia kazi na mahali pake ni kwenye kanuni kwa sababu hiki kitu ni *variable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaji-*commit* sisi kwamba tunalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Nadhani inatosha hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 88  
Kifungu cha 89  
Kifungu cha 90  
Kifungu cha 91  
Kifungu cha 92  
Kifungu cha 93  
Kifungu cha 94

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 95

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 96

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kipengele hiki cha 96 kwanza ni kuonyesha kwamba yule aliyekutwa mwenye ardhi ni lazima apate fidia. Lakini ilivyowekwa kwenye Sheria hii, haimzuii yule aliyepata *mining rights* kuendelea na shughuli zake. Katika sheria nyingi wanaweka hiyo *condition* kwamba huwezi ukaendelea na uchimbaji au na *activity* mpaka *the correct compensation* imefanyika. Halafu ukienda kwenye *section (4)* ndiyo inatuonea kila siku. Inasema: “*Where the value of any land, has been enhanced by prospecting or mining operations,*

*compensation payable pursuant to sub-section (3) in respect of the land shall not exceed any amount which would be payable if the value of the land not been enhanced.” So, enhanced.*

Kwa hiyo, umeshagundua hiyo *area* ni ya thamani, eti yule uliyemkuta pale asi-*benefit*, siyo muhimu kwake. Leo ukijenga daraja la kwenda Kigamboni, nyumba zote ambazo ziko Kigamboni bei yake itakwenda juu. Lakini ukipata Urambo dhahabu, eti hiyo *area* thamani yake isiongezeke na ndiyo Sheria tunayoitunga hapa. Mimi nafikiri ndiyo maana wananchi wote ambao wanakutwa na madini ni sawa sawa na kukutwa na kifo. Kwanza wewe huhusishwi katika mazungumzo, nani anapewa hiyo *right*? Yule anayepewa *right* anakuja, huna hata nafasi ya kuweza kuzungumza naye atakulipa kiasi gani. Halafu juu yake ni kwamba hata kupata kujua hapa kuna thamani, unaambiwa ule uthamani ambao Waziri anajua, wewe haukuhusu huwezi uka-*benefit*. Mimi nafikiri hapa ndiyo maana hatupati mafao kwa kuwa na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza, kama Mheshimiwa Waziri anaweza kututafutia utaratibu ambao kwanza ni kuhakikisha kuwa tutakuwa na *right compensation*, lakini pili, yule aliyepewa *right* asiendelee kabla hayo mazungumzo ya *compensation* hayajamalizika. Ndiyo hilo tu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-section 4* ya kifungu kidogo (iv) cha kifungu cha 66 kinaeleza wazi. Labda nianze kwanza kuhusu huyu mtafutaji au mchimbaji kwamba anakuja bila kuwa na mazungumzo na wewe, lina msingi wake tu. Sisi umiliki wa ardhi Tanzania, mali yote, ardhi ni ya Serikali. Sisi ni kama wapangaji, tofauti na nchi nyingine ambazo unapomiliki unamiliki ukiwekea kitu.

Lakini la pili, ukikisoma vizuri kifungu kidogo cha nne, sasa kinatambua tofauti na sheria iliyopo sasa kwenye Muswada huu kinatambua kwamba eneo ambako limefanyiwa *prospecting* ama hata matarajio ya kuanzishwa mgodi linakuwa na thamani zaidi ya thamani ya kawaida. Sasa hiki kifungu kidogo cha nne kinaelezea, thamani yako ikishafanyika tathmini ya kiasi gani, sasa kwa kuzingatia ongezeko la thamani hiyo wanasema fidia yako isiwe juu ya hilo ongezeko la thamani iliyoletwa na utafiti au upatikanaji wa madini hapo. Kama sikosei, ninavyomwelewa baba yangu, Mheshimiwa Cheyo ni kwamba anataka kusema huko juu kusiwe na ukomo, yaani iende hata zaidi ya hicho kiwango ambacho kimeongezeka kwa sababu ya ongezeko la thamani ya utambuzi kwamba kuna madini hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali hiyo unaweza kukuta imeshafanyika *prospecting* mahali, watu wanataka kuanzisha mgodi na mgodi huo ni kwa maslahi ya Taifa. Watu wanadai fidia ambayo kwa mfano, fidia sasa ingekuwa labda shilingi milioni 100, mtu anaweza kukwambia baada ya kuwa *enhanced*, baada ya kuwa *enhanced value* yake kwa sababu imethibitika kuna madini, mtu anaweza kuja anadai shilingi trilioni mbili. Sasa katika mazingira hayo utafanyaje? Ndiyo hiki kifungu sasa kinasema fidia yako isiwe juu ya ile thamani ambayo tayari itakuwa imeshaongezeka baada ya lile eneo kugundulika kwamba kuna madini. Maana hilo eneo likishagundulika

ni tofauti na ardhi nyingine, hata kama mngokuwa mmejenga nyumba za kiwango kile kile au maendeleo yale yale, lakini maadam hapa kumegundulika madini, thamani yake inapanda tayari katika utaratibu mpya unaokuja. Kwa hiyo, ukiruhusu kwamba iendele, sasa tunaweza kufika mahali haiwezekani hata kufidia. Hiki kifungu ndiyo kinazingatia hali ya namna hiyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kwanza kuna vipengele viwili ambavyo natumaini hajavijibu. Kwanza hajanjibu kama kuna uwezekano katika *section* hii ukaweka kinga kwamba wewe hautatoa *mining licence* mpaka hayo mazungumzo yamekamilika. Ili ku-*save rights* za wale kwamba yule mwenye *right* anaweza akaendelea *whether* kuna *compensation* au hakuna *compensation*. Hiyo ni *one part* ambayo bado sijajibiwa.

Lakini pia ukisoma kile kifungu cha nne, labda mimi nakisoma vibaya. Niko *willing* kabisa with *all humility* kusahihishwa. Ukisoma ile sentensi ambayo inasema: “*the value shall not exceed any amount which would be payable if...*,” nairudia: “...*if the value had not been so enhanced...*” you see! So, in actual fact what, mimi ninavyoisoma hii ni kwamba *enhancement* ile imekuwa *completely ignored* ndiyo kifungu hiki kinavyosema. You see! Wewe utakuwa *compensated as if* hapakuwa na madini hapo. Ndiyo maana yake. Kwa hiyo, Bunge lako Tukufu linatunga sheria ya ku-*deliberate* kuwapunja watu ambao hawana sauti. Ndiyo maana yake?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo tafsiri ambayo hata mimi naona ndivyo ilivyo na kuna msingi wake. Nafikiri ndiyo msingi ule sasa wa kuelezea. Lakini anavyosema Mheshimiwa Cheyo ndiyo ilivyo kwamba nafikiri ni Kiingereza, *the Queen’s language is very simple*. Wanasema: “*Where the value of any land has been enhanced by prospecting or mining operations compensation payable person to sub-section (3) (ambayo ipo juu hapo) in respect of the land shall not exceed any amount which would be payable if the value had not been so enhanced.*” Kwa hiyo, unarudi kwenye *status call* pale na ndiyo maelezo kwamba sasa ukifanya vinginevyo, utafanya huyo mtu ambaye anakuja itakuwa *very expensive for him*. Labda hiyo ndiyo ya kuelezea tu, lakini anavyosema Mheshimiwa Cheyo ndivyo ilivyo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mashaka haya ya Mheshimiwa Cheyo na mimi nayapata katika kifungu hicho hicho na pengine kinga yake inaweza ikapatikana kwa Waziri kuweka katika kanuni zake. Katika mazingira ninakotoka mimi ambako ardhi inakuwa *owned communally* kwa ajili ya malisho ya mifugo na pale ambapo imegundulika kuna madini na kwa vyovyote sheria hii itaruhusu madini yale yatoke kwa manufaa ya nchi, lakini wakati huo huo kuna watu utawaondoa pale na katika eneo unalowaondoa hakuna kahawa, hakuna mgomba utakaokata, lakini ni malisho ya mifugo kama ilivyo katika maeneo yale ya machimbo ya *Tanzanite* pale katika Kijiji cha Naisinye na Langasiti.

Lakini wale wameondolewa wakapishe migodi pale. Sasa watu hao kwa sababu wanahitaji fidia, nilifikiri wanahitaji fidia kwa maana umewatenganisha maeneo ya malisho na maeneo ya maji yaliko. Sasa kunahitajika *compensation* ya namna ambayo itahakikisha watu wanakwenda ku-*settle* maeneo mengine. Sasa hili nilifikiri ni muhimu

labda Waziri aingize pia katika kanuni ili fidia ipatikane hata katika maeneo haya ambayo yanamilikiwa kwa ujumla na jamii ya wafugaji na hasa maeneo ambayo kuna madini pia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tuwasikie kwanza, maana yake wapo kadhaa. Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kama alivyosoma Mheshimiwa Cheyo ule mstari wa mwisho na ukiangalia kwamba Serikali, Sheria yenyewe hii imekuja ikiwa inatambua kwamba huwa kuna *unfairness* katika *compensation* na ukiangalie ile *foot note* inasema: “*Rights and a mineral right to be exercised reasonably.*” Yaani tayari wanaelewa kuna *un-reasonability* katika kulipa *compensation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisoma hapa mbele kwenye *sub-section (3)* ya 96 anasema inapotokea mtu mwenye *mining licence*, anasema *is liable*, ule mstari wa mwisho, *is liable to pay the lawful occupier fair and reasonable compensation.* *Fair and reasonable* ni nini? Lakini inakuwa tena *disqualified* na hii *statement* inayosema mwisho kabisa: “*if the value had not been so enhanced.* Sasa kwa kweli wananchi wetu wengi wanaotoka katika maeneo ya uchimbaji ambako kunagundulika madini inakuwa ni kama kiama. Wanatoka wakiwa na manung’uniko, wanakuwa maskini zaidi na hata ukiangalia katika takwimu tulizopewa za Mfuko wa Majimbo, takwimu iliyoangaliwa ya watu wanaotoka kwenye maeneo ya machimbo ndio masikini kuliko wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeiomba Serikali, inaposema *enhanced* ya kwanza, basi iwe na kule mwishoni isii-*disqualify* tena, maana hii ni *claw back clause*. Umepewa, halafu tena wakatoa. Sasa hii sio sheria nzuri. Mimi ningeiomba Serikali hapa ione jambo hili ni *very serious* kwa maslahi ya wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Mimi nadhani ingeishia pale penye: “*to pay the occupier fair and reasonable compensation*”, *full stop*. Kama ukiondoa hata ile ya nne, basi, inajibu yote. Kwa sababu hoja za Waheshimiwa Wabunge hapa ni za kweli kabisa.

Kwenye ile *schedule* ya Wizara ya Ardhi, kulipiwa mpapai, sijui nini, halafu yeye abaki achukue dhahabu yote na mpapai ni Sh. 20,000/=, mwembe ni Sh. 12,000/=, hii kweli jamani? Kama ardhi thamani yake imepanda kwa sababu pamegunduliwa madini yenye thamani kubwa, thamani hiyo iweze kuwa *fairly*, iangaliwe kwa haki kabisa ili mhusika au wahusika waweze kulipwa. *This is nothing more, you know; fair and reasonable compensation.* Lakini ukirudi kwenye ile *schedule* ya ardhi ile ambayo ndio tunayoitumia tunapopitisha milingoti ya umeme, mabua shilingi tano, nini, hii haifanani hata kidogo! Kweli watu wetu wasipate kitu! Hii hapana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushauriana na Waziri Mhusika, tunashauri kwamba kifungu kile kidogo cha (4) kiondolewe kusudi kisiondoe zile haki za kifungu cha (3). (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, hiki kinazungumzia tu *disturbance* na *damage*. Kwanini hatuishii kwenye *fair and reasonable compensation*, basi? *Damage* ndio hiyo kukata milimao; hii haitoshi kabisa jamani. Kweli tuwahurumie watu hawa. *Nature* imewaweka mahali penye thamani kubwa, wangukuwa na mtaji wange-*mine* wenyewe. Sasa unaambiwa basi tumekusumbua, nyumba yako ya nyasi tutaifidia na miembe miwili tuliyoikuta, ahsante sana. Halafu jamaa linajikita pale linatengeneza mabilioni yanayokwenda. Aah! (*Makofi*)

Nadhani, kifungu hicho kinaafikiwa. Tunaishia *fair and reasonably compensation*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba wewe ni Mwanasheria na bila ya shaka nafahamu pia kwamba unajua tofauti kati ya *surface rights* na *land rights*. *Minerals* ambazo ziko *under surface* sio mali ya yule mtu ambaye yuko kwenye eneo hilo, huo ndio ukweli mgumu. *Well*, ndio ukweli mgumu, ndio sheria ya nchi, kuzomea au bila kuzomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri...

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

**MWENYEKITI:** Endelea AG. Jamani naomba tumsikilize Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kazi ni ngumu sana! (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mmh! Kazi nyingi ni ngumu, hata ya Waziri wa Nishati ni ngumu sana pia. (*Kicheko*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ile *disturbance* na *damage*, *vita-cover* ule usumbufu wa kuondoka pale na ninafikiri tuache tu mpaka pale mwisho, ila tuondoe kile kifungu cha (4) kwa sababu ndicho kinachoondoa zile haki. Ukikiondoa kile, hakitakuwa na matatizo kokote. Kwa sababu, ukikisoma, kuanzia pale, kinasema: "*fair and reasonable compensation in respect of the disturbance,*" yaani hata kumhamisha pale, *or damage according to the respective rights* ambazo ni kwenye sheria ya ardhi au sheria nyingine au, *interest of the lawful occupier in the property concerned, this is wider* kuliko hiyo ukiishia pale ulipokuwa unasema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ni hivi, huyu mkulima mfugaji, madini yaliyopo chini sio yake, hiyo tunaielewana. Lakini mara madini yanapogunduliwa panakuwa na thamani zaidi ya ile mipapai au malisho yaliyopo.

Tunachoomba hapa kwa ulimwengu wa kisasa ni kwamba alipwe *fair and reasonably compensation*, basi. Ukimrudisha kwenye kurudishiwa mimbaazi, sio haki. Sasa naomba tupige kura. Tutapiga kura. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna haja ya kura. Nafikiri mimi sibishani na wewe, kwa sababu yale maneno unayosema yaondolewe pale ndio yanayotoa haki kwa huyo mtu. Mimi ukiishia pale, nitasema tu kwa sababu sitaki kubishana na wewe, ninanyamaza, lakini nitakuwa *very unprofessional* na mimi sitaki kuwa *unprofessional*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria, kutunga Sheria ni siasa. Hatuwezi watu wetu hawa wanaondolewa kwenye migodi, maeneo yana madini yenye thamani kubwa, kwa mfano sasa Kibakwe kwa Mheshimiwa Simbachawene, wamegundua madini yana thamani kushinda almasi, ndio inaitwa *red* nini!

**MJUMBE FULANI:** Safaya.

**MWENYEKITI:** Sasa unapomwondoa yule mwananchi wa Kibakwe unamwambie ni pale tu tumekusababishia athari za mimea yako na nyumba yako, *mostly* nyumba ya nyasi, basi. Halafu anayeingia pale anatajirika kuliko kifani. *It is just not fair, it doesn't work*. Ni lazima Kamishna aweze kupima aseme haki ya Mtanzania hapa ni kiasi fulani kwa sababu mahali hapa sasa pana thamani. Tukifanya hivyo hata hii migogoro tunayoipata ya watu kuondoka wakiwa fukara zaidi, eti yakigunduliwa tu madini ni laana kwako, wewe utaondoka uwe masikini zaidi kuliko wenzio wote; kwa nini? *This doesn't make sense*. (*Makofi*)

Jamani, mkitaka, tupige kura tu. Maana ndio Kanuni! Eeh! Kwa sababu tunabishana nini? *Reasonable and fair compensation* kama itakavyopimwa na Kamishna wa Madini, ili kutenda haki kwa watu wetu. Mwisho ni *reasonable compensation* hapo hapo. (*Kicheko/Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake*)

Kifungu cha 97

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa *spirit* hiyo hiyo naona kifungu cha 97(a), ninashauri kwamba asiwe ni *Mineral Right Holder* ndio amu-advise huyo *keeper* wa *land* kuondoka, bali iwe ni *Local Government Authority* lakini baada ya kuwa wameshakubali kubadilisha *land use* na huyu *occupier* wa hii *land* ameshakuwa *compensated*.

**MWENYEKITI:** Sasa tunatunga sheria. Muwe mnalenga mahali ili tujue tunatunga kitu gani sasa. Sasa hiyo ya kusema fidia iwe tayari imelipwa, itakaa wapi hiyo sasa?

**MHE. CHARLES M. KAJEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika kifungu cha (b), ndio wanasema kwamba ana-*submit proposal ya plan ya compensation and relocation*. Lakini huku ya kwanza anasema huyu *Mineral Right Holder* ndio anamu-*advise* huyu *occupier wa land* kuondoka.

Sasa mimi ninafikiri hapo ndio kutakuwa na migongano; ni vyema kwanza huyu *Mineral Right Holder* kwanza aongee na Serikali ya eneo husika, akishakubaliana na *amendment ya land use plan*, then ndio wanaweza wakakubaliana kwamba huyu *occupier* sasa anaweza kuondoka. Lakini hivi ilivyo hapa, inamfanya huyu aweze kumwondoa huyu *occupier wa land* kabla hata hajampatia *compensation* na matatizo kama haya tunayo mahali pengi sana katika sehemu za migodi.

**MWENYEKITI:** *Actually* ni kama vile ile ya (a) ingeshuka chini, labda (b) iwe (a). Yaani kwanza, yule anayeishi pale aione hiyo *proposed plan on compensation*. Nadhani inakuwa *fair*. Usianze kumfukuza kwanza halafu ndio *Authorities* waione *plan of compensation*. Nilikuwa nadhani utaratibu huo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Kajege, ni kama kinavyojionesha, ndio hicho ambacho kimeandikwa kwenye kwenye kifungu kidogo cha (a). Kwa sababu anasema asiondolewe kwanza, ni lazima ifanyike *consultation* na Mamlaka ya pale ambapo kama ni Kijijini, itakuwa ni Serikali ya Kijiji. Kwa hiyo, kimsingi analoongea Mheshimiwa Kajege, liko-*covered*. Sasa labda kama unavyosema kwamba ni ku-*interchange*, hiyo ni kitu kingine.

Lakini kwa maana ya *content* kwamba hasa zinajitosheleza, kutomwondoa kabla ya kuwasiliana na Serikali iliyoko pale ama kuishirikisha Serikali iliyoko pale, ni jambo ambalo liko dhahiri kwenye sehemu (a).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani ile (b) ingekuwa (a) na inamshirikisha huyo. Maana awe anaona, sio alipwe, aione ile *proposed plan ya compensation, relocation and resettlement just for good orders' sake*; kwamba kiwe ndio kitu cha kwanza, halafu haya mengine sijui unasema *advised owner au agree on a time table for vacation of the area?*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *order* tu ya ku-*arrange* hizi, nadhani sio jambo lenye madhara; halibadilishi maudhui ya hii sehemu.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 98  
Kifungu cha 99  
Kifungu cha 100



(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 101

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 101, kinatoa *power of entry* katika maeneo yale ya migodi. Na kama tulivyofanya masahihisho yale ya kuingiza *agency* ile, na kwa kuwa, *role* yake bado ni ileile ya “*to monitor and audit quality and quantity of minerals produced,*” sasa ni muhimu basi na *power* ya *agency* nayo ikapewa nafasi katika nafasi hiyo kama inavyosomeka kwamba *Commishner or an Authorised Officer may at any time inter upon any area of which, a mineral right has been gntated or any premises or working places, other than...*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christopher, hilo tumeshalifanya kwa kuangalia kifungu cha (4). Tumemweka huyo *as an Authorised Officer,* ni *a type of an Authorised Officer.*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 102

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 102 kinahusiana na *dispute settlements.* Katika maelezo ya Kambi ya Upinzani, tulizungumzia umuhimu wa kuanzishwa kwa *Tribunal,* ambapo Mheshimiwa Waziri, ameji-*commit* katika uanzishwaji wa *Tribunal,* tunakubaliana na hilo kwa sababu hatuwezi kuianzisha sasa.

Lakini katika *amendments* ambazo zimekuja na nilikuwa nashauriana kidogo hapa na Mheshimiwa Jussa kuhusiana na Kamishna kutoa ile *order* yake kuwa *enforced* na Mahakama, ambapo wameondoa: “*The order shall be enforced*” na wameweka *course to be enforced.* Sasa tunaona kama ni kitu kile kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*withdraw;* Mheshimiwa Jussa, ameniambia kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ameshampatia maelezo na iko *okay.*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 103

(Kifungu klichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 104

Kifungu cha 105  
Kifungu cha 106  
Kifungu cha 107  
Kifungu cha 108

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 109

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kutambua *seniority* ya wale ambao tumetangulia hapa. Kweli nichukue nafasi hii ya pekee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, ambao kwa namna moja au nyingine, pamoja na Waziri waliotoa kwa dhati kabisa pongezi kwangu kwa kazi tuliyofanya kwenye Kamati. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la 109 mimi nadhani kusudio la Serikali ni zuri sana, lakini tulivyoliandika linapotosha msingi wenyewe. Katika kifungu hiki, dhana inayotafutwa ni kuwapatia wananchi wa Tanzania nafasi ya kushiriki katika umiliki wa migodi pale ambapo watapenda kufanya hivyo na fursa hiyo imetolewa.

Katika hatua hii, hatuuzii hizi hisa Serikali imeshapata haki yake tangu mwanzo kwenye kifungu cha 10 tulipoanza, ia Serikali na yenyewe kama mwanahisa katika Kampuni hiyo, wakikubaliana kwamba na yenyewe inataka kutoa sehemu ya hisa zake ziende zikauzwe kwenye soko itakuwa ni sehemu ya hayo.

Lakini hapa msingi tunaouweka ni kusema kwamba *requirement on a procedure for selling shares to citizens of Tanzania*. Hiyo ndio shabaha ambayo inakusudiwa hapa na sio Serikali katika hatua hiyo iuziwe hisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba Serikali pendekezo hili tulikubali kwa sababu linajieleza lenyewe kama nilivyolieleza, lakini limekosewa tu katika utekelezaji wake kupitia Muswada huu.

Kwa hiyo, naiomba Kamati yako ikubali kwamba badala ya kusema: “*to the Government*” tuseme “*to the Citizens of Tanzania*” ili pale ambao watapewa fursa hiyo, wanaopenda kushiriki kama walivyofanya juzi kwenye nafasi iliyotolewa kwa *Barrick*, wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimejieleza vizuri, nadhani Kamati yako itanielewa.

**MWENYEKITI:** Umejieleza vizuri tu na ninadhani kuiboresha ingekuwa, “*to Tanzanian Nationals.*” Ina-read vizuri zaidi nadhani kuliko *to the citizens* na kuiweka na nchi yetu tena.

Mheshimiwa Waziri, kuna shida hapo? Maana yake hii ukisema *Government*, ni yale mambo ya *expropriation* tena. Tunauzia Serikali inayosema inataka kujiondoa kwenye biashara, halafu iuziwe!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hakuna tatizo. Tulishateta na Mheshimiwa Chenge.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Job Ndugai.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kwenye fungu hili hili la 109, kama tunavyokumbuka hapo mwanzo linaendana sana na lile fungu la 10 tulilijadili pale mwanzo sana. Mimi hoja yangu mojawapo ilikuwa ni hiyo ya *Tanzanian National* ambayo imeshakubaliwa.

Lakini tatizo langu la pili kwenye kifungu hiki ni pale inaposema *Minister shall, in consultation with* hawa watu wenye *special mining licence* katika wajibu wa Waziri wa kutengeneza *regulations*, na mahali pengi tumesema Waziri atatengeneza *regulations* na Waziri anapotengeneza *regulations* yeye ataangalia ni wadau gani ambao wanapaswa kuwa katika zoezi zima la kupata *regulations* hizo za Serikali. Sasa ni kwa nini hapa tunamlazimisha Waziri kwamba lazima a-consult hawa katika masuala haya ya *shares* na hakika wadau wako wengi, wako wengi *Tanzania Chamber of Commerce*, wako watu wa *capital market*, wako watu wengi ambao ni wadau katika zoezi zima la kutengeneza *regulations*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pendekezo langu lilikuwa kwamba tusimfunge Waziri kwamba lazima katika kutengeneza hizo *regulations* awa consult watu fulani peke yao. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, angesema *and other stake holder's* inakufaa?

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Sawa kabisa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kwa kuanzia ni kwamba kwenye mazingira ya kwamba Serikali tayari ni mbia kwa sababu ya zile *shares free cards interest* kule inajenga hoja ya kwamba ni vyema kuongea na kufanya *consultation* na kukubaliana kile kiwango ambacho kitakuwa *prescribed*. Kwa sababu na sisi wakati huo tunaweza kuwa tayari ni wana hisa katika hili. (Makofi)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kifupi sana sina nia ya kutofautiana sana na Mheshimiwa Waziri lakini picha inayotokea hapa ni kama vile wadau ni wawili tu, Serikali na hawa waliotajwa hapa. Ndio maana nilikuwa na nia ya kwamba tuweke *and other stake holder's* isiwe hawa wawili peke yao kama hivyo ndivyo. Kwa sababu jukumu la kutengeneza *regulation* kimsingi ni la Waziri kwa kuwa anataja mdau mmoja kwa nini wengine ananyamaza?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mpango uliopo wa wanahisa ni kwenda kuandikisha hisa kwenye soko la hisa. Sasa labda nisaidiwe labda sijamuelewa vizuri Mheshimiwa Job Ndugai, wadau wengine kwa sababu hisa hizi sasa zitakuwa zimeshikiliwa kwa niaba ya wananchi sasa nilikuwa naomba tu nisaidiwe kuelewa wadau wengine ni akina nani pengine kwa mantiki ipi katika hatua hiyo ya kutaka kwenda kusajili labda nisaidiwe kidogo hapa sijaelewa vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Labda atasaidia Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa tutafika tu huko.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kutunga Kanuni ni la Waziri mwenye dhamana, *mechanisms* za utungaji wa kanuni hizi yeye mwenyewe anafahamu. Kwa hiyo, kama ni kushirikisha wadau anawafahamu, kwa hiyo, kwa vyovyote vile wadau watahusika na mpaka kwenye ngazi ya Bunge hapa tuna Kamati ya sheria ya ndogo ndogo wanahusika. Sasa kwa sababu suala la msingi ni utungaji wa kanuni hakuna sababu ya hata ya kuweka maneno yanayosema *in consultation with holders of minimum special mining licence*, ingesomeka kama ifuatavyo; *“The Minister shall make regulations prescribing the minimum share holding requirement and procedures for selling shares to the Tanzanian Nationals and accordance with the provisions of the capital market and securities act offering shares to the public through listing with a stock exchange*, basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hapa mimi naona tunakwenda mbali zaidi, hawa watu wamewekeza dola 400, dola bilioni moja, sasa huu uzalendo wa kusema nikishaziandika tu ofisini natangaza watasikia kwenye *official gazette*. Nadhani Serikali ilikuwa na maana hapa hakuna mdau mkubwa ni mdau ambaye kama mbia kabisa ni yule anayewekeza ndiyo, uungwana tu, ni ungwana kwamba mtu katika nchi ya mbali kaja kuwekeza na tujue tu kwamba tukiweka yale yanayotisha sana itayaathiri sio sekta ya madini peke yake hata utalii watasema kumbe inaweza kutungwa wakati wowote kanuni za kukulazimisha uwauzie Watanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani *consultation* sio kitu kibaya sio kwamba watatushinda, tunashauriana tu kama hilo limeeleweka na hamleti kipya sijui mnasimama kufanya nini tena kwenye hili. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kuna jipya kwenye hilo hilo.

**MWENYEKITI:** Nitaruhusu jipya tu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na nilisema wakati tunazungumzia kipengele cha 10(2) na Waziri akaahidi kwamba atatoa maelezo kwamba hivi vipengele ni viwili tofauti. *In principle* hivi vipengele ni *redundant* ukisoma 109; *The Minister shall, in consultation with holders of special mining licence* tume-define

*special mining licence* ni uwekezaji wa kuanzia dola milioni 100, na tumesema kwamba watu watakaoingia *MDAs* ni watu wenye kuwekeza kuanzia dola milioni 100 na tayari kwenye masharti ya kupata mkataba tumeshasema kwamba Serikali itachukua hisa pale kwenye masharti ya kupata mkataba. Kwa hiyo, *the whole 109* yaani 102 na 109 haviendani kabisa ndiyo maana nilikuwa nimesema mwanzo wakati wa kifungu cha 102 kwa ajili ya kuweza ku-align hizi *section* mbili lazima ziwe *aligned* kwa sababu tunazungumzia kitu kile kile, sasa Waziri akasema kwamba kuna maelezo tofauti ambayo anayo lakini hajayatoa na *humbly* kabisa kama Waziri ana maelezo tofauti aweze kuyatoa lakini nadhani kuna umuhimu mkubwa sana wa ku-align hivi vipengele viwili 102 na hiki kipengele cha 109.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba maelezo ya Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Zitto, mgongano wewe unauona wapi sasa hebu tamko hizo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 109 kinasema *The Minister shall, in consultation with holders of special mining licence.* Ukiangalia *schedule of amendment* tume *define* sasa kwa mara ya kwamba *mining holder* wa *mining licence* anapaswa kuwa na *investment* ya kiasi gani. Ukienda kwenye kuingia mikataba na tumesema ni dola milioni 100, ukienda kwenye kuingia mikataba tumesema kwamba uwekezaji wa dola milioni 100 *and above* ndiyo tulichokisema kwa hiyo, *holders* wa *mining licence* ndiyo mwenye mkataba kwa maana ya ile.

Sasa huku kifungu cha 109 tunarejea *the only thing* ambayo iliongezeka hapo ni *a listing* ambayo tunapaswa kuiweka kule wakati Serikali inafanya *negotiation* ya *free carried interest state participation* na tulisema kabisa kwamba ni *state participation* na *listing* inapaswa kuwa sehemu moja hatupaswi kuwa na vipengele viwili tofauti. Lakini Waziri alisema atatoa maelezo kwamba hii ina maana tofauti sasa nilikuwa nahitaji hiyo maana tofauti ni ipi ambayo ilikuwa maana yake Waziri hajaeleza hiyo maana tofauti.

**MWENYEKITI:** Maana ya tofauti ndiyo hiyo *listing*.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** *Listing* 109 inapaswa kuwa *lined* na 102 ili *listing* iwe wakati tunaingia mikataba Mwenyekiti hapa ni *technically* tu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho niliahidi ndiyo nataka nikitolee maelezo kwa Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba kwanza kuna vitu viwili tofauti hapa, kile kifungu cha kumi inaweza kuwa hatua za awali ambapo shughuli za biashara haijachanganya mpaka ukajisajili kwenye soko la hisa. Hapa kifungu cha 109 shughuli imeshaanza namna gani kwamba tumeshakuwa na sifa hilo la kwanza.

Lakini la pili, namuelewa Mheshimiwa Kabwe Zitto *assumption* anayoitumia hapa ni kwamba kila mwenye mtaji zaidi ya dola 100 lazima awe na mkataba wa *MDA* si lazima kwa sababu anaweza kuja mwekezaji ana fedha yake akaangalie ile *package* ya

*physical regime* yetu akakubali akaridhika tu akasema mimi nimeridhika na utaratibu wenu huu wa kodi zenu wa ushuru wenu nawekeza bila kutokuhitaji mkataba maalum wa MDA. Sasa haya ndiyo maelezo ambayo nilikuwa nimeweka kama akiba ya kuja kumsaidia Mheshimiwa Kabwe Zitto ili twende kwa uelewa mmoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Serikali inatuchezea.

**MWENYEKITI:** Wewe bila ridhaa yangu unasimama mara tatu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Samahani Mwenyekiti, samahani, umeniruhusu sasa?

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 110

Kifungu cha 111

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 112

**MHE. ISMAIL JUSSA LADHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida na nadhani kuweka *credit* na kuweka mambo kwa uwazi hiki kifungu cha 112 kinahusu *regulations* na hakikuwa *generally* tu lakini kimesema pale mwanzo kwamba bila kuepuka *generality*, lakini kimetaja mambo mengi ambayo yanaweza kutungiwa *regulations*.

Sasa nilikuwa nasema hapa katika mjadala kuna vitu kadhaa tumeshavitaja *specifically* na tumevitaja kwamba viongezwe katika *regulations*, tumetaja kwa mfano suala hili la kwamba kuwe na *reference* au *publish reference price*, tumetaja suala lile la *employment* na *training* wanayopaswa kufanya, awali pale kuna mambo mengine nilikuwa naomba yale kwa ajili ya *record purpose* iwe katika *Hansard* lile lile alilosema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali asiye akaambiwa amechomeka vifungu basi yale mambo yote ambayo tuliyataja iwekwe katika *record* kwamba hapa yataingizwa katika kifungu hiki ili yawe ni sehemu ya orodha ambayo mambo yatatungiwa *regulations*, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hakuna haja ya kufanya hivyo kwa sababu unapoisoma hii sheria pale panapowekwa uzito haya madogo madogo haya kama *to prescribe fee charge rent* nayo yamewekwa hapa ukiyachanganya na *listing* na *fee drafting* itakuwa sio nzuri, ndiyo maana wameweka hivi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Umechelewa Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama mwanzoni.

Kifungu cha 113

Kifungu cha 114

Kifungu cha 115

Kifungu cha 116

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tumechoka. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Wewe umechoka unayechelewa. *(Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali la kwanza ni masahihisho madogo *sub section 2* msitari wa pili kuna maneno pale mstari wa pili mwisho yanayosema *specified* halafu limeandikwa neno “I” nadhani palipaswa pawe na neno *specified in the notice* kwa hiyo neno “I” pale ni *in*.

**MWENYEKITI:** Ni wapi hapo unasoma?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Ukurasa wa 79, *sub section 1, sub section 2*.

**MWENYEKITI:** *In the notice* kweli ni *typing error*.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Halafu hapo hapo *sub section 3* mstari wa pili ni *typing error or death or* kuna herufi “s” pale katikati kwenye *sessions of membership*.

**MWENYEKITI:** *or is unable is there should be “I”* pale, sawa kabisa.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamuita Waziri wa Nishati na Madini ambaye ndiye mtoa hoja kutueleza taarifa ya shughuli za Kamati namuomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge atumie Kanuni ya 150 ili tutengue Kanuni ya 28(2) na kwa maana hiyo tuweze kuendelea baada ya saa 1:45 hadi shughuli zote za Bunge zikamilike.

### **HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa vile muda tulionao hautatosha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Mkuu wa Shughuli ya Kiserikali Bungeni kumaliza hotuba yake ya kuahirisha Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge, naomba kutumia masharti ya Kanuni ya 150(1) kuomba kuwa Kanuni ya 28(2) itenguliwe ili Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kukamilisha hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu ni ya kutengua Kanuni ya 28(2) ili tuweze kumaliza kazi ndogo sana iliyosalia ituwezeshe kuendelea na ratiba ya semina kesho. Kwa hiyo, sasa nitawahoji. Nilivyosikia walioafiki wameshinda. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini taarifa ya Kamati.

***Muswada ya Sheria ya Madini wa Mwaka 2010  
(The Mining Bill, 2010)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria kifungu kwa kifungu na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika na kwa hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010 yaani *The Mining Bill, 2010* sasa ukubaliwe.



Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja ya kupitisha Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010 *The Mining Bill, 2010* imetolewa na Mheshimiwa Waziri imeungwa mkono na sasa wajibu wangu uliosalia ni kuwahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge*)

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda na kwa hiyo namuita Katibu ili asome utaratibu unaofuata kwenye Muswada huu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 91 Muswada sasa umesomwa kwa mara ya tatu na kwa hiyo nauthibitisha kwamba sasa Muswada huo umepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatua iliyobaki ni kuufikisha kwa Mheshimiwa Rais ili uweze kupata kibali chake. (*Makofi*)

Naipongeza sana Serikali pamoja na Wizara, huu ni moja ya Miswada ambayo imefanyiwa kazi kubwa sana na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mara nyingine ilibidi Spika atumie ubabe, lakini haya ndiyo mamlaka sasa utafanyaje maana yake huwezi kukabidhiwa Mamlaka halafu unaogopa kuyatumia. Kwa hiyo, niliyatumia kwa nia njema ya kuendeleza nchi yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

## **HOJA ZA KAMATI**

### **Taarifa ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge Kuhusu Uendeshaji Usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania Uliofanywa na Kampuni ya RITES ya India**

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu utendaji usioridhisha wa *TICTS* na *TRL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge, tarehe 10 Februari, 2010, Kamati yangu iliwasilisha taarifa yake kuhusu hoja mbili za Bunge lako Tukufu kuhusu *TICTS* na hoja kuhusu kampuni ya *TRL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TRL* Kamati ilisisitiza Serikali itekeleze hoja ya Bunge ya kuvunja mkataba kati ya *RITES* ya India kwa kuwa utendaji kazi wa kampuni ya *TRL* ni mbaya kiasi kwamba huduma za treni zimekuwa mbaya zaidi kuliko hata kabla ya ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania yaani *TRC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu sababu za kutaka kuvunjwa kwa mkataba wa *TRL*, Kamati ilitoa sababu kumi na tatu za kuhalalisha kuvunjwa kwa mkataba wa *TRL* kwani

mkataba huo umekiukwa na umevunjwa vipengele kadhaa vya mkataba ikiwa ni pamoja na;

Kwanza, kushindwa kulipa *concession fees* pamoja na *variable fees* ya 5% kulingana kifungu cha 18(3)(b)(2a) cha Mkataba, pili, kushindwa kulipa *performance bond* kiasi cha dola za Marekani milioni mbili, tatu, kushindwa kutumia *TRC Civil Engineering Manual 1962* ambayo inaelekeza matumizi ya nguvukazi inayohitajika kutumika katika utengenezaji wa njia ya reli kwa ajili ya usalama na nne, kushindwa kutimiza jukumu lake la msingi la kulipa mishahara ya wafanyakazi wake kulingana na Sheria za nchi na kusababisha Serikali kulipa shilingi 8,753,381,582/= kama nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi wa kampuni ya *TRL* kwa kipindi cha Machi, 2008 hadi Juni, 2009.

Tano, kushindwa kuwalipa washitiri na kulimbikiza madeni makubwa na sasa washitiri hao wanatishia kufungua madai Mahakamani hali inayotishia uwezekano wa *TRL* kuwekwa chini ya mufilisi, sita, kushindwa kumudu kununua mafuta ya kuendesha treni hadi kusababisha treni kusimamisha huduma zake kutokana na kuishiwa mafuta baada ya Washiriti kusitisha zabuni zao kutokana na kutokulipwa malipo wanayodai na saba, uongozi wa *TRL* kuwa na uhusiano mbaya na wafanyakazi kiasi kwamba sasa haukubaliki na hawatakiwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilizingatia kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *RITES* ya India ameeleza kwamba hawapo tayari kuwekeza fedha yoyote katika kampuni ya *TRL* na kwamba wako tayari kuiuzia Serikali ya Tanzania hisa zake za 51%. Aidha, Kamati iliarifiwa kuwa *RITES* walitoa *notice* ya siku 60 na kukusudia kuwaondoa mameneja wa *TRL* ifikape tarehe 31 Januari, 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Kamati ilikutana na Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Dar es Salaam na kupewa taarifa kuwa Serikali sasa imefika mahali pa kukubali kuwa utendaji kazi wa kampuni ya *TRL* ni mbaya kiasi kwamba ni busara kuvunja mkataba kati ya Serikali na *RITES* kwa utaratibu ambao wanaona utafaa na hautasababisha malumbano ya kufikishana Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshafanya uamuzi wa kuachana na *RITES* kwa kuzingatia hoja ya Bunge na ushauri wa Kamati, ni vyema Bunge lako Tukufu lipewe taarifa rasmi leo na Serikali kuhusiana na uamuzi huo uliofanywa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu *TICTS*, taarifa ya Kamati ilisisitiza utekelezaji wa hoja ya Bunge kuwa Serikali isitishie nyongeza ya miaka 15 iliyopewa kampuni ya *TICTS* kwa kuwa nyongeza hiyo ilitolewa kinyume cha utaratibu kwani katika mkataba wa awali kifungu cha 9.1 kiliweka bayana kuwa kifungu cha *the lease period* hakitafanyiwa marekebisho yoyote bila ya kufuata taratibu zinazoonyeshwa katika mkataba huo wa kwanza. (*Makofi*)

Aidha, taarifa ya Kamati ilibainisha kuwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika taarifa yake ya mwaka 2007/2008 alieleza kuwa nyongeza ya miaka 15 waliyopewa *TICTS* haikuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma namba 21 ya mwaka 2004 na hivyo nyongeza hiyo ni batili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kamati ilikubaliana kimsingi na Serikali kwa kufanikiwa kuwaondolea *TICTS* ukiritimba au *exclusivity*.

Mheshimiwa Spika, hapo awali taarifa ya Serikali haikuwa imeeleza sababu za msingi za kushindwa kusitisha nyongeza ya miaka 15 na kwa hali hiyo hivi karibuni Kamati ilipokutana na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu Dr. Shukuru Kawambwa ilimtaka aeleze sababu ambazo zinaifanya Serikali ishindwe kusitisha nyongeza ya miaka 15 jana Bunge lilivyoazimia. Tunatazamia kuwa Serikali katika taarifa yake itakayotoa leo hii italieleza Bunge lake Tukufu sababu hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kujadili suala hili kwa muda mrefu na kubaini kuwa kulikuwa na upungufu kadhaa katika mchakato mzima wa kutoa nyongeza ya miaka 15 kwa *TICTS* na hivyo kusababisha kukiukwa kwa baadhi ya Kanuni na taratibu tulizojiwekea, hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuwa ili kulipatia ufumbuzi suala hili ni vyema Serikali ikakiri kuwepo kwa upungufu kadhaa katika mchakato wa nyongeza ya miaka 15 na kwamba katika siku za usoni Serikali iwe makini zaidi katika ufungaji wa mikataba na ionyeshe mfano katika kuheshimu Sheria, Kanuni na taratibu tulizojiwekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Miundombinu, naomba pia nimshukuru Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Hezekeah Ndahani Chibulunje, Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu Mhandisi Bwana Omar Abdallah Chambo, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi yao nzuri na ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mwenyekiti. Wajumbe wafuatao ndiyo wanaounda Kamati ya ya Miundombinu naomba niwataje kwa majina yao kama ifuatavyo:

Mimi Mheshimiwa Mohamed Missanga ambaye ni Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Gosbert Blande, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu.

Wengine ni Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Alhaji Mtutura Mtutura, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa

Mwaka Abrahaman Ramadhani, Mheshimiwa Prof. Phillemon Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Zambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashillilah, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kulihudumia Bunge ipasavyo. (*Makofi*)

Aidha, naomba niwashukuru makatibu wa Kamati hii Bi. Justina Mwaja Shauri na Bwana Abdallah Hancha kwa kuweza kuhudumia vyema Kamati na kuandaa taarifa ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Miundimbinu naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa upande wa Serikali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu hebu tupe hali halisi ilivyo hadi sasa. Mheshimiwa Naibu Waziri karibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu naomba kuwasilisha taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge juu ya uendeshaji usioridhisha wa Kampuni ya Reli ya Tanzania (*TRL*) kama ilivyofikia mpaka hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja binafsi ya uendeshaji wa Kampuni ya Reli Tanzania unaofanywa na kampuni ya *RITES* ya India iliyowasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, hoja hii iliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliomalizika Dodoma tarehe 25 Aprili, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Azimio la Bunge, Bunge lilijadili hoja binafsi kuhusu uendeshaji usioridhisha wa usafiri wa reli unaoendeshwa na kampuni ya *RITES* na kuazimia kama ifuatavyo ili kuondoa kasoro mbalimbali za uendeshaji katika kampuni hiyo, kuweka uwiano mzuri katika *management* ya Kampuni ili kuleta ufanisi wa Reli ya Kati na kuwapunguzia adha watumiaji wa reli.

Kwanza, kuangalia Mkataba wa Ukodishaji wa Shirika la Reli kwa Kampuni ya *RITES* ili kuondoa dosari zote zilizopo kwa maslahi ya Taifa.

Pili, kwa kuwa Serikali ina hisa 49% na Kampuni ya *RITES* hisa 51% *management* ya Shirika hilo iwe na uwiano sawia kati ya Watanzania na wakodishaji hao. (*Makofi*)

Tatu, kwa kuwa *station* na magenge yamefungwa zichukuliwe hatua madhubuti za kuhakikisha usalama wa reli na vyombo vyake vyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge, hoja ya kwanza ilihusu kuangalia mikataba ya ukodishaji. Serikali iliunda Kamati ya Wataalamu yaani *Diversiter Technical Team* chini ya *Consolidated Holding Cooperation* ili kuangalia dosari zilizopo kwenye Mkataba wa Ukodishaji, Mkataba wa Wanahisa yaani *Memorandum and Articles of Association*. Kamati ilikamilisha kupitia mikataba hiyo na kuainisha maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kamati ya Wataalamu ilibainisha upungufu na kupendekeza maboresho katika mikataba kama ifuatavyo:-

Moja, kuhusu Mkataba wa Ukodishaji yaani *Concession Agreement*. Mpango wa biashara wa kampuni yaani *Business Plan* si sehemu ya mkataba wa sasa kwa hiyo, ilipendekezwa kuwa mpango wa biashara uwe ni sehemu ya mkataba ili kufuatilia utekelezaji wake.

Pili utaratibu wa mkodishaji (*TRL*) kumkodisha mtu mwingine mali iliyokodishwa haikuwekwa bayana kwa hiyo ilipendekezwa kuwa utaratibu bayana wa kufuata endapo mkodishwaji atataka kukodisha mali aliyokodishwa kwa mtu mwingine. Aidha, ilipendekezwa kuwa *RAHCO* ipewe nguvu ya kutoa idhini endapo *TRL* itataka kukodisha mali iliyokodishwa. Tatu, vigezo vya kupima utendaji haviko wazi kwa hiyo ilipendekezwa kuwepo kwa vigezo vya kupima utendaji, aidha, vigezo vya namna ya kukatisha mkataba vinahitaji kuboreshwa. (*Makofi*)

Kuhusu mkataba wa wanahisa yaani *Share Holders Agreement*. Mkataba hauonyeshi utaratibu wa kufuata katika manunuzi ya ndani kwa hiyo hii hutoa mwanya kwa kampuni kufanya manunuzi mahali popote hivyo ilipendekezwa kuwa na kifungu kinachoelezea wazi utaratibu wa manunuzi ya huduma na vifaa ndani ya kampuni. (*Makofi*)

Pili, idadi ya sasa ya Wakurugenzi wa Bodi ni ndogo sana hii inafanya uwakilishi wa Serikali kuwa mdogo. Ilipendekezwa kuongeza idadi ya Wakurugenzi wa Bodi, aidha, uteuzi wa wawakilishi wa Serikali ndani ya *TRL* kuzingatia ujuzi na uzoefu unaotakiwa hususani ujuzi na uzoefu katika masuala ya Reli. (*Makofi*)

Tatu, kuainishwa kwa majukumu ya *management* na yale ya Bodi ya Wakurugenzi na nne, uhitaji wa kuboresha masuala ya haki za wanahisa wa *TRL* ikiwa ni pamoja na suala la mikataba ya misaada ya kiufundi yaani *Technical Assistance* ambayo hayana budi yaamuliwe na Bodi.

Kuhusu mkataba wa kuanzisha kampuni yaani *Memorandum and Article of Association* ya *TRL* ilibainika kwamba Mwenyekiti wa sasa wa Bodi ya Wakurugenzi anatoka kampuni ya *RITES* na hachaguliwi na wanahisa wote wala Bodi ya Wakurugenzi. Kwa upungufu huo ilipendekezwa kuongeza idadi ya Wakurugenzi wa Bodi na haki ya wanahisa kuchagua na kumpata Mwenyekiti wa Bodi. Pia utaratibu wa sasa wa kuweka *management* ya kampuni hauko wazi na wala hauwahusishi wanahisa.

Kwa hiyo, ilipendekezwa *MEMATS* kuweka bayana kuhusu suala la kuwa na mkataba wa *management* na uhusishe wanahisa wote. (*Makofi*)

Tano, kwenye Bodi ya sasa hakuna kipengele kinachosema idadi ya wawakilishi wa kila mwanahisa inayotakiwa kuwepo ili kutumiza *quorum*. Hii inatoa mwanya kwa kikao cha Bodi kukaa kikiwa na Wakurugenzi wa mwanahisa mmoja tu, hivyo ilipendekezwa kuwa pawekewe bayana na *quorum* inayohitajika kuwepo kwa wawakilishi wa kila mwanahisa. (*Makofi*)

Tano, Bodi ya sasa ya Wakurugenzi ndiyo inayomteua Mkaguzi wa Hesabu za Kampuni. Utaratibu huu unaipa mwanya zaidi *RITES* kuteua mkaguzi na siyo wanahisa wote. Kwa hiyo, ilipendekezwa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa hayo yote mmekwishapita sasa Serikali tunaambiwa imevunja mkataba, hebu tuchukue kuanzia hapo kwani historia hiyo tunaifahamu sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba basi niende moja kwa moja kwenye hali halisi ya *TRL* na mpango wa Serikali. (*Makofi*)

Katika kikao cha mwisho cha wanahisa kilichofanyika tarehe 17 Novemba, wanahisa walikiri kwamba *TRL* inakabiliwa na matatizo matatu kimsingi kama ifuatavyo:-

Moja, hali mbaya ya fedha kiasi cha kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi, kukarabati miundombinu na kutoa huduma kwa ufanisi; pili, uhusiano mbaya kati ya *management* na wafanyakazi ambao ulisababisha wafanyakazi kugoma mara kwa mara na tatu, wafanyakazi kugoma kutumia injini na mabehewa yaliyokodishwa kutoka *RITES*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo hayo wanahisa walikubaliana kwamba suluhisho ni kwa kampuni ya *RITES* kujiengua kutoka *TRL*, hivyo *RITES* iliwasilisha mapendekezo ya kuuza hisa zake 51% ndani ya *TRL*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapendekezo ya kikao hicho cha wanahisa, Wizara iliandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri na kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya *RITES* kujiengua ndani ya *TRL* na Serikali ya Tanzania kuchukua hisa zote za kampuni hiyo, pamoja na kwamba majadiliano baina ya Serikali na kampuni ya *RITES* yamechukua muda mrefu takribani miezi kumi na saba, Serikali kwa kipindi chote hicho imeendelea kuchukua hatua madhubuti kutekeleza maazimio ya Bunge baada ya kujadili wasilisho la Wizara ya Miundombinu, Baraza la Mawaziri limefanya maamuzi yafuatavyo:-

Kwanza, Serikali kununua hisa zote za *RITES* kiasi cha 51% ndani ya *RITES* na hivyo kuondoa *management* ya *RITES* ndani ya *TRL*.

Pili, kutoa ridhaa kwa Serikali kujadiliana na *RITES* ili kukubaliana bei ya hisa zao katika *TRL*, na tatu, Serikali kuendesha Shirika la Reli kwa kipindi cha mpito mpaka mwendeshaji au mwekezaji mwingine atakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kununua hisa zote za *RITES* ndani ya *TRL* Serikali itachukua jukumu la kuendesha *TRL* kwa muda wakati akitafutwa mwendeshaji au mwekezaji mwingine. Hata hivyo kabla ya kumtafuta mwekezaji mpya wa *TRL* Serikali itafanya tathmini ya upungufu uliojitokeza katika mkataba huo hususani mambo yaliyosababisha ubia uvunjike. Hatua hii itasaidia kutengeneza mkataba mzuri yaani *appropriate concession model* na kuepusha matatizo kwenye mikataba ya baadaye. *(Makofi)*

Aidha, Serikali itafanya tathmini ya hisa za *RITES* ndani ya *TRL* kabla ya kukamilisha ununuzi wa hisa zote.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha zoezi la ununuzi wa hisa za *RITES* Serikali iko kwenye hatua za mwisho sasa za kumteua kwa ushindani mtaalamu mshauri yaani *consultant* atakayefanya tathmini ya *TRL* ili kupata thamani halisi ya hisa za *RITES*, tathmini hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei. *(Makofi)*

Aidha, Serikali inakamilisha zoezi la kumteua Mkaguzi wa Mahesabu ambaye atakagua mahesabu *TRL*. Ripoti ya Mkaguzi itatoa hali halisi ya mahesabu ya Kampuni na itasaidia kuthibitisha madai yaliyowasilishwa na *RITES* kuhusu huduma walizozitoa kwenye Kampuni ya *TRL*. Wakati tunasubiri ripoti hizi mbili, Serikali imeshafanya mawasiliano na Mheshimiwa Rais ili majadiliano ya wanahisa yaanze mapema iwezekanavyo, majadiliano ya awali yamepangwa kufanyika mapema mwezi Mei, 2010. *(Makofi)*

Baada ya majadiliano ya wanahisa kukamilika mkataba kati ya Serikali na *RITES* utafutwa na hivyo Serikali itamiliki Kampuni ya *TRL* kwa asilimia mia moja mpaka hapo atakapopatikana mwendeshaji au mwekezaji mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, pamoja na kushughulikia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, Serikali imeendelea kushughulikia changamoto ya kurudisha miundombinu ya reli ambayo ilisombwa na mafuriko yaliyotokea mwezi Desemba, 2009 na Januari, 2010 katika Wilaya za Kilosa na Mpwapwa. Kufuatia kusitishwa kwa huduma za reli baada ya mafuriko hayo Serikali imeazimia kufanya yafuatayo:

Kwanza, itaendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi wa *TRL* kwa sababu *TRL* kwa sasa haina fedha. Pili, itatoa fedha za uendeshaji wa huduma za treni za abiria na mizigo kuanzia Dodoma kwenda Kigoma na Mwanza kwa kuwa Kampuni haina fedha kwa sasa. Serikali pia itaendelea kufanya matengenezo ya maeneo yaliyoathirika na mafuriko hadi huduma zitakaporejea kuanzia Dar es Salaam. *(Makofi)*

Aidha, ili mtandao wa reli uliopo nchini uwe na manufaa na tija kubwa zaidi kwa uchumi wa nchi, Wizara ya Miundombinu inafanya uchambuzi wa kina kuhusu mahitaji ya huduma na miundombinu ya reli ili kuwa na uhakika wa raslimali katika kuboresha mtandao wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Umeomba kuwasilisha tu. Kwa sababu wewe sio mtoa hoja, mtoa hoja ni Mwenyekiti. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa namwita Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu atusomee hali halisi sasa ya *TICTS* hakuna haja ya historia kwa sababu tunajua. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nitazingatia yale uliyozungumza kwamba baadhi maneno nitayaruka kwa vile yanaeleweka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja binafsi kuhusu utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *TICTS* iliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliomalizika Dodoma tarehe 25 Aprili, 2008. Hoja hiyo iliwasilishwa na Mheshimiwa Godfrey Zambzi, Mbunge wa Mbozi Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Azimio la Bunge, Bunge lilijadili hoja binafsi kuhusu utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *TICTS* na kuazimia kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali isitishe nyongeza ya mkataba na kufanya mapitio ya mkataba wa awali ili vifungu vya mkataba huo ambavyo havina manufaa kwa Taifa virekebishwe na pili, ni kwamba baada ya muda wa mkataba wa awali wa miaka 10 kumalizika nyongeza yoyote ya mkataba mwingine mpya uzingatie Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge, baada ya kutoa maelezo ya jumla naomba sasa nitoe Taarifa ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kama ilivyoazimiwa na Bunge tarehe 25 Aprili, 2008 katika Mkutano Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Machi, 2008 Serikali iliunda Kamati ya Serikali ya majadiliano ili kupitia Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha. Lengo lilikuwa ni kubaini maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho kwa maslahi ya Taifa. Kamati hiyo ilihusisha Wizara na Taasisi zifuatazo; Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Wizara ya Fedha na Uchumi,



Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania na *CHC*. Serikali iliunda pia Kamati ya Mawaziri kuendeleza majadiliano na *TICTS*. Kamati hiyo ilijumuisha Waziri wa Miundombinu akiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha na Uchumi, Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kimsingi Azimio la Bunge liliipa msukumo mpya kazi ambayo tayari ilikwishaanza kutekelezwa na Kamati iliyoundwa na Serikali.

Majukumu ya Kamati hiyo yalikuwa ni kuangalia upya Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha ili uwe wa manufaa zaidi kwa pande zote mbili na pia uweze kuzingatia mahitaji ya kuwepo kwa vifungu vinavyomtaka Mkodishaji awajibike kuwekeza katika kuendeleza utoaji wa huduma ya makasha. Mambo muhimu yaliyobainishwa katika Azimio ya Bunge yalishaanza kushughulikiwa na Serikali kabla ya hoja binafsi juu ya *TICTS* kuletwa Bungeni. Wakati wa majadiliano kati ya Serikali na *TICTS* kimsingi suala la muda wa ukodishaji na umuhimu wa kurekebisha vipengele vya mkataba ili kuboresha na kufanya wenye tija kwa Taifa vilizingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya upande wa Serikali kufanya mapitio ya mkataba ilibainishwa kuwepo kwa vipengele vya mkataba vilivyosababisha kushuka kwa utendaji na vipengele visivyokuwa na maslahi kwa Taifa hivyo kutakiwa kurekebisha au kufutwa. Baada ya kupitia vipengele vya mkataba, Kamati ya Serikali ya Majadiliano ilikutana na wawakilishi wa *TICTS* na kufanya majadiliano na kutoa mapendekezo yafuatayo ambayo nimeyaorodhesha katika taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika masuala yaliyojadiliwa vipengele vifuatavyo vilikubaliwa na pande zote mbili. Moja kuondoa kipengele kinachoipa *TICTS* ukiritimba wa kuhudumia meli za makasha katika bandari ya Dar es Salaam. Pili, kuongeza vigezo vya kupima utendaji ambavyo ni kupima ufanisi wa matumizi ya *yard* na pili kupima ufanisi wa matumizi wa mitambo inayotumika kuhudumia makasha katika *yard*. (*Makofi*)

Tatu, *TICTS* kutayarisha na kuwasilisha mpango wa uwekezaji wa miaka mitano, mitano kwa kipindi cha Januari, 2009 mpaka 2013; Januari, 2014 mpaka mwaka 2018 na wa miaka saba kuanzia 2019 hadi mwaka 2025. (*Makofi*)

Nne, *TICTS* kurudisha vifaa vilivyokwisha muda wake wa matumizi kwa *TPA* na kulipa fidia kwa vifaa vilivyonyofolewa vipuri. Tano, kurekebisha utaratibu wa kukusanya tozo ya kutumia miundombinu ya bandari ili *TPA* wakusanye tozo hiyo kila siku wenyewe badala ya utaratibu wa *TICTS* kukusanya tozo hiyo na kuwasilisha *TPA* kila mwisho wa mwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matokeo ya majadiliano kati ya Serikali na *TICTS* ni kwamba mnamo tarehe 5 Oktoba, 2009 Serikali na *TICTS* walisaini nyongeza namba 3 ya Mkataba na Hati ya Maelewano ya Utekelezaji wa masuala yaliyokubaliwa na pande zote mbili. Miongoni mwa vipengele ambavyo havikupata muafaka kwa pande zote mbili,

moja ni kusitisha nyongeza ya muda wa ukodishaji na namba mbili kuongeza viwango vya malipo ya pango na mrahaba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha ulitiwa saina tarehe 5 Mei, 2000. Mkataba huu ulikuwa wa miaka 10 na hivyo ulitegemewa kwisha mwaka 2010. Mwaka 2005 wakati Mkataba wa Kukodisha Kitengo cha Makasha unafanyiwa marekebisho na kuongeza kipindi cha muda wa miaka 15 zaidi muda wa Mkataba wa Ukodishaji ulikuwa haujamalizika na hivyo isingewezekana kutangaza upya ili kuruhusu ushindani kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 21 ya mwaka 2004.

Zaidi ya hilo utaratibu uliotumika mwaka 2000 kubinafsisha Kitengo cha Kuhudumia Makasha ni ule wa *PSRC* ama Mamlaka ya Kurekebisha Mashirika ya Umma. *PSRC* ilikuwa na utaratibu wake maalum wa ubinafsishaji wa Mashirika na vitengo ambao ulikubaliwa baina ya Serikali na Benki ya Dunia ambayo ilifadhili mradi mzima wa urekebishaji wa Mashirika ya Umma. Mchakato huu ulihusisha Mtaalam Mshauri, Kamati ya Wataalam, Kamati ya Makatibu Wakuu, Bodi ya *PSRC* na hatimaye Wizara yenye dhamana ambayo hutayarisha Waraka wa Baraza la Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 lilipohitajika kufanya marekebisho katika vipengele vya Mkataba, Serikali ilielekeza utaratibu na mchakato wa *PSRC* ufuatwe kwa kuzingatia kuwa muda wa Mkataba ulikuwa haujamalizika na kwa kuwa ni *PSRC* ndiyo iliyoingia Mkataba kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya nyongeza ya muda wa ukodishaji wa miaka 15 yalizingatia pia kifungu cha 9.1 cha Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha. Pamoja na kwamba kifungu namba 9.1 cha mkataba kinakataza muda wa mkataba kurekebishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mikataba ama *The Law of Contract Act Cap. 345*, Mkataba au kifungu chochote cha Mkataba kinaweza kurekebishwa wakati wowote endapo kama kuna maridhiano ya pande mbili. Wakati wa majadiliano ya hoja ya upande wa Serikali kuhusu kusitisha ama kufuta nyongeza ya muda wa ukodishaji wawakilishi wa *TICTS* walieleza kwamba *TICTS* hawako tayari kufutwa kuondolewa kwa nyongeza ya muda wa ukodishaji kwa kuwa nyongeza hiyo ni maridhiano ya pande zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kushindwa kwa Kamati ya Majadiliano ya Serikali, kuondosha nyongeza ya muda wa Mkataba iliyopewa *TICTS* iliwasilishwa Serikalini kwa njia ya Waraka wa Baraza la Mawaziri. Pendekezo la Waraka lilikuwa Serikali ivunje mkataba na *TICTS*, Baraza lilitafakari suala hili na kubaini kuwa nyongeza hiyo ya kipindi cha mkataba ni halali kwa mujibu wa Sheria za Mikataba na iwapo Serikali ingetumia nguvu kuvunja au kusitisha nyongeza ya muda wa ukodishaji na suala hili likafikishwa kwa msuluhishi, Serikali ingeweza kupata hasara ya kuilipa *TICTS* fidia iliyokadiriwa kuwa shilingi bilioni 645. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuweza kuihakikishia Serikali ushindi katika kesi hii. (*Makofi*)

Aidha, *TICTS* ingeweza kwenda Mahakamani na kuweka pingamizi ambalo lingeweza kusimamisha huduma za bandari kwa muda usiojulikana na hivyo kuathiri na kuleta na hasara kiuchumi na kuharibu sifa ya nchi yetu, huo ndio ugumu uliojitokeza. Katika juhudi za Serikali kutekeleza Azimio la Bunge la Kusitisha Nyongeza ya muda wa Mkataba. Kufuatana na hali hiyo Serikali haikuona busara kuchukua uamuzi wa kuvunja mkataba na *TICTS* jambo ambalo lingeweza kuingiza nchi katika hasara kubwa. Badala yake Serikali ikafanya maamuzi ya kufanya juhudi ya kuondoa kipengele cha ukiritimba wa kuhudumia meli za makasha katika Bandari ya Dar es Salaam. Kuhusu nyongeza ya viwango vya mrahaba, pande zote mbili ziliridhia kwamba marejeo yafanyike mwaka 2010 kama ilivyobainishwa katika nyongeza ya pili ya mkataba (*addendum* namba 2). Kwa sasa Serikali kupitia *TPA* inafanya maandalizi ya kufanya majadiliano na *TICTS* kuhusu marejeo ya viwango vya mrahaba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi ya pango ambapo kigezo kilichotumika kukadiria viwango vya pango ni ukubwa wa eneo tengefu na vifaa vya *TPA* vilivyokodishwa kwa *TICTS*. Hoja hii ilikosa nguvu kwa kuwa Serikali haina mpango wa kuongeza mpango wa ukubwa wa eneo tengefu na kuipa *TICTS* vifaa vya nyongeza. Serikali ilizingatia kwamba mapato ya Serikali ama mrahaba yataongezeka kulingana na kukua kwa biashara inayopita kwenye Kitengo cha Makasha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua zilizochukuliwa kuongeza ufanisi, wakati majadiliano na *TICTS* yakiendelea Serikali iliunda Kamati ya Wadau wa Bandari ya kuongeza ufanisi wa utendaji katika Bandari ya Dar es Salaam Wajumbe wa Kamati hiyo walijumuishwa kutoka Wizara ya Miundombinu, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato (*TRA*), Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*), Kitengo cha Kuhudumia Makasha (*TICTS*), Chama cha Wapokea na Wapeleka Shehena (*TAFa*), Chama cha Wamiliki wa Magari ya Mizigo (*TATOA*), Waendeshaji wa Huduma za Reli ya Kati (*TRL*), Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (*TAZARA*), Chama cha Wakala wa Meli (*TASA*), Kitengo cha Ukaguzi wa Mizigo Bandarini (*TISCAN*) na Chama cha Wamiliki wa Vituo vya Kuhifadhi Mizigo (*ICDs*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Wadau ilibaini kuwa pamoja na matatizo yaliyomo katika mkataba wa *TICTS* yapo matatizo 10 ya msingi yanayozorotesha ufanisi na utendaji katika bandari ambayo yanasababishwa na wadau wengine wa bandari. Matatizo yaliyobainishwa na Kamati ya Wadau na kutakiwa kuyatafutia ufumbuzi wake ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni kuongeza ufanisi wa kushughulikia kadhia ya forodha ambalo ni jukumu la *TRA*, pili, upatikanaji wa haraka wa taarifa za malipo ya wateja ambalo ni jukumu la *TRA* na tatu, upokeaji wa haraka wa taarifa za mizigo katika meli, jukumu la *TRA*. Nne, kuweka tozo zenye kuwafanya wenye mizigo wasitumie bandari kama ghala la kuhifadhi mizigo, jukumu la *SUMATRA*, tano, kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi ndani na nje ya bandari ambalo ni jukumu la Wizara ya Miundombinu; na sita, kuelimisha na kuhamasisha wadau kuhusu uaminifu na uharaka wa kushughulikia utoaji mizigo bandarini ambalo ni jukumu la *TPA*.

Saba, kuimarisha taaluma ya fani ya kutoa na kusafirisha mizigo ambalo ni jukumu la Chama cha Wapokea na Wapeleka Shehena; nane, kuimarisha barabara ndani ya bandari ambalo ni jukumu la Wizara ya Miundombinu; tisa, utoaji wa haraka wa mizigo bandarini ambalo ni jukumu la TPA na TICTS; na kumi, utoaji wa haraka wa taarifa za mizigo melini ambalo ni jukumu la Chama cha Wakala wa Meli (TASA).

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali za kuwashirikisha wadau katika kuboresha huduma za Bandari zimeleta mafanikio yafuatayo:-

Kwanza, kusajili na kutumia vituo vya kuhifadhi makasha ama *inland container depot (ICDs)*. Hadi sasa vituo vya kuhifadhi makasha nje ya bandari viko 10 na vina uwezo wa kuhifadhi makasha 9,000 na vinafanya kazi; pili, muda wa makasha kukaa bandarini ama *dual time* umepungua kutoka wastani wa siku 20, tarehe 26 Januari 2009 hadi kufikia siku 12 mwezi Februari 2010; tatu, muda wa meli za makasha kusubiri nje ya lango la bandari umepungua kutoka wastani wa siku 25 tarehe 26 Januari 2009 mpaka kufikia siku 3 na nusu mwezi Februari 2010; na nne, kuongeza maeneo ya kuhudumia makasha ndani ya bandari kwa sasa TICTS ina uwezo wa kuweka makasha 11 TUs badala ya TU 7,500 za awali. (Makofi)

Tano, kupunguza mlolongo wa kushughulikia kadhia za forodha, mfumo wa SCUDA ++ umeboreshwa ambapo kwa sasa unaruhusu wateja kutuma nyaraka za mizigo kwa njia ya mtandao. Awali muda wa kushughulikia nyaraka za mizigo ulikuwa siku 9 na sasa ni siku 2 au masaa 48. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zilizotajwa hapo juu Serikali inaendelea na mipango madhubuti ya kuboresha usafiri wa reli na barabara kuu zierendazo nchi jirani kwa lengo la kuongeza kasi ya uondoshaji wa makasha katika bandari ya Dar es Salaam. Kwa kushirikiana na nchi za Rwanda na Burundi, Serikali inaendelea kusimamia mpango wa kubadili reli ya Dar es Salaam hadi Isaka iwe kwa kiwango cha *standard gauge* na kujenga reli mpya kutoka Isaka hadi Kigali na Keza nchini Tanzania hadi Msongati nchini Burundi kwa kiwango cha *standard gauge*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua ya awali ya upembuzi yakinifu imekamili na Serikali zetu zimejipanga kwa hatua zinafuata. Kwa upande mwingine Serikali inaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA). Katika kutekeleza mkakati wa kuvutia wawekezaji shindani watakaowekeza katika shughuli za kuhudumia makasha na shehena nyingine katika Bandari ya Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Hali ya sasa ya utendaji katika bandari ya Dar es Salaam inaridhisha ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwezi Januari 2009. Serikali imeendelea kufanya jitihada za kuboresha utendaji katika bandari ya Dar es Salaam kwa kushirikisha wadau wote wa bandari na jambo hili ni muhimu na ndio kiini cha mafanikio yaliyopatikana ushirikishwaji wa wadau wote wa bandari nzima. Matunda ya juhudi hizi za Serikali kwa kushirikiana na wadau yameanza kuonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuiondolea *TICTS* ukiritimba wa kuhudumia meli za Makasha, Serikali kupitia *TPA* imeanza kutekeleza mpango wa kuboresha miundombinu ya bandari kwa kujenga ghati mbili mpya na kuboresha zilizopo ili kuongeza uwezo wa kuhudumia meli kubwa, miradi hii itatekelezwa kushirikisha wawekezaji kutoka sekta binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kutekeleza Maazimio ya Bunge, maoni ya Waheshimiwa Wabunge yamechukuliwa na kufanyiwa kazi kwa umakini unaostahili kwa ngazi zote za Serikali na Mamlaka ya usimamizi wa Bandari Tanzania. Jambo kubwa lililozingatiwa katika mchakato huu ni kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wa bandari na hivyo kuchangia ongezeko la uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba kuna mapungufu yamejitokeza katika baadhi ya vipengele vya Mkataba wa ukodishaji wa Kitengo cha kuhudumia makasha katika Bandari ya Dar es Salaam. Huu ndiyo msingi wa Serikali kuingia kwenye majadiliano na *TICTS*. (*Makofi*)

Baada ya mchakato huu Serikali itazingatia somo lililopatikana katika zoezi la ukodishaji wa kitengo cha makasha Bandarini na Serikali itajitahidi kuepukana na kasoro kama hizo katika mikataba ambayo itaingia. Napenda pia kusesitiza kuwa Serikali itaendelea kuwa makini zaidi katika kusimamia uendeshaji wa bandari ili kutimiza lengo lilikusidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge nimetafakari jambo hili la Mashirika hayo mawili, *TRA* na *TICTS* na nimeona hakuna faida yoyote ya kuendeleza mjadala juu ya mambo hayo. Kwa hiyo, kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 116 inayosomeka hivi: “Spika anaweza kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yoyote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kushughulikiwa na Kamati hiyo.” (*Makofi*)

Kwa hiyo, nimeona badala ya Bunge zima kujihangaisha na masuala ya *RITES* na *TRL* na *TICTS* nakabidhi sasa kwa niaba yenu kwa Kamati ya Miundombinu ifuatilie kwa karibu sana utekelezaji wa Serikali katika masuala haya na tuweze kupata taarifa. Vinginevyo tutaendelea na mjadala ambao nadhani Serikali imejitahidi, imefika pahala ambapo mathalani kwenye Mkataba wa *TICTS* ni dhahiri sio mzuri na taabu ya mikataba hii ni kwamba mkiingia Mahakamani athari inaturudia na wananchi na walipakodi ndiyo wanakuja kuathirika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tuyaache hapo lakini tutegemee kwamba Serikali itaendelea kuboresha mambo haya na huduma za Reli ya Kati nazo ziweze kurejea salama na Kamati ya Miundombinu itakuwa ikitupa taarifa wakati hadi wakati. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi Kiongozi wa Kambi ya Upinzani alihoji maamuzi niliyoyatoa wakati hati zimewasilishwa mezani nilisema kwamba hakuna

aliyesimama kutaka kuomba taarifa yoyote ijadiliwe kwa hiyo tunaendelea. Kutokana na maelezo yangu hayo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani alitumia Kanuni ya 68 kuniomba Muongozo na akaenda ndani kwa kutumia Kanuni ya 37(7) inayosemwa taarifa zitakazowasilishwa Bungeni na Kamati ya Kudumu na kadhalika zitatengewa muda wa kujadiliwa bila hoja kutolewa na akaomba muongozo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ufafanuzi wa kitaalam ni kuwa kujadiliwa kwa taarifa yoyote iliyowasilishwa Bungeni kwa kuwekwa mezani ikiwa ni pamoja na taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge kunatawaliwa na utaratibu mrefu uliowekwa katika Kanuni ya 37. *(Makofi)*

Kanuni ya 114(15) imeweka sharti la jumla tu la ulazima kwa kila Kamati ya Kudumu kuwasilisha Bungeni taarifa za mwaka. Hata hivyo suala la kujadiliwa kwa taarifa hizo sio moja kwa moja yaani si *automatic* kwamba zikishawasilishwa au kuwekwa mezani basi zitajadiliwa tu pasipo kuzingatia masharti mengine, hapana. Suala la kujadiliwa limewekwa masharti katika fasili ya nne na ya sita ya Kanuni hiyo ya 37 ambayo Kiongozi wa Upinzani hakuzingatia. *(Makofi)*

Ufafanuzi wa masharti hayo ni kwamba kwa mujibu wa fasili ya nne ya Kanuni ya 37 inasema baada ya hati kuwasilishwa Bungeni, iwe ya Waziri, Mwanasheria Mkuu au Mbunge, Mbunge atatakiwa kutoa hoja kwamba Bunge lijadili hati hiyo na hoja hiyo itabidi niwahoji ili muikubali au kuikataa. Hoja hiyo mkiikubali ndiyo itashughulikiwa kwa kufuata mpangilio wa shughuli za Bunge. Aidha, fasili ya 16 ya Kanuni ya 114 pia inaeleza kwamba taarifa ya Kamati inapowasilishwa Bungeni itashughulikiwa kwa kufuata mpangilio wa Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kilichotokea kuhusiana na taarifa za Kamati zilizowalishwa Bungeni asubuhi ya leo ni kwamba masharti hayo ya fasili ya nne hayakuzingatiwa. Kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Kanuni hiyo fasili ya nne ilibidi hoja ya kutaka taarifa hizo zijadiliwe itolewe halafu ifuatiwe na kukubaliwa kwa mujibu wa fasili ya sita na ndipo taarifa hizo zitengewe muda wa kujadiliwa Bungeni kwa mujibu wa fasili ya saba aliyonukuu Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Kwa sababu masharti ya fasili ya nne ya Kanuni ya 37 hayakuzingatiwa ndiyo maana nilieleza tena kwa usahihi kabisa kwamba kwa kuwa hakuna Mbunge aliyesimama kuomba taarifa yoyote kati ya zilizowasilishwa zijadiliwe basi taarifa hizo haziwezi kujadiliwa. *(Makofi)*

Kwa kuzingatia ufafanuzi huo Muongozo wangu sasa kwa Bunge ni kwamba maelezo niliyoyatoa asubuhi kuhusiana na taarifa za Kamati zinazowasilishwa Bungeni ni sahihi pasipo mashaka yoyote na hakuna mgongano wowote wa maelezo yangu na fasili ya saba ya Kanuni ya 37. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi huu nimeutoa leo Ijumaa, tarehe 23 Aprili, mwaka 2010. Ahsanteni. *(Makofi)*

Sasa kwa mujibu wa shughuli zetu hapa tunaendelea na hatua moja ya mwisho ambayo nitaomba Katibu ututajie.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limemaliza shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano wa Kumi na Tisa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Baada ya tangazo hilo kwa heshima na taadhima sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili aweze sasa kutoa hoja ya kuliahirisha Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. (*Makofi*)

### **KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kumaliza shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tangu Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge, nchi yetu imeendelea kukumbwa na majanga mbalimbali yakiwemo mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile kumekuwepo na ajali ya kufukiwa na kifusi cha udongo katika Mgodhi ulioko Wilayani Geita, Mkoani Mwanza iliyotokea tarehe 12 Aprili, 2010. Katika ajali hiyo watu nane walifariki na wengine kujeruhiwa.

Aidha, majanga mengine ni ajali za majini ambapo watu walikufa maji na pia wapo wengi waliopoteza maisha kwa ajali za barabarani. Napenda kuwapa pole waliopoteza ndugu zao katika ajali hizi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahala pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge, jumla ya Maswali 118 ya Msingi na 249 ya Nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Wizara husika. Aidha, Utaratibu wa Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kila Alhamisi uliendelea kwa Waheshimiwa Wabunge kuuliza na kujibiwa maswali yao. Jumla ya Maswali 18 ya Msingi na matano ya Nyongeza yaliulizwa na kujibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya Miswada sita imesomwa na kupitia hatua zake zote. Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wa mwaka 2010 (*The Persons with Disabilities Bill, 2010*); Muswada wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo wa mwaka 2010 (*The Livestock Identification, Registration and Traceability System Bill, 2010*); Muswada wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo wa mwaka 2010 (*The Grazing-Land and Animal Feed Resources Bill, 2010*); Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana wa mwaka 2010 (*The Capital Markets and Securities (Amendments) Bill, 2010*); Muswada wa Sheria ya Madini wa Mwaka 2010

(*The Mining Bill, 2010*); na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2010 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2010*).

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilijadili na kupitisha Maazimio mawili ambayo ni Azimio la Kuongeza Mtaji wa Mfuko wa Dhamana (*Advance Fund*) na Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, pia Bunge lako Tukufu lilipokea na kujadili Taarifa za Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kama ifuatavyo ; Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*Local Authorities Accounts Committee - LAAC*); Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (*Public Accounts Committee – PAC*); na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Mashirika ya Umma (*Parastatal Organisation Accounts Committee – POAC*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli ya Waziri wa Habari na Utamaduni na Michezo kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shughuli rasmi za Serikali na Kauli ya Waziri wa Miundombinu kuhusu uharibifu wa Miundombinu ya Barabara na Reli nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kujadili na kupitisha Miswada, Maazimio na Taarifa za Kamati mbalimbali zilizowasilishwa hapa Bungeni. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri mlioutoa ambao utasaidia katika utekelezaji wa Sheria na Maazimio yaliyopitishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali za kutoa msukumo katika kilimo na pia kukabiliana na changamoto zake, tarehe 17 na 18 Machi 2010 ulifanyika Mkutano wa pamoja wa watafiti wa sekta ya kilimo, kwa maana ya utafiti wa mazao, mifugo na uvuvi, jijini Dar es Salaam. Mkutano huu, ulilenga katika kupata taarifa za hali ya tafiti zinazoendelea kwenye vituo mbalimbali hapa nchini pamoja na changamoto zinazowakabili watafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huo, watafiti walipata fursa ya kueleza namna wanavyofanya kazi zao pamoja na mafanikio ya ugunduzi wa teknolojia zinazosaidia katika kuendeleza sekta ya kilimo. Hii ikiwa ni pamoja na ugunduzi wa mbegu bora, urutubishaji udongo, pembejeo, kilimo cha umwagiliaji na ushauri wa kitaalam kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mkutano huu wa watafiti pia ulijadili na kuainisha changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utendaji wa kazi kwenye vituo vya utafiti. Changamoto hizi ni pamoja na ufinyu wa Bajeti ya utafiti; upungufu wa wataalam na maslahi duni ya watafiti; ukosefu wa miundombinu na vitendea kazi kwa watafiti. Hii ni pamoja na ukosefu wa maabara za kisasa, ofisi, nyumba za kuishi watafiti pamoja na maghala ya kutunzia bidhaa, ukosefu wa zana za kilimo na pembejeo za kufanyia kazi, hususan matrekta, magari, pikipiki na baiskeli, usambazaji hafifu wa teknolojia zinazogunduliwa na watafiti. Hii imesababisha mawasiliano duni kati ya mtafiti, mgani



na mkulima na kusababisha teknolojia zinazogunduliwa kutowafikia walengwa na vituo vya utafiti kutokuwa na hati za kumiliki ardhi. Hivi sasa maeneo mengi ya vituo vya utafiti yamevamiwa na watumiaji wengine wa ardhi hasa kutokana na ukweli kuwa vituo vya Serikali havijapimwa na hii inatokea hasa kwenye maeneo ya vituo vilivyo karibu na miji inayoendelea kupanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa na watafiti, Serikali itachukua hatua zifuatazo; Bajeti ya Utafiti itaongezwa kuanzia mwaka ujao wa fedha kwa lengo la kufika/kukaribia asilimia moja ya Pato la Taifa; Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia zitashirikiana na Wizara na sekta nyingine zinazohusika na watafiti ili kuangalia Sheria, Taratibu na Kanuni zitakazoweza kuimarisha shughuli za utafiti nchini pamoja na kutoa mapendekezo yatakayoweza matokeo ya utafiti kuwafikia walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kutokana na majadiliano ya Mkutano huu tulikubaliana kuwa muundo wa utafiti na maslahi ya watafiti yaboreshwe suala ambalo sasa linafanyiwa kazi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta zinazohusika na watafiti. Aidha, Serikali imeainisha idadi halisi ya watafiti nchini ili kuwezesha kuwapanga vizuri katika muundo mpya unaoandaliwa. Vilevile, wadau walikubaliana kukamilisha mapema maandalizi ya sera ya maendeleo ya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ni kiungo muhimu kwa sekta nyingine kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Hivyo, hatuwezi kupunguza kiwango cha umaskini uliopo bila kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo hapa nchini hasa kuongeza uzalishaji. Uchambuzi wa kitaalam unathibitisha kuwa ukuaji wa uchumi unaotokana na ukuaji wa kilimo unachangia karibuni mara mbili zaidi katika kupunguza umaskini kuliko unaochangiwa na sekta nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufikia malengo ya maendeleo ya sekta ya kilimo, tunahitaji kuwekeza zaidi ili kuongeza kukua kwa sekta na kufikia angalau asilimia 10 kutoka asilimia 4 ya ukuaji wa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuongeza rasilimali katika sekta ya kilimo. Kwa mantiki hiyo na ili kufanikisha utekelezaji wa azma ya kuleta mapinduzi ya kilimo nchini katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali inatarajia kuweka kipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuongeza upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo (mbolea, mbegu bora na dawa); pili, kuongeza kasi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; tatu, kuimarisha mashamba ya uzalishaji mbegu bora na mitamba; nne, kuviwezesha vituo vya utafiti, kupata teknolojia sahihi na tano, kuimarisha upatikanaji wa dawa ili kudhibiti visumbufu vya mimea na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sita, kuimarisha mafunzo kwa maafisa ugani; saba, kuongeza fedha za mfuko wa pembejeo za kilimo; nane, kuongeza upatikanaji wa zana za kilimo

(matrekta, plau na majembe); tisa, kuimarisha masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi; kumi, kuimarisha na kuendeleza vyama vya ushirika na kumi na moja, kuimarisha miundombinu ya sekta ya mifugo uvuvi. *(Makofi)*

Kumi na mbili, kupima na kutenga maeneo ya kilimo na ufugaji ili kurahisisha uwekezaji, kumi na atatu, kujenga na kuimarisha viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na kilimo, mifugo na uvuvi ili kuongeza thamani ya mazao yetu na hivyo kukuza uchumi wa taifa letu; na kumi na nne, kuimarisha miundombinu ya barabara, reli na bandari ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ni muhimu kama tunataka kupiga hatua katika kuleta mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Spika, usalama wa chakula nchini unategemea sana mtandao mzuri wa barabara unaopitika kwa urahisi wakati wote kuanzia ngazi ya kijiji hadi barabara kuu. Hii ni kutokana na ukubwa wa nchi yetu na kutofautiana kwa uzalishaji wa aina ya mazao kutoka sehemu moja ya nchi hadi sehemu nyingine.

Vilevile tofauti ya mtawanyiko wa mvua kimkoa inayosababisha kutofautiana kwa uzalishaji wa mazao na pia kuwepo kwa maeneo yenye chakula cha ziada na maeneo mengine kutokuwa na chakula. Kwa mantiki hiyo, mtandao wa barabara ni muhimu katika kusafirisha chakula kutoka maeneo yenye ziada ya chakula na kupelekwa sehemu yenye upungufu wa chakula. Hivyo, mpango wa kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini hauna budi kwenda sambamba na uboreshaji wa mtandao wa barabara zote nchini. Maboresho ya masoko ya mazao ya chakula nayo ni muhimu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huu, Dira ya Maendeleo ya Taifa kuelekea mwaka 2025 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 zimetilia mkazo kwa Serikali kuendelea kuweka kipaumbele cha juu cha uwekezaji katika miundombinu, hususan ya barabara. Serikali za Awamu ya Tatu ya Mheshimiwa Benjamín Mkapa na ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete zimeendelea kutambua umuhimu wa barabara nzuri kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini, hasa kupitia sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Serikali ya Awamu ya Tatu, miradi 14 ya ujenzi wa barabara yenye jumla ya kilomita 1,226 ilianzishwa. Kati ya miradi hiyo, iliyokamilika katika kipindi hicho ni saba yenye jumla ya urefu wa kilomita 403. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete ilipoingia madarakani ilirithi miradi saba yenye urefu wa jumla ya kilomita 823 ambayo ilikuwa bado kukamilika. Kati ya miradi iliyorithiwa, jumla ya kilomita 803 tayari zimejengwa kwa kiwango cha lami kufikia mwezi Aprili, 2010. Hii ina maana kuwa hadi sasa miradi yote ya ujenzi wa barabara iliyorithiwa kutoka Serikali ya Awamu ya Tatu imekamilika kasoro kipande chenye urefu wa kilomita 20 kati ya Manyoni na Isuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete imeanzisha miradi mipya 27 ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 1745. Miradi hiyo, sasa inaendelea kutekelezwa katika hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maendeleo haya ya ujenzi wa barabara za lami yamepunguza kwa kiasi kikubwa kero iliyokuwepo ya usafiri wa barabara nchini. Sambamba na hatua hizo za ujenzi wa barabara mpya nchini kwa kiwango cha lami, Serikali ya Awamu ya Nne imeendelea kuzingatia umuhimu wa kuimarisha mtandao wa barabara zote nchini kwa kufanya matengenezo kwa viwango vinavyotakiwa kwa kuongeza Bajeti ya matengenezo ya barabara kupitia Mfuko wa Barabara. Mfuko huo uliimarishwa kwa kuuongezea fedha kwa asilimia 155 kutoka shilingi bilioni 85.74 mwaka 2006/2007 hadi shilingi bilioni 218.47 mwaka 2007/2008 na hali ya Mfuko imeendelea kuwa nzuri hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza kazi nzuri ambayo imefanyika hadi sasa, katika mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015, miradi 23 ya ujenzi wa Barabara Kuu kwa kiwango cha lami yenye urefu wa jumla wa kilomita 2,993 itatekelezwa. Sambamba na miradi hiyo, ukarabati mkubwa wa Barabara za lami zenye jumla ya kilomita 853 utafanyika kwa kutumia fedha za mkopo wa Benki ya Dunia. Aidha, fedha za Mfuko wa Barabara zitaongezwa ili kufidia pengo lililopo hivi sasa la mahitaji ya shilingi bilioni 435 kwa mwaka kwa ajili ya matengenezo ya mtandao wa barabara nchini kutoka kwenye wastani wa shilingi bilioni 260 kwa mwaka zinazotolewa hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuunganisha miji mikuu ya Mikoa kwa barabara za lami na Makao Makuu ya Wilaya zote nchini kwa barabara za changarawe ifikapo mwaka 2018, kulingana na mpango kabambe wa uwekezaji katika sekta ya usafiri na usafirishaji wa mwaka 2007. Hatua hizo zitachochea sana uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu na kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, uwekezaji katika kilimo kwa kuhamasisha sekta ya umma na sekta binafsi ni sehemu tu ya uhamasishaji tunaofanya katika uwekezaji kwa ujumla. Katika kipindi cha miaka 15 iliyopita Serikali imetekeleza mageuzi makubwa katika sera za kusimamia uchumi jumla ambazo zililenga katika kujenga uchumi wa soko na kuifanya sekta binafsi kuwa injini ya ukuaji wa uchumi. Kutokana na mageuzi hayo, Serikali ilijitoa katika shughuli za moja kwa moja za kufanya biashara na kujielekeza zaidi katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ya dola, ikiwemo kujenga mazingira mazuri ya sera na Sheria ikiwa ni pamoja na miundombinu ya msingi kwa ajili ya kuvutia wawekezaji na ukuaji wa sekta binafsi iliyo imara na endelevu. *(Makofi)*

Aidha, katika kipindi hicho, Serikali imetekeleza programu mbalimbali za kuleta mageuzi katika Sekta ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Usimamizi wa Fedha na Bajeti ya Serikali, Sheria, Utawala Bora pamoja na Sekta za Kitaaluma za Elimu, Afya, Maji na Ardhi. Programu zote hizi zimelenga kukuza uchumi na kuondoa umaskini,

pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini na kuvutia wawekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa programu hizo, kumekuwepo na mafanikio ya kuridhisha katika Ukuaji wa Uchumi na Uwekezaji. Kwa mfano, tangu mwaka 2000 hadi 2008 uchumi wetu umekua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 5 mpaka 7 kwa mwaka. Aidha, uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja umeongezeka kutoka dola za Kimarekani 150.86 milioni mwaka 1995 hadi dola za Kimarekani milioni 695.5 mwaka 2008. Pamoja na mafanikio hayo, bado kasi na kiwango cha ukuaji wa uchumi wetu pamoja na uwekezaji hakikidhi mahitaji na malengo ya kuondoa umaskini. Kasi ya ukuaji wa uchumi na uwekezaji inahitajika kuongezeka zaidi hasa katika kipindi hiki ambacho uchumi wa dunia umepata msukosuko wa kifedha na hivyo kuongeza ushindani wa kuvutia wawekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa tuliyopata awali katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, tangu mwaka 2007 kumekuwepo na mwenendo usioridhisha wa mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. Katika tathmini iliyofanywa na Benki ya Dunia mwaka 2009 kuhusu hali ya wepesi wa kufanya biashara katika nchi mbalimbali duniani, taarifa inaonyesha kuwa katika viashiria 10 vilivyotumika, Tanzania imeshika nafasi ya 131 miongoni wa nchi 183 zilizofanyiwa tathmini. Nafasi ya Tanzania mwaka huu ni ya chini ikilinganishwa na nchi jirani katika Ukanda wetu ambazo zimewekwa katika nafasi zifuatazo, Rwanda (67); Kenya (75); Zambia (90) na Uganda (112). (Makofi)

Aidha, taarifa za miaka ya nyuma zinaonyesha kuwa Tanzania ilishika nafasi ya 124 mwaka 2007 na nafasi ya 127 mwaka 2008. Nchi ya kwanza duniani kwa wepesi wa kufanya biashara na uwekezaji ni Singapore.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa viashiria kumi vilivyotumika kuandaa taarifa ya jumla ya wepesi wa kufanya biashara na nafasi ya Tanzania kwa kila kiashiria kuhusu hali ya ufanisi wa mazingira ya biashara na uwekezaji ikilinganishwa na nchi nyingine ni kama ifuatavyo:-

- (i) Uanzishaji wa Biashara 120;
- (ii) Vibali vya Ujenzi 178;
- (iii) Ajira ya Wafanyakazi 131;
- (iv) Usajili wa Rasilimali zisizohamishika 145;
- (v) Upatikanaji Mikopo 87;
- (vi) Ulinzi wa Wawekezaji 93;
- (vii) Ulipaji Kodi 119;
- (viii) Wepesi wa Biashara ya Nje 108;
- (ix) Kulinda Mikataba 31;
- (x) Usitishaji au Kufunga Biashara 113; na
- (xi) Wastani wa Urahisi wa Kufanya Biashara 131.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kufikirika kuwa inachukua siku 328 kupitia taratibu 22 tofauti kupata kibali cha kujenga ghala dogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari kuhusu mwelekeo wa kuendelea kushuka kwa Tanzania katika viashiria vya Kimataifa vya wepesi wa mazingira ya uwekezaji kufanya biashara nchini na kuona kuwa hauendani na juhudi kubwa za Serikali za utekelezaji wa mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii yanayoendelea kufanyika kupitia maboresho mbalimbali ya Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu; pamoja na utekelezaji wa programu mbalimbali za kissekta chini ya mpango wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile mwenendo huo hauendani na dhamira ya Serikali ya kuifanya sekta binafsi kuwa injini ya ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo endelevu nchini. Kwa maana hiyo, tangu mwezi Septemba, 2009 Serikali imeunda kikundi kazi cha Makatibu Wakuu ambacho kimesimamia uchambuzi wa vikwazo vilivyopo kwa lengo la kuchukua hatua za haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa hadi sasa kikundi kazi cha Makatibu Wakuu kimekamilisha kazi yake na kuandaa taarifa ambayo imewasilishwa Serikalini kwa hatua zaidi. Aidha, tayari Serikali imeanza kutekeleza baadhi ya hatua zilizopendekezwa ikiwa ni pamoja na taratibu za taarifa ya thamani za mali *(Property Valuation Report)* na kaguzi zinazofanywa na wataalam mbalimbali. Lengo la Serikali ni kufanya mapitio ya kina ya Sheria na Kanuni zinazochangia kuwepo kwa vikwazo vya uwekezaji na biashara hasa katika maeneo ya upatikanaji wa vibali vya ujenzi, kuanzisha biashara, kupata mikopo, ulipaji wa kodi, kuajiri wafanyakazi, uandikishaji wa rasilimali, kulinda mikataba na wepesi wa biashara ya nje hasa kurahisisha mchakato wa kupitisha na kugomboa mizigo bandarini na katika Vituo vya Forodha. Ninayasema haya ili Watanzania wote tuweze kuona uzito wa suala hili na kwa pamoja tuweze kubadilika na kurejesha hadhi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na marekebisho ya Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu ambayo yanahitajika kufanyika katika sekta zote, napenda kuisisitiza kuwa ili Tanzania iweze kupiga hatua katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, ni muhimu tujizatiti kikamilifu kukabiliana na changamoto zifuatazo:-

Kwanza ni kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara, reli na bandari pamoja na upatikanaji wa nishati nchini ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

Pili, ni umuhimu wa kuongeza ufanisi na kasi ya utekelezaji wa maboreshao yanayoendelea katika sekta ya ardhi; na eneo la uanzishaji wa biashara pamoja na maboresho ya mfumo wa usuluhishi wa migogoro ya kibiashara.

Tatu, ni kushughulikia suala la upatikanaji wa Vibali vya Ujenzi nchini ambalo limekuwa moja ya kiashiria kinachoonekana kuwa na urasimu mkubwa unaojumisha taratibu 22 zinazochukua wastani wa siku 328 ikilinganishwa na wastani wa siku 30

katika baadhi ya nchi zilizo na ufanisi na wepesi wa kufanya biashara na uwekezaji. Ili kupata ufumbuzi wa suala hili mapema, inabidi kuondoa nafasi ya Kamati za Madiwani katika Halmashauri katika kutoa vibali.

Nne, ni kubadili mitazamo ya Watumishi wa Umma katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kutoka katika fikra na mifumo ya udhibiti na kuwa na mitazamo na hulka za uwezesaji kwa wafanyabiashara na wawekezaji nchini na tano, ni kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kunakuwepo na mkakati endelevu wa kuboresha mazingira wezesaji ya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo mpya wa udahili wa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, changamoto zitokanazo na ongezeko la Vyuo Vikuu nchini ni nyingi. Moja ya changamoto hizo ni kuweka mfumo mzuri wa udahili wa wanafunzi ambao utapunguza gharama kwa vyuo na hata kwa wadhiliwa. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali kwa kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Vyuo vya Elimu ya Juu imeanzisha mfumo wa udahili wa wanafunzi wa vyuo vikuu na vya elimu ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfumo huu mpya wa udahili wa wanafunzi unazingatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yaliyotokea hapa nchini na duniani kote kwa ujumla. Aidha, mfumo huu unalenga kuondoa matatizo yaliyokuwepo katika udahili kama vile wanafunzi kudahiliwa na Chuo zaidi ya kimoja na hivyo kuziba nafasi kwa wengine wenye sifa kuachwa kudahiliwa; wanafunzi kudahiliwa kwa kutumia vyeti bandia au vya kughushi; wanafunzi kupangiwa na/au kupokea mkopo zaidi ya mmoja kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu; waombaji wanojiunga na elimu ya juu kuingia katika gharama kubwa kwa kulazimika kulipia fomu katika kila Chuo wanachoomba. Aidha, baadhi yao pamoja na wazazi wao husafiri masafa marefu ili kwenda kwenye vyuo mbalimbali wanakoomba udahili; vyuo kulazimika mara kwa mara kusogeza mbele kuanza kwa mwaka wa mosomo kutokana na matatizo ya udahili na vyuo karibu vyote kuendeshwa chini ya kiwango chake cha udahili, baada ya wanafunzi waliochaguliwa kuwa wamejiunga na vyuo vingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mfumo huu mpya waombaji watumia mtandao wa *internet* au simu zao za mkononi kutuma maombi ya udahili katika vyuo mbalimbali nchini. Waombaji wamepewa fursa ya kuomba udahili katika programu mpaka 12 kwenye vyuo mbalimbali. Kigezo pekee cha kudahiliwa ni ufaulu wa mwombaji katika masomo ya sekondari yaani katika kidato cha nne na cha sita kwa kulinganisha ufaulu wa waombaji wote wa programu husika na nafasi zilizopo. Matokeo ya mitihani ya waombaji yatapatikana moja kwa moja kutoka kwenye mtandao wa Baraza la Mitihani la Taifa bila waombaji kuhusika na kutuma vyeti vyao kwa ajili ya udahili. Hii itaondoa usumbufu kwa waombaji na kuondoa udanganyifu wa kutumia vyeti bandia katika kuomba udahili. Hii pia itapunguza gharama kwa mwombaji na usumbufu wa kusafiri kupeleka maombi kwenye vyuo mbalimbali kwa vile kwa mfumo mpya mwombaji anaweza kuomba udahili katika vyuo mbalimbali kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwaomba wanafunzi wanaotarajia kuomba nafasi katika vyuo vya elimu ya juu nchini waanze kujielimisha juu ya mfumo huu mpya wa udahili. Tume ya Vyuo Vikuu iwawezeshe wanafunzi hao kupata taarifa sahihi na rafiki juu ya matumizi ya mfumo huu. Itakuwa jambo jema ikiwa nanyi Waheshimiwa Wabunge mtaunga mkono matumizi ya mfumo huu kwa kuwahamasisha wanafunzi tarajiwa wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini katika Majimbo yenu kutumia mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapambano dhidi ya malaria na ukubwa wa tatizo, moja ya eneo ambalo Serikali ya Awamu ya Nne imeamua kulishughulikia ni mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria. Takwimu zinaonyesha kwamba wagonjwa wanaosumbuliwa na ugonjwa wa malaria ndiyo wanaongoza kwa mahudhurio ya mara kwa mara katika vituo vya huduma ya afya. Mahudhurio hayo ni asilimia 30 hadi 40 ya magonjwa yote. Wagonjwa takriban milioni 12 wa malaria huripotwa kufika katika vituo vya afya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, vifo vinavyotokana na malaria katika vituo vya afya ni kati 15,000 hadi 20,000 kwa mwaka hapa nchini. Hata hivyo, idadi halisi inakisiwa kuwa kubwa zaidi kati ya 60,000 na 80,000 sawa na asilimia 80 ya vifo vyote hapa nchini, kutokana na vifo vingi kutokea nje ya vituo vya afya. Asilimia 80 ya vifo ni vya watoto wadogo wenye umri chini ya miaka mitano na mama wajawazito. Kwa wastani malaria huua mtu mmoja katika kila dakika 5, sawa na watu 12 kila saa au watu 288 kila siku. Kwa mantiki hiyo ugonjwa huu ambao una kinga, ni mzigo mkubwa unaoelemea utoaji huduma za afya hapa nchini. Vilevile, inakadiriwa kuwa Tanzania hupoteza asilimia 3.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka kutokana na ugonjwa wa malaria. Gharama hii ni kubwa kwa Taifa. Kwa ufupi, malaria ni chanzo kimojawapo cha umaskini wa kaya, jamii na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inalenga kupunguza idadi ya wagonjwa na vifo vinavyotokana na malaria kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2013. Punguzo hilo ni sawa na kupunguza wagonjwa wa malaria kutoka milioni 12 hadi milioni 6 na idadi ya vifo kutoka kati ya 60,000 na 80,000 hadi kati ya 30,000 na 40,000 kwa mwaka. Lengo hili litaweza kufikiwa iwapo utekelezaji wa mikakati tuliyonayo ya kupambana na malaria utafikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati ya kinga na tiba ya malaria na mikakati mtambuka. Mikakati ya kinga inahusisha; matumizi ya vyandarua vyenye viutilifu, upulizaji wa viutilifu majumbani, matumizi ya dawa ya kujikinga na malaria kwa mama wajawazito, usafi wa mazingira na ujenzi wa nyumba bora zenye kuzuia mbu kuingia ndani ya nyumba hizo. Mikakati ya tiba ni pamoja na matumizi ya dawa mseto za kutibu malaria kama ALU badala ya dawa zilizopitwa na wakati. Mikakati mtambuka iliyopo ni pamoja na uelimishaji jamii ili iwe na uelewa mpana zaidi na kubadili tabia na mienendo yao ambayo ama inachangia tatizo la malaria au inadumaza juhudi za mapambano dhidi ya malaria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mikakati hii kumekuwepo na matokeo chanya. Kwa mfano; mwaka 2008 takribani asilimia 50 ya kaya hapa nchini zilikuwa na vyandarua vyenye dawa ya kudumu (NGAO). Kuanzia mwaka 2008, Serikali ilianzisha kampeni ya ugawaji bure vyandarua kwa watoto wenye umri chini ya miaka 5. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2010 watoto takribani milioni 9 walikuwa wameshagawiwa bure vyandarua vyenye dawa ya kudumu. Kampeni hii imekamilika katika Mkoa yote isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo kampeni inatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2010. Aidha, kuanzia mwezi wa Agosti, 2010 kampeni ya pili ya kugawa bure vyandaru milioni 14.6 itaanza nchi nzima na kila kaya itaongezewa vyandarua viwili au zaidi bure.

Mheshimiwa Spika, kampeni ya upulizaji wa viuatilifu majumbani ilianza Mkoa wa Kagera mwaka 2007 na hadi mwaka 2009 zoezi hili lilikuwa limekamilika katika Wilaya zote za Mkoa wa Kagera. Kampeni itaendelea katika Mkoa ya Mara na Mwanza kuanzia Agosti, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya mikakati mtambuka ni pamoja na kuanza kutolewa kwa elimu ili kuiwezesha jamii kubadili tabia zinazokinzana na mapambano dhidi ya malaria. Elimu hii imeanza kutolewa nchi nzima kupitia njia mbalimbali kama kupitia sanaa, vyombo vya habari na kwa njia ya mawasiliano ya moja kwa moja kwa walengwa. Kampeni ya Zinduka ambayo ilizinduliwa tarehe 13 Februari, 2010 na Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete inalenga kufikia lengo hilo. Mafanikio mengine ni kuwa wagonjwa wa malaria wanaokwenda kutibiwa katika vituo vya afya vya Serikali wanatibiwa bure au huchangia gharama kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya tunazo changamoto mbalimbali zinazoyakabili mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria nchini. Changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa dawa katika vituo vya huduma kila wakati, mama wajawazito kuchelewa kuanza kiliniki na uelewa wa kutosha wa mama mjamzito, mume na familia kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kupambana na malaria.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa wananchi kuwa wazingatie wanayoelemishwa kuhusu ugonjwa wa malaria. Mfano, matumizi ya vyandarua kila siku, usafi wa mazingira na ujenzi wa nyumba ambazo haziruhusu mbu kuingia ndani na kuwahi kwa daktari mara wanaposikia dalili za ugonjwa wa malaria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, huu ni mwaka wa Uchaguzi. Jukumu la Serikali ni lile la kuwezesha zoezi hili kufanyika kama linavyotarajiwa na wananchi wote. Kwa mujibu wa Sheria, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga kura mara mbili kati ya Uchaguzi Mkuu mmoja na unaofuata. Tume ilifanya Uboreshaji wa Daftari, Awamu ya Kwanza kuanzia mwezi Oktoba, 2007 hadi Desemba, 2008 ambapo Wapiga kura waliongezeka kutoka 15,935,493 na kufikia wapiga kura 18,014,667. Katika Uboreshaji huo, wapiga kura 806,170 waliweza kuhamisha taarifa zao au kupewa kadi mpya na wapiga kura 69,161 walifutwa kwa sababu za kifo. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, idadi ya wapiga kura iliyofikiwa hadi sasa ni watu 20,801,202. Idadi hiyo, itabadilika kidogo baada ya kukamilika kwa kazi inayoendelea ya uchambuzi wa fomu za Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam na pia zoezi la kuwaondoa wapiga kura waliopoteza sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa Awamu ya Pili ulianza mwezi Agosti, 2009 na kumalizika mwezi Machi, 2010 kwa Tanzania Bara. Hata hiyo, kutokana na wingi wa wapiga kura waliojitokeza katika mkoa wa Dar es Salaam, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina nia ya kuongeza siku mbili katikati ya mwezi Mei 2010, ili kukamilisha uboreshaji huo kwa mkoa wa Dar es Salaam. Zoezi hilo litafanyika baada ya kukamilisha Uchambuzi wa Taarifa za wote waliojiandikisha katika kipindi kilichopita. Kwa Tanzania Zanzibar, uboreshaji unategemewa kufanyika kati ya tarehe 31 Mei, 2010 na kumalizika tarehe 5 Juni, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa Awamu ya Pili utakuwa wa mwisho kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010. Hata hivyo, Tume inatambua kuwa wapo wapiga kura wachache kwa sababu mbalimbali watahitaji kuhamisha taarifa zao. Kwa mfano, wanafunzi ambao wamemaliza shule na kurudi nyumbani na wafanyakazi mbalimbali waliohama na kadhalika. *(Makofi)*

Aidha, wapiga kura wengine wanahitaji kutoa taarifa za ndugu zao waliofariki ili waweze kutolewa katika daftari. Kutokana na sababu hizo, Tume inakusudia kuruhusu marekebisho ya wale watakaokuwa wamehama kutoka Jimbo/Kata moja kwenda nyingine kufanyika katika daftari ambapo mpigakura anayehitaji kubadilisha taarifa zake atatakiwa aende mwenyewe kwa afisa mwandikishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, Tume haitafungua vituo vya kuandikisha wapiga kura kama ambavyo imekuwa ikifanyika wakati wa uboreshaji wa daftari katika awamu ya kwanza na pili. Zoezi hilo la wale waliohama litafanyika kuanzia tarehe 01 Julai, 2010 hadi 15 Julai, 2010 kwa Tanzania nzima kwa wakati mmoja ili kuruhusu kukamilisha daftari kabla ya uteuzi wa wagombea tarehe 19 Agosti, 2010. Nitumie fursa hii kusisitiza kwa wananchi wote kutumia vizuri fursa itakayotolewa kurekebisha taarifa zao kwenye daftari la wapiga kura kwa sababu Tume ya Taifa ya Uchaguzi haitatoa muda mwingine kwa ajili ya marekebisho hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuweka wazi daftari, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuweka wazi Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Mikoa iliyo kwenye Kanda ya Tano hadi Kanda ya Saba kuanzia tarehe 10 Mei hadi 4 Juni, 2010 ili kuwezesha Wapiga Kura kukagua Taarifa zao, kusahihisha na kuweka pingamizi. Mikoa iliyo kwenye Kanda hizo ni Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro na Dar es Salaam. Mikoa mingine ambayo ipo katika Kanda ya Kwanza hadi ya Nne tayari imekamaliza zoezi hili la uwekaji wazi wa Daftari kwa Ukaguzi. Mikoa hiyo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Kagera na Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha zoezi la kukagua daftari, Tume imeweka mfumo wa kukagua taarifa kupitia ujumbe mfupi wa maneno wa simu za kiganjani. Utaratibu huu unatarajiwa kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kupitia vipeperushi, redio, luninga, magazeti na pia utatumika na wasimamizi wa uchaguzi, siku ya uchaguzi pale ambapo taarifa za mpiga kura zinakosekana. Ninatoa wito kwa wananchi kutumia utaratibu huu kwani pia unaokoa muda wa kwenda kukagua taarifa zao katika Daftari la Kudumu la Mpiga Kura kwa ajili ya kujiandaa na zoezi la Kupiga Kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasihii Wapiga Kura kukagua taarifa zao katika kipindi hicho ili Tume ikamilishe masahihisho yote yanayohitajika kabla ya kuchapisha daftari lililo sahihi na litakalotumika wakati wa uteuzi wa wagombea na katika Uchaguzi Mkuu. Aidha, nitumie fursa hii kuipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kazi nzuri ambayo imeifanya hadi sasa katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba, Mheshimiwa Rais alitia saina Sheria ya Gharama za Uchaguzi tarehe 19 Machi, 2010. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imekwishatoa nakala ya Sheria hii pamoja na vipeperushi kwa vyama vyote 18 vyenye usajili wa kudumu. Vipeperushi vilivyotolewa vitawasaidia wananchi kujua masuala ya msingi wanayotakiwa kuyafanya na yale ambayo hawatakiwi kuyafanya chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Aidha, juhudi hizi zitakwenda sambamba na Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa kutoa elimu kwa umma nchi nzima kuanzia tarehe 30 Aprili, 2010 katika Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki na kumalizia katika Kanda zilizobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kanuni za Sheria ya Gharama za Uchaguzi, rasimu ya Kanuni ambazo zimetokana na Sheria ya Gharama za Uchaguzi zimekamilika baada ya kujadiliwa na wadau wakiwemo kutoka vyama vya siasa pamoja na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Hii ni pamoja na amri ambayo Waziri mwenye dhamana ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi anapaswa kuridhia kiwango cha juu cha gharama za uchaguzi kwa matumizi ya vyama vya siasa baada ya kupata maoni ya wadau. Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kujadili Kanuni hizo katika semina ya Wabunge itakayofanyika tarehe 24 Aprili, 2010 hapa Dodoma kwa ajili ya kupata maoni zaidi kabla ya kuwekwa saina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Aprili, 2010 Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilizindua rasmi elimu kwa umma ambapo kwa sasa Msajili wa Vyama vya Siasa amekwishaanza kutoa maelezo na ufafanuzi wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi na Kanuni zake kupitia vipindi vya redio na luninga pamoja na semina kwa lengo la kutoa elimu kwa umma. Natoa wito kwa wananchi wote kuzingatia masharti ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi kwa kuacha kufanya vitendo vyote ambavyo vimekatazwa na Sheria kabla na wakati wa mchakato wa Uchaguzi, ndani ya Vyama vya Siasa, wakati wa Kampeni na Uchaguzi kwani kwa kwenda kinyume, Sheria itachukua mkondo wake na

kuwaweka kando wale wote ambao watashindwa kutekeleza masharti ya Sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya mauaji ya walemavu wa ngozi na vikongwe, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuelezea tena hali ya sasa ya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi na vikongwe ikilinganishwa na tulikotoka. Tangu Oktoba, 2009 hadi sasa taarifa tulizo nazo ni mauaji ya mlemavu mmoja wa ngozi na wawili walijeruhiwa. Nawasihi Watanzania wote tuendelee kulaani vitendo hivi viovu na kuwataja wahusika ili wachukuliwe hatua za Kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya jitihada za hivi karibuni ambazo Serikali imechukua katika kuhakikisha tatizo hili la mauaji ya walemavu wa ngozi linadhibitiwa ni kutungwa kwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010 (*The Persons with Disabilities Act, 2010*). Muswada wa Sheria hii mpya umepitishwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge. Sheria hii kwa ujumla inatarajiwa kuwapatia watu wenye ulemavu, haki na usawa wa fursa katika nyanja zote za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kura ya maoni, mwezi Machi, 2009 zoezi la kura ya maoni lilifanyika kwa Mikoa yote Tanzania Bara. Jumla ya watu 97,736 walipigiwa kura kuwa wanahusika na makosa hayo. Upelelezi wa kina unaendelea kuhusu watuhumiwa na wale ambao ushahidi unapatikana wanafikishwa Mahakamani. Hadi sasa watu 3,217 wamefikishwa polisi, watu 295 wamefikishwa Mahakamani na watu 106 wamehukumiwa. Kati ya kesi zilizofikishwa Mahakamani, 11 ni za mauaji ya walemavu wa ngozi, kesi tatu zimetolewa hukumu na Watuhumiwa nane wamehukumiwa kunyongwa. Upelelezi wa matukio mengine 27 ya mauaji unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia vyombo vyake vya ulinzi na usalama pamoja na kushirikiana na wananchi bado inaendelea na juhudi za kupambana na wauaji wa watu wenye ulemavu wa ngozi na vikongwe. Juhudi hizo ni pamoja na kufuatilia kazi za waganga wa jadi, kuwashawishi wananchi kuwa na imani za kiroho, kuwekeza na kutoa elimu rasmi ili kupunguza imani za kishirikina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na nguvu zote na tatizo hili, uongozi wa Mikoa yote umeelekezwa kuhakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu katika kulinda maisha ya wananchi wetu ambao ni walemavu wa ngozi na vikongwe. Jeshi la Polisi nalo linaendelea kuchukua hatua za haraka kila mara linapopata taarifa kuhusu hatua zozote za kuhatarisha maisha ya walemavu wa ngozi na vikongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nirudie kuyasema haya tena hapa Bungeni kwa kuwa pamoja na hatua kali tulizochukua mauaji haya bado yanaendelea. Hatuwezi kukubaliana na hali hii. Napenda kusisitiza kuwa watu hawa ni binadamu wenzetu na wana haki ya kuishi kwa amani wakati wote. *(Makofi)*

Nawaomba viongozi wa dini kuendelea kuwaelimisha Watanzania juu ya vitendo hivi viovu, vinavyofanywa na wauaji hawa. Taasisi zisizo za Kiserikali nao waendelee

kutoa elimu dhidi ya vitendo katili kwa walemavu hawa na kuwasaidia kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii wakiwa huru. Waandishi wa habari na vyombo vyao nao waendeleo kuunga mkono juhudi hizi za Serikali. Nirudie kuwasihii waganga wa kienyeji waache kutumika kuchochea ukatili huo, wasiwadanganye watu kwani hakuna utajiri unaopatikana kwa kukata mkono wa binadamu mwenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikutano ya Kimataifa, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu naomba nitumie fursa hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa nchi yetu imepata heshima ya kuchaguliwa na Jumuiya ya Kimataifa kuwa mwenyeji wa Mikutano miwili mikubwa ya Kimataifa itakayofanyika mwezi Mei, 2010. Mikutano hiyo ni Mikutano wa Ishirini wa Kiuchumi wa Dunia kuhusu Afrika (*20<sup>th</sup> World Economic Forum on Africa 2010*) unaotarajiwa kufanyika tarehe 5 hadi 7 Mei, 2010, Mjini Dar es Salaam. Mikutano huo unafanyika kwa mara ya kwanza katika Ukanda wa nchi za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Aidha, Mikutano huo ambao utawakutanisha viongozi wa kada mbalimbali wa sekta ya umma na sekta binafsi kutoka Bara la Afrika na kwingineko na utajadili masuala mbalimbali yanayohusu kuboresha hali ya Kiuchumi kwa nchi za Afrika. *(Makofi)*

Mkutano mwingine ni ule Mikutano wa Mawaziri kuhusu Ushirikiano baina ya Nchi za Afrika na Japan maarufu kama *TICAD IV* ambao utafanyika kuanzia tarehe 2 hadi 3 Mei 2010, ili kujadiliana kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Mikutano wa Ushirikiano huo uliofanyika Yokohama, Japan mwaka 2008, kuhusu kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Mikutano hii pamoja na kufanikisha malengo yake, itatoa fursa ya kipekee ya kuitangaza nchi yetu na kuchochea sekta ya utalii na uwekezaji nchini. Aidha, itatoa fursa kwa wafanyabiashara kujiongezea kipato kutokana na kutoa huduma mbalimbali kwa wajumbe wa Mikutano huo. Hivyo, natoa wito kwa wananchi na sekta binafsi na wadau mbalimbali kushirikiana na Serikali kufanikisha Mikutano hiyo, na pia kutumia fursa zitakazojitokeza kutangaza vizuri vivutio vya utalii wa Tanzania na kuvutia uwekezaji, pamoja na kutoa huduma bora na nzuri kwa wajumbe wa Mikutano hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha Mikutano wa Kumi na Tisa wa Bunge tukiwa tumebakiza Mikutano mmoja tu kabla ya kuvunjwa Bunge na kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba, 2010. Napenda nirudie wito wangu kwa wananchi wote kuendelea kudumisha amani, utulivu na mshikamano. *(Makofi)*

Aidha, kwa kuzingatia changamoto mbalimbali ambazo zinatukabili katika kipindi hiki, mambo ya msingi ambayo ningependa kuyasisitiza ni haya yafuatayo:-

Kwanza, tunayo fursa nzuri ya kutumia watafiti tulionao nchini. Tujenge utamaduni wa kutumia tafiti mbalimbali zilizopo hususan katika kuendeleza kilimo. Tuendeleze juhudi za kukamilisha uboreshaji wa miundombinu ya utafiti ili watafiti waweze kufanya kazi zao vizuri.

Pili, mazingira wezeshaji ya biashara na uwekezaji ni muhimu sana katika kukuza uchumi na kujenga sekta binafsi imara, endelevu na yenye uwezo wa ushindani. Natoa wito kwa Wizara na Taasisi zote za Umma zinazohusika pamoja na Halmashauri kuangalia upya taratibu zinazohusu kuvutia wawekezaji na biashara ili kuondoa vikwazo vya kukuza uwekezaji na maendeleo ya sekta binafsi nchini.

Tatu, tumezindua mfumo mpya wa udahili katika vyuo vya elimu ya juu nchini. tuwahimiza wanafunzi wote wanaotarajia kuomba nafasi katika vyuo hivyo waanze kujielimisha juu ya mfumo huu. Tume ya Vyuo Vikuu iwawezeshe wanafunzi kupata taarifa sahihi juu ya matumizi ya mfumo huu.

Nne, bado tunazo changamoto mbalimbali kuhusu ugonjwa wa malaria. Tuendeleo kuelimishana kuhusu ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na matumizi ya vyandarua kila siku, usafi wa mazingira na kumuona daktari kwa matibabu mara unaposikia dalili za malaria. Tano, mweleko wa viashiria vya Kimataifa vya wepesi wa kufanya biashara na mazingira ya uwekezaji nchini hauendani na juhudi tunazowekeza katika maboresho ya sera za kiuchumi katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Tuongeze juhudi katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sita, hadi sasa maandalizi yote kwa ujumla kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu yanaendelea vizuri. Tume ya Taifa ya Uchaguzi imejipanga vyema kukamilisha zoezi zima la Uchaguzi Mkuu kwa mafanikio. Pamoja na kuipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kazi nzuri ambayo imeendelea kufanyika hadi sasa, tuwahamasishe wananchi wote kufuata maelekezo ya Tume na kushiriki katika maandalizi haya ili kuepuka uwezekano wa kukosa haki ya msingi ya kupiga kura.

Saba, Sheria ya Gharama za Uchaguzi imekamilika na utekelezaji wake utaanza katika kipindi hiki tunapoelekea katika Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2010. Tuwahamasishe wananchi kuzingatia masharti ya Sheria hii wakati wa mchakato wa Uchaguzi ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kwa kushindwa kutekeleza masharti hayo. Tuwahimiza kutoa ushirikiano kwa wataalam watakaokuwa wanatoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa Sheria hii na Kanuni zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nane, bado tunalo tatizo kubwa la ajali za barabarani ambazo zinasababisha vifo na upotevu wa mali. Narudia kutoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri na madereva kuwa makini katika matumizi ya vyombo vya usafiri. Aidha, napenda kuisisitiza kwamba taasisi zinazosimamia masuala ya usafiri wa barabarani wakiwemo polisi wa usalama barabarani na *SUMATRA* waongeze juhudi za kusimamia kikamilifu Sheria na kuchukua hatua zinazostahili ili kudhibiti ajali za barabarani ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwashukuru tena wote waliotusaidia katika kufanikisha Mkutano huu. Shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika kwa umahiri wako katika kuliongoza Bunge hili kwa kasi na viwango vya Kimataifa. Vilevile, namshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti kwa kutuongoza vizuri.

Niwashukuru Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu na kukubali kupitisha Miswada mbalimbali na Maazimio yaliyowasilishwa katika Mkutano huu. *(Makofi)*

Namshukuru Katibu wa Bunge na wasaidizi wake kwa huduma mbalimbali katika kufanikisha Mkutano huu. Wapo wataalam wa Serikali, madereva na vyombo vya habari ambao wote kwa pamoja ninawashukuru kwa kutimiza wajibu wenu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa siwatendei haki wapiga kura wa Jimbo langu la Mpanda Mashariki kama sitatumia fursa hii kuendelea kuwashukuru kwa kuendelea kuniunga mkono na kutambua dhamana kubwa niliyobebeshwa na Taifa na hivyo kunivumilia kwa muda wote, naomba pia kumshukuru sana mke wangu Mama Tunu Pinda na watoto wote kwa kuwa wavumilivu na watu wenye kuniunga mkono na kunipa faraja kila wakati nilipopata msongo kutokana na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawatakia wote safari njema wakati mnaporejea katika Majimbo yenu. Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu kuwa liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 8 Juni, 2010 saa tatu kamili asubuhi, litakapokutana hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru na kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako hiyo ambayo ni wazi ina maelekezo bayana ya kazi na changamoto zinazotukabili. Lakini zaidi nikupongeze kwa sababu kiu cha Wabunge kuipata hotuba na kwenda nayo nyumbani umekitimiza. Sasa hivi tunawapongeza sana waliohusika na juhudi hizo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naoungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kama nilivyosema siku za nyuma jumba hili ni darasa kubwa sana. Mkusanyiko uliomo humu wa watu wenye busara na hekima na uzoefu sijui kama unaweza kuupata mahali pengine popote katika nchi yetu. Kwa hiyo, kuwemo humu ni aina fulani ya bahati na kwa hilo ninawashukuru sana. Mimi mwenyewe naendelea kujifunza na tuzidi kutakiana heri ili Mungu atukutanishe tena kwenye Mkutano wa Ishirini ukiwa ni Mkutano wa mwisho. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo sasa naomba wote tusimamae kwa ajili ya Wimbi wa Taifa. *(Makofi)*

Hoja haijaamuliwa kweli nilisahau, Waheshimiwa Wabunge, mbele yetu ipo Hoja ya Kuliahirisha Bunge imetolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na imeungwa mkono na sasa wajibu wangu ni kuwahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wanaliosema siyo ah! Walewale tu kila siku, walioafiki wameshinda.  
*(Makofi)*

Kwa hiyo sasa niwaombe tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliimba wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa natangaza kwamba tunaliahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne, tarehe 8 Juni, 2010 saa tatu asubuhi hapa Dodoma. *(Makofi)*

*(Saa 3.20 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 8 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*